ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Tano - Tarehe 20 Juni, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

TAARIFA

Mhe. Spika: Naona Waheshimiwa Wajumbe leo kuna vijana wenu wengi tu na vijana hawa ni wageni ambao wapo pale juu. Kwa hiyo nataka nikujulisheni kwamba nakuombeni Waheshimiwa Wajumbe muwatambue wageni wetu waliopo katika ukumbi wetu wa juu ambao ni wanafunzi wa darasa la saba kutoka Skuli ya Kajificheni ilioko katika Jimbo la Mji Mkongwe mwenyewe hayupo.

Jumla yao wanafunzi 67 hawa wamefuatana na walimu wao ambao ni watatu na naomba wote wasimame. Tunamshukuru Mhe. Mwakilishi wa Mji Mkongwe kutuletea vijana wake ili kuja kuona shughili zetu japo mwenyewe hayupo, lakini ujumbe utamfika kwamba wageni wapo hapa kabla ya mwenyewe kufika. Nakushukuruni ahsanteni.

MASWALI NA MAJIBU

Nam 69

Uboreshaji wa Mazingira ya Baraza la Wawakilishi ili liwe Rahisi kwa Walemavu Kutumia

Mhe. Saleh Nassor Juma Aliuliza:-

Baraza la Wawakilishi Zanzibar *Legislature* ni moja kati ya mihimili mikuu ya nchi na kwa kuwa kila mwananchi anayohaki ya kushiriki moja kwa moja au kupitia uwakilishi ndani ya chombo hiki bila kujali maumbile, rangi, kabila au jiografia mtu anakotoka. Kwa kuwa kila mjumbe ana haki ya kushiriki katika mijadala ya Baraza hili na kwa kuwa miundombinu hairuhusu kwa baadhi ya wananchi wenye ulemavu kufuatilia na kushiriki katika mijadala hata maandiko yatolewayo na Baraza hili.

(a) Ni lini Serikali itaanzisha rasmi maandishi ya Baraza ikiwemo majarida kwa njia ya “maandishi nundu” yaani *Breilled*.

(b) Kwa kuwa jengo la Baraza ni jipya halikuangalia mahitaji ya walemavu. Je, kuna uwezekanao wa kulifanyia marekebisho ili liende sambamba na mahitaji ya watu hao.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika**,** kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 69 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Ofisi yangu kupitia Baraza la Wawakilishi Zanzibar imekuwa ikichukua hatua mbali mbali ili kuwawezesha wananchi kufuatilia na kushiriki katika mijadala ya Baraza. Miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais katika kupata wataalamu wa lugha kwa ishara ambao kwa muda sasa wakitoa huduma ya kutafsiri mijadala hiyo kwa ishara kwa ajili ya kuwawezesha wenzetu wenye ulemavu waweze kufuatilia mijadala inayofanyika katika Baraza Tukufu.

Mhe. Spika vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-, baada ya maelezo hayo, naomba sasa nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye

(a) Mhe. Spika, suala la kuwepo kwa majarida na machapisho mengine kwa njia ya maandishi nundu linahitaji kwanza kufanyiwa utafiti hasa kwa kuangalia kama tunao wataalamu wa kutosha wa kufanya shughuli hiyo. Endapo uwezekano utakuwepo Ofisi yangu kwa kushirikiana na taasisi nyengine, haitakuwa na kipingamizi kuanzisha utaratibu huu.

(b) Mhe. Spika, ni kweli kuwa jengo la Baraza l;a Wawakilishi halikuzingatia kwa kina mahitaji ya baadhi ya walemavu. Hata hivyo ushauri tunaupokea ili tuufanyie kazi kitaalamu na endapo muundo wa jengo uliopo sasa unaweza kuruhusu marekebisho hayo basi Ofisi yangu kupitia Afisi ya Baraza la Wawakilishi, itaangalia uwezekano wa kufanya marekebisho hayo ili kuwawezesha watu wenye ulemavu kushiriki kwa karibu zaidi katika mijadala ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na majibu mazuri sana aliyoyatoa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, naomba niulize swali dogo tu la nyongeza:-

Mhe. Spika, kwa kuwa Katiba yetu hii ya Zanzibar na hata ile ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaeleza wazi juu ya usawa wa binadamu kila pahala hata pale mbele ya sheria kwamba binadamu wote ni sawa bila ya kujali ulemavu wao na wapi wanatoka wote ni sawa.

Kwa kuwa haki ya kushiriki pamoja na kupata taarifa za Baraza ni haki ya kila Mzanzibari na Mtanzania kwa jumla na kwa kuwa ndio kwanza Ofisi yako inafanya utafiti katika kuweza kuanzisha hayo maadishi *breilled*. Tangu Baraza hili lianzishwe katika miaka 80 mpaka leo hii watu wenye ulemavu wa macho wanakosa kupata taarifa za majarida yanayotolewa katika Baraza pamoja na kushiriki vile vile ndani ya Baraza hili, kwa maana ya wale walemavu wa macho hawapati aidha kushiriki au kupata taarifa za ndani ya Baraza kwa yale maandishi yao ya kupapasa, na kwa kuwa haki ikichelewa kutolewa ni sawa sawa na kuwa haikutolewa kabisa.

(a) Je, hamuoni kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar toka 64 mpaka leo imewanyima haki Wazanzibari wa ulemavu wa macho.

(b) Je, katika hili Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iko radhi kuwaomba radhi walemavu hawa wa macho na wale wa mambo ya miguu ambao wanashindwa kufika hata hapo juu kupata haki za msingi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais- Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma swali lake lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

Kwanza niseme kwamba Mhe. Saleh Nassor Juma anapenda kunipambanisha na kunigombanisha na watu muhimu sana katika nchi hii. Mhe. Spika, sisi katika Serikali tunaamini haki, usawa wa binadamu wote na Serikali yetu haina nia wala haitokuwa na nia wa kumbagua yeyote, walemavu ni wenzetu na hakuna mkamilifu katika dunia hii ukiwa bado uko hai tumuombe Mwenyezi Mungu atusitiri lakini lolote linaweza kutokea katika maisha.

Kwa hivyo, hatuwezi kabisa kumdharau ama kuwakosesha haki yao. Hivyo, nia ya Serikali kufanya kila jitihada kuhakikisha ndugu zetu hawa wanapata haki zao zote za msingi ikiwemo na kupata taarifa zinazotokana na Baraza hili Tukufu.

Nakubali Mhe. Spika, kwamba ni kipindi kirefu toka lianzishwe Baraza hili na hatukuweza kuchukua hatua stahiki za kuwawezesha walemavu wote kupata fursa stahiki inayotakiwa. Lakini nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi na wananchi wetu wa Zanzibar kama tutachukua kila jitihada kuhakikisha kwamba inafanya kila liwezekanalo ili wenzetu hawa waweze kupata taarifa stahiki zinazotokana na Baraza hili.

Mhe. Spika, naomba sana kabisa wenzetu hawa watusubirie wavute subra kwa sababu tunalijua na linatusikitisha, linatusononesha lakini ni hali halisi ya uchumi wetu, tutafanya kila jitihada tulimalize tatizo hili.

Nam 42

Uhaba wa Eneo Maalum la Biashara Zanzibar

Mhe. Viwe Khamis Abdalla- Aliuliza:-

Kwa kuwa tatizo la ajira kwa vijana limekuwa kubwa sana na hivyo husababisha vijana hao kuamua kujiajiri wenyewe kwa kufanya biashara.

Je, Wizara haioni kuwa muda umefika halmashauri zetu kutenga sehemu maalum kwa ajili ya biashara kwa vijana ili kuondosha msongomano mkubwa uliopo hapo Darajani.

Mhe.Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi -Alijibu:-

Mhe. Spika**,** naomba kumjbu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 42 kama ifuatavyo:-

Nakubaliana kabisa na ushauri uliotolewa na Mhe. Mwakilishi wa kutafuta eneo maalum kwa ajili ya biashara kwa vijana. Kwa kuanzia, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Baraza la Manispaa limetenga eneo maalum la Saateni kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo wadogo ili kupunguza msongamano mkubwa uliopo Darajani. Eneo hilo ni la Saateni ni la wazi kama ilivyo eneo la Darajani na kuna milango 25 ya maduka ambayo kwa sasa haijahamiwa na wafanyabiashara. Juhudi zinaendelea kuchukuliwa za kuwashajihisha wafanyabiashara ndogo ndogo ambao wanasababisha msongamano mkubwa katika eneo la Darajani ili waweze kuhamia katika eneo maalum lililotengwa hapo Saateni kwa ajili yao.

Mhe. Spika, ukienda Saateni hivi sasa utakuta nafasi nyingi tu tena nyengine wenyewe walikwisha kwenda wakajenga miundombinu lakini kwa utashi wao wenyewe wakahama na kuja Darajani kuleta msongamano huo. Kwa hivyo, naungana na Mhe. Mwakilishi kuwaomba wafanyabishara hawa wote wadogo wadogo ambao hawana nafasi Darajani basi kwa kuanzia turudi Saateni tukaendeleze biashara zetu. Wakati Serikali ina mpango mwengine wa kuiendeleza Darajani.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, kabla ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku hii ya leo kufika hapa kwa hali ya afya na uzima.

Mhe. Spika, kwa kuwa wananchi hawa wameteseka siku nyingi na kwa kuwa bado soko la Saateni halijaridhisha, je, atakubaliana na mimi Mhe. Waziri kwamba ni vyema wakapitia upya na wakahakikisha kwamba linapangwa ipasavyo ili tubadilike na mfumo ule tulionao wa maturubali, madude mabovu, atakubaliana na mimi hivyo?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa kuwa mimi sikubaliani nae Mhe. Asha Bakari Makame. Utaratibu umewekwa soko limetengenezwa Saateni, nafasi zimewekwa watu walikwenda wakaanza biashara wakahama wakarudi Darajani kuja ku-*block* nafasi za kupita daladala na kuja ku-*block* Skuli ya Vikokotoni na Skuli ya Darajani. Leo wanatundika vitu mpaka kwenye madirisha ya madarasa watoto wanaosoma wanawakera. Sasa nafikiri Mhe. Spika, hilo halikubaliki.

Suala la msingi sisi Serikali kama nilivyosema tunaandaa utaratibu wa kupaendeleza Darajani kwa kuwa- *accommodate* hawa wafanyabishara wote ambao tunahisi watapatiwa nafasi.

TAARIFA

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, sikusema soko la Darajani nimesema soko la Saateni kwamba atakubaliana na mimi kuna haja ya kubadilika kwa ule mfumo wa maturubali mabovu matakataka haukupangika vizuri. Atakubaliana na mimi kwamba Aende akakague na akaangalie ili tuweke mfumo mzuri.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri mmetofautiana na Mhe. Asha Bakari Makame katika swali na jibu.

Mhe.Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, niseme tena kwa mtizamo Mhe. Asha Bakari Makame bado sikubaliani nae na inaelekea hajenda huko Saateni kupaona palivyo. Mhe. Spika, Saateni kumepangwa vizuri, vile vibanda vimepangwa vizuri na wenyewe wamejenga vibanda vivuli hakuna mabadiliko yoyote naona ni utashi tu wa watu wameona waondoke kule waje Darajani.

Sasa ninachosema kama mapungufu Serikali tutajitahidi hayo mapungufu kuyaweka sawa. Pale mapungufu ya Saateni kuyaweka sawa ili washajihike zaidi wabaki pale. Lakini sio kuondoka Saateni kwa kisingizio hicho hicho alichosema Mhe. Asha Bakari Makame. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza.

Kwa kuwa askari wetu ni walinzi wa wananchi wetu kwa kuwalinda pamoja na mali zao, na swali mama alisema kwamba vijana wetu hawana ajira vijana walioko Darajani wamejiari kwa biashara zao ndogo ndogo.

(a) Mhe. Spika, askari wetu huenda pale na vijana wetu kukimbia na mali zao kuchukuliwa je, huoni hilo ni tatizo?

(b) Mhe. Spika, kwa kuwa inasemekana vijana wetu hawa hufurushana na askari ishafikia hadi kutupiana mawe. Je, hamuoni ni kuwafundisha utundu vijana wetu katika hali ya Zanzibar ambayo hii hali haistahili?

Mhe.Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, sijui kama nimempata vizuri lakini nilitaka kusema si nia wala si lengo la Serikali yetu kwamba vikosi vyake vya ulinzi na usalama kwenda kufukuzana na wananchi hasa wafanyabiashara. Sisi lengo letu wafanyabiashara kila mmoja afanye biashara pale panapostahiki kwa salama na amani.

Lakini baya Mhe. Spika, inapofika kwamba lazima vyombo vya ulinzi na usalama vitumie pale tena unapokhalif sheria na unaambiwa, unabembelezwa unaombwa husikii kidogo haipendezi, hapo tena ndio vyombo vya ulinzi na usalama inabidi viingilie lakini si nia yetu. Kwa hivyo, tatizo hili ni dogo sana tu tusichoke tufuate taratibu zilizowekwa na Serikali basi.

Kama pale Darajani pale wameona kuwa wako wengi hapatoshi wanajumuiya yao wakasema wanataka kujenga *shopping mall* wakaleta wazo hilo Serikalini na tumelifanyia kazi Serikali na tumeifanyia kazi, sasa huu ndio uungwana. Lakini ikiwa unafanya fujo na unagombana na askari unawatupia mawe haipendezi, sasa hawa na wao kama binadamu lazima wahisi.

Nam 82

Jaa la Eneo la Vitongoji Makaani

Mhe. Saleh Nassor Juma- Aliuliza**:-**

Kumekuwa na uchafuzi mkubwa wa mazingira unaofanywa na Baraza la Mji wa Chake Chake kwa kufanya jaa katika eneo la Makaani Vitongoji jambo ambalo limezalisha nzi wengi na kusababisha maradhi ya kuhara na kutapika katika vijiji vilivyoko karibu na jaa hilo, kama vile Udusini, Kibokoni,

Matunguu, Kisiwani, Vumba, Changuo na Darajani. Kwa kuwa taka hizo hazina udhibiti na zinaachiwa kuzagaa na hatimae watoto kuchezea jambo ambalo linazidi kuathiri afya za wananchi wa vijiji hivyo.

(a) Je, Serikali inayo taarifa hiyo.

(b) Kama Serikali inayo taarifa hiyo ni hatua gani za kisheria na kimazingira zilizochukuliwa ili kunusuru afya za walipa kodi hao

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rai - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako, na kwa heshima kubwa na unyenyekevu naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 82 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi inayo taarifa kwamba Makaani Vitongoji kuna eneo la mashimo ambalo limetumika kwa ajilii ya kutupa taka za maeneo ya Mji wa Chake- Chake, taarifa hiyo Serikali inayo.

b) Katika kukabiliana na tatizo hilo hatua zilizochukuliwa na Idara ya Mazingira Pemba kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ni kama ifuatavyo:-

“Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imelitaka Baraza la Mji wa Chake Chake kutafuta eneo jengine la kutupa taka taka na kuachana na eneo hilo kwa ajili ya kulinda afya ya wananchi wetu. Kwa taarifa tulizonazo, Baraza la Mji wa Chake-Chake linaendelea kushirikiana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kuweza kuzifukia taka zote zilizokuwepo katika jaa hili na kwa asilimia kubwa taka hizo zimeshafukiwa na kazi ya mwisho mwisho ilikuwa inamaliziwa. Lakini pia Mhe. Spika, Ofisi ya Ofisi ya Makamo wa kwanza wa Rais kupitia Idara ya Mazingira Pemba ilikubaliana na Baraza la Mji wa Chake-Chake kwa kushirikiana na uongozi wa Shehia za Vitongoji na Shehia ya Kibokoni pamoja na Jumuiya isiyo ya Kiserikali ya kuhifadhi mazingira ya Vitongoji *VECA* kutafuta eneo jengine la kutupa taka.

Mhe. Spika, nina furaha kumueleza Mhe. Mwakilishi kwamba siku wa Mazingira duniani katika kuiadhimisha siku hiyo huko Pemba siku ya tarehe 5/6/2013 shughuli iliyofanyika pale kwanza ni kuweka usafi katka jaa ambalo limehamwa na tayari jaa hilo sasa limehamishiwa katika eneo jengine la Vitongoji kunakoitwa Kwa Mtora.

Mhe Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, kwa kuwa taarifa inaonekana imepewa wizara yake si ya uhakika kwa sababu anasema kwamba kuna

mashimo ambazo taka zinatupwa kwenye mashimo. Lakini kumbe taka zimekuwa zikitupwa juu tu hivi na kuzagaa na kusababisha nzi wengi, jambo ambalo kama lilivyoelezwa katika swali la msingi limesababisha wananachi wengi kuugua matumbo pamoja na kuharisha. Na kwa kuwa kwenye kipindi chote hiki cha kuugua matumbo Serikali ya Shehia pamoja na Diwani walikuwa wanasafirisha wagonjwa kutoka Uwandani kupeleka Vitongoji, na Vikunguni kwa mgharama zao, kwa sababu suala hili ni uzembe na Baraza la Mji na kwa kuwa wagonjwa wale wamekaa mpaka mwezi mmoja na nusu wengine wameshindwa kusaidiwa na familia zao pamoja na kuweza kulipa kodi kwa ajili ya maendeleo ya nchin hii.

(a) Je, wizara yake na kwa kushirikiana na Wizara inayoongozwa na Mhe Mwinyi Haji Makame wako tayari kulipa fidia katika kipindi chote walichougua wale wagonjwa pamoja na kurejesha gharama walizotumia kwa Diwani na Masheha wa Shehia mbili zile .

(b) Kwa kuwa ugonjwa ule umesababishwa na uzembe kwa sababu hawajafahamu taka zitupwe kwenye shimo wao wakatupa juu ni hatua gani za kisheria itakayochukuliwa kwa uongozi wa Baraza la Mji ili kuweza kutenda haki kutokana na uzembe aliowafanyiwa wananchi wa Vitongoji.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

(a) Mhe. Spika, awali ya yote napaenda kuwashukuru sana Serikali na Shehia lakini pia na ndugu yetu Diwani kwa kushirikiana na wananchi pale yalipokuwa yanatoke matatizo na kuweza kuwasaidia wananchi kuondokana na matatzio. Hii ndio kazi ya viongozi tunawapongeza sana.

Mhe. Spika, suala la kulipwa fidia ni suala ambalo linahitaji kufanyiwa utafiti wa kisheria. Kwanza kuchunguzwa pamoja na haya anayoyaeleza ukubwa wa tatizo lenyewe na kama baada ya kukaa pamoja taasisi zinazohusika ikithibitika kwamba kunahitajika kisheria kulipwa fidia Serikali haitakuwa wazito kulifanya hilo.

Mhe. Spika, lakini kwa kadri ninavyoelewa Serikali imesimama kidete kwa pamoja kuona kwamba tatizo lile linaondoka na sasa pahala hapo ni safi na jaa limehamishiwa katika eneo ambalo liko mbali sana na makaazi ya wananchi na hata kama litatokea tatizo la taka kuto kutumbukizwa ndani ya shimo ambalo liko hapo basi hakuna wananchi ambao wataathirika. Tumefanya hivyo makusudi kwa ajili ya kulinda afya ya wananchi wetu.

(b) Mhe. Spika, hili la pili linakwenda na la kwanza pia ulipaji wa fidia na kuona kwamba Baraza la Mji litawajibika kushitakiwa. Haya ni masuala ya

kisheria naomba wale waliohusika kwa kuwa yanahusika kisheria inabidi yapelekwe mahakamani ili kama kuna suala ambalo la kisheria mahakama nayo iweze kuamua.

Nam. 16

Ufunguaji wa Chuo cha Mabaharia

Mhe. Fatma Mbarouk Said- Aliuliza**:-**

Kwa kuwa vijana wengi wameamua kujiingiza katika ajira ya ubaharia. Je, kuna juhudi gani za Serikali katika kufungua Chuo cha Ubaharia Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 16 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Serikali ni kweli iliona umuhimu wa kupatikana Chuo cha Ubaharia hapa Zanzibar. Kwa hivyo, mnamo mwaka 2011 iliunda tume kutokana na Kampuni inayoitwa *Danaos* ikishirikiana pamoja na wadau wengine wa vyombo vya baharini pamoja na wizara yetu kupitia Mamlaka ya Usafiri Baharini, waliandaa utaratibu maalum wa kuanzishwa kwa chuo hicho. Lakini mnao mwaka 2012 kulijitokeza dalili nzuri ya kuwa na wawezekaji zaidi ya mmoja aliyeonesha dalili ya kuanzisha chuo hiki. Kwa hivyo, katika mwaka huu wa 2013 tulibadilisha msimamo na kuweka msimamo kuwa sasa chuo hiki kipitie *ZIPA* kama mwekezaji, kwa sababu kiweze kuruhusu kuanzishwa kwa zaidi ya chuo kimoja kama watatokeza ambao wanahitaji kuekeza katika chuo hiko. Kwa bahati nzuri mpaka sasa hivi kampuni mbili zilijitokeza na zote zimo katika matayarisho kwa kupitia *ZIPA* na tunategemea muda sio mrefu, sisi tunatoa ushirikiano kikamilifu kupitia Mamlaka ya Usafiri Baharini ili chuo hiki au kampuni hizi zilizojitokeza ziweze kupata usajili na ziweze kuanzisha chuo hicho. Ni dhahiri kwamba Zanzibar kama ni visiwa vinahitaji chuo hivyo kwa sababu tuna ukosefu mkubwa wa ajira kwa vijana wetu, lakini tuna vyombo vingi vya usafiri na tunaweza kupata hata ajira za nje nyingi zaidi, tukiweza kuwa na chombo hicho. Kwa hivyo, kwa niaba ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, namshukuru sana Mhe. Mwakilishi kwa kuweza kuuliza swali hili ambalo ni muhimu kwa kuongeza ajira kwa vijana wetu.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama

hivi ifuavyao. Kwa kuwa vijana wengi wanafanyakazi ya ubaharia na kwa sasa kazi hii imekumbwa na uharamia na kusababisha kupoteza maisha.

a) Je, ni Wazanzibari wangapi waliokumbwa na kadhia hii.

b) Serikali imesaidia vipi familia za watu waliofikwa na kadhia hiyo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, swali lake Mhe. Mjumbe kidogo alirudie, lile la mwanzo.

Mhe. Spika: Rudia swali la mwanzo.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Kwa kuwa vijana wengi wanafanyakazi ya ubaharia na kwa sasa kazi hii imekumbwa na uharamia.

a) Je, ni Wazanzibari wangapi wamekubwa na kadhia hiyo ya kukumbwa na uharamia.

b) Serikali imezisaidia vipi familia za watu waliokumbwa na kadhia hiyo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwa kweli ni vijana wangapi waliokumbwa na uharamia, huo ni utafiti ambao kwa sasa nitakuwa sina takwimu sahihi. Kwa hivyo, inabidi turudi kwa sababu vijana wengi wanaokwenda nje, bahati ni kwamba hawapitii mlango wa serikali, wanakwenda nje kwa kupitia taratibu zao wenyewe. Kwa hivyo sio rahisi kuweza kutambua moja kwa moja jambo ambalo liko katika mikono yake yenyewe binafsi.

Lakini kama nilivyosema chuo hiki cha ubaharia kikianzishwa itakuwa hao vijana wanasoma hapa, wanasajiliwa hapa hapa na wanapewa zile taarifa kamili zitakuwepo serikalini. Sasa ndio nikasema ule umuhimu wa kuwa na Chuo cha Ubaharia hapa, hizo taarifa zitapatikana. Ama hawa waliokwenda nje kupitia sehemu mbali mbali na kupata ajira zao binafsi.

Mhe. Spika, hata hivyo utafiti utafanywa na *Inshaallah* tutaleta mbele ya Baraza lako tukufu kwa maandishi utafiti huu utakapokamilika.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, hivi karibuni katika vyombo vya habari mbali mbali viliripoti kuwa Watanzania Wazanzibari ambao ni

mabaharia katika nchi ya Brazil, walikamatwa kwa kujihusisha na masuala ya madawa ya kulevya.

Je, taarifa hizi ni kweli na kama ni kweli hao waliokamatwa ni Wazanzibari halisi au ni Watanzania waliopitia hapa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwa kweli sisi sio dhamana wa vijana ambao wako nje wanaojishughulisha na mambo mbali mbali. Hii ni idara maalum ya usalama ambayo zaidi ni mambo ya uhamiaji ndio wanaojua taratibu zake. Kwa hivyo, kwa njia hiyo siwezi kumpa takwimu yoyote au uhakika wowote kwamba hayo ni sahihi au sio sahihi, kwa sababu sio shughuli ambayo hasa tunafanya sisi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Mhe. Spika, Mhe. Waziri amesema kwamba serikali ina malengo ya kujenga Chuo cha Mabaharia hapa Zanzibar, ili kuwapatia vijana wetu na kuweza kusaidia serikali mzigo mkubwa wa ajira tulionao.

Mhe. Spika, hivi karibuni wapo vijana Wazanzibari ambao wameamua kusoma fani hii ya ubaharia, katika Chuo cha DMI Dar es Salaam. Wakati wanaendelea na masomo yao walitolewa nje ya chuo kwa ajili ya kufanya kazi ya vitendo, yaani *field work*. Sasa walipoamua kufanya kazi hizi za vitendo, waliamua kufanya kazi hizo katika Meli ya MV Maendeleo, lakini serikali ilikataa kuwapatia nafasi hizo vijana wale, kwa sababu kuna wa mazoezi ya vitendo. Badala yake MV Serengeti wakaamua kuwabeba vijana wale wote.

Mhe. Spika, ni kwa nini meli ya serikali ambapo malengo yake ni kuwaboresha vijana, ilikataa kuwapatia nafasi vijana wetu na meli ya binafsi ya MV Serengeti kuwapatia.

b) Kwa msingi huo huoni kwamba kama serikali haina nia ya kuwanasua vijana wetu katika fani hiyo ya ubaharia.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nashukuru kupata swali hili kutoka kwa Mwakilishi.

Mhe. Spika, naomba kwa ruhusa yako aniletee hizi taarifa kamili kwa sababu mimi mwenyewe binafsi mpaka hivi sasa sijapata kwa maandishi au kwa manung'uniko ya mdomo. Namuhakikishia kwamba ikiwa hivyo ndivyo ilivyo kama alivyosema basi tutaifanyia kazi kikamilifu, kwa sababu wale ni

vijana wetu na wana haki ya kupata nafasi za kufanya mazoezi katika vyombo vinavyosafiri hapa.

Lakini taarifa hii na kwa taarifa ya Baraza hili, mimi binafsi ni mara ya mwanzo kuisikia, sio kutoka kwa mwakilishi tu lakini hata kutoka kwenye njia zozote zile kwa maandishi au kwa mdomo. Kwa hivyo, namuomba aniletee huo ushahidi ili tuweze kuufanyia kazi na namuhakikishia kwamba mimi na yeye tutakwenda pamoja ili kuonana na huo uongozi.

Nam. 3

Maabara ya Afya ya Jamii Wawi - Pemba

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hilo ameliondoa)

Nam. 138

Katiba ya Zanzibar Kuandikwa Upya Kabla ya Uchaguzi Mkuu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea na mchakato wa kupata Katiba mpya ya Muungano.

(a) Je, Serikali ina mpango gani na Katiba ya Zanzibar ambayo imekuwa ikiwekewa viraka badala ya kuandikwa upya kulingana na wakati.

(b) Je, ni lini wananchi wa Zanzibar watakuwa na Katiba yao inayotokana na maamuzi ya wananchi badala ya Muungano kupata maoni ya wananchi wake.

(c) Serikali imejiandaa vipi na mabadiliko ya Katiba ya Muungano kwa vile moja kwa moja mabadiliko yatakayotokea pia yatagusa na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 138 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kifungu cha 80 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kimetoa uwezo kwa Baraza la Wawakilishi kubadilisha kifungu

chohcote cha Katiba, ambapo mswada wa kubadilisha Katiba hautopitishwa na Baraza isipokuwa uwe umeungwa mkono kwa mara ya kwanza na mara ya pili kwa kura si chini ya theluthi mbili ya kura zote za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Hivyo, Mhe. Spika marekebisho yaliyofanywa kwenye Katiba yamefanywa kwa kufuata masharti ya kifungu cha 80 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Mhe. Spika, miongoni mwa marekebisho muhimu yaliyofanywa kwenye Katiba ni kama ifuatavyo:-

(i) Zanzibar kufuata mfumo wa kidemokrasia wa vyama vingi vya siasa chini ya kifungu cha 5 cha Katiba.

(ii) Mgawanyo wa madaraka kati ya mamlaka tatu, kifungu cha 5(a)(1).

(iii) Kuwepo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka, Kifungu cha 56(a)(1).

(iv) Muundo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Kifungu cha 9(3).

Mhe. Spika, marekebisho hayo na mengine mengi yaliyofanywa sio viraka, ni marekebisho ya msingi kwa maslahi ya Zanzibar na kwa wananchi wote wa Zanzibar.

(b) Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi katika kikao chake cha tarehe 09 Oktoba, 1984 kwa niaba ya wananchi na kwa madhumuni ya kujenga jamii na kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Zanzibar inaongozwa na Serikali yenye kufuata misingi ya demokrasia, ilitunga Katiba ya Zanzibar ambayo kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha Katiba hiyo, itakuwa na nguvu za kisheria nchini kote.

Mhe. Spika, kifungu cha 9(2)(a) cha Katiba kinaeleza kuwa mamlaka ya kuendesha nchi ni ya wananchi wenyewe ambapo nguvu na uwezo wote wa Serikali kufuatana na Katiba itatoka kwa wananchi wenyewe.

Mhe. Spika, ni dhahiri kwamba Katiba hii imetokana na wananchi wenyewe ambao Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanawakilisha wananchi wote, na kwa niaba yao tarehe 09 Oktoba, 1984 wakatunga Katiba hii ambayo mpaka hii leo imeendelea kuwa ndiyo sheria mama na dira ya nchi, iliyoweka kinga ya haki za lazima, wajibu na uhuru wa mtu binafsi.

(c) Mhe. Spika, kwa kuwa mchakato wa kupata Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano bado unaendelea ni vyema tusubiri kwanza kukamilika na mchakato huo, na ipatikane Katiba mpya ya Jamhuri ya

Muungano. Kwa kipindi hichi ni mapema sana kuanza kufikiria marekebisho ya Katiba ya Zanzibar, bila ya kujua kwanza Katiba ya Jamhuri ya Muungano inataka nini na inaelezea nini. Baada ya kuwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano, wananchi wa Zanzibar kwa mujibu wa taratibu uliowekwa na Katiba ya Zanzibar, wanaweza wakihisi ipo haja ya kufanya marekebisho ya Katiba yao wakafanya hivyo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe.Waziri kutokidhi swali la msingi.

Wananchi wa Zanzibar ni lini watapata haki yao ya demokrasia ya kutoa maoni juu ya Katiba ya aina gani wanaitaka, baada ya kufanyiwa marekebisho na viongozi au wana siasa kwa niaba ya wananchi.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo kwamba hivi sasa tuko katika mchakato wa kupata Katiba ya Jamhuri ya Muungano, baada ya kupata Katiba ya Jamhuri ya Muungano, ikishakubalika vyovyote itakavyokuwa, hapo wananchi watakuwa na uhuru kwa kupitia Waheshimiwa Wawakilishi wao kwamba kuna mambo ikiwa wanahisi kuwa katika Katiba hiyo inahitaji marekebisho, basi wanao uwezo wa kukaa pamoja na kuyapima ili ule mchakato wa kuanza kurekebisha Katiba ya Zanzibar ukafanywa.

Kwa hivyo, mimi nafikiri na ninavyoshauri kwamba bado tusubiri mpaka baada ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano kupatikana. Kwa hivyo, kama kuna haja ya Katiba ya Zanzibar kurekebishwa ndio tuweze kurekebisha kwa sababu hivi sasa tunaweza kurekebisha kitu kabla ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, halafu ikabidi tuje tufanye tena marekebisho. Kwa hivyo, kwanza tusubiri, baadae wananchi wetu kwa kupitia Wawakilishi wao wanaweza wakaanzisha huo mchakato wa kurekebisha Katiba kwa mujibu wa vifungu vya Katiba vinavyosema.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, muda sio mrefu tulikuwa na semina kuhusu Katiba hii ya Muungano, semina ambayo iliendeshwa na mtaalamu mkubwa katika nchi hii na mada yake ya mwisho ilikuwa kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kusoma ilikuwa ni mada inayozungumzia athari za Katiba mpya ya Zanzibar. Kifungu cha kwanza kilisema hivi

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe hebu subiri kidogo, sauti yako haisikiki vizuri Mhe. Waziri pale na Wajumbe pia hawafahamu.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Nitajitahidi Mhe. Spika. Mhe. Spika, hivi karibuni tulikuwa na semina inahusiana na mchakato wa Katiba mpya ya Muungano, iliyoendeshwa na mtaalamu mkubwa na mada yake ya mwisho ilikuwa ni mada inayohusiana na athari za Katiba mpya kwa ya Zanzibar. Kwa ruhusa yako naomba kusoma athari hizo kama ifuatavyo, halafu ndio swali langu lifuate.

1. Hati ya Muungano, yaani *Article of Union* haitokuwa tena na nguvu ya kisheria, yaani itakuwa waraka wa kihistoria na sio tena sheria ya nchi.

2. Katiba mpya ya Muungano ndio itakuwa Katiba mama na Katiba ya Zanzibar itakuwa kwa mujibu wa Katiba ya Muungano.

3. Katiba ya Zanzibar iliopo kama ilivyoelezwa mara ya kwanza mnamo mwaka 1990, ilipata uhalali wake kutokana na watu wa Zanzibar na iliibana hati ya Muungano na sio Katiba ya Muungano.

4. Baada ya kufuata mchakato wa Katiba mpya, ingawa kuna walakini katika mchakato huo, kwa hivyo itabidi ama Katiba irekebishwe ili ifuate Katiba ya Muungano au iandikwe upya na pale ambapo pana mgongano wa Katiba hizi mbili, basi Katiba ya Muungano itakuwa na kauli ya mwisho.

Mhe. Spika, kwa sababu tuliona kuna matatizo kati ya Katiba ya Muungano na Katiba ya Zanzibar na tukaunda Katiba mpya na kwa sababu fikra za mhadhiri wa semina hii, ina maana kwamba baada ya kuundwa Katiba ya Muungano ambayo itakuwa ni Katiba mama, Katiba ya Zanzibar itakayotungwa basi isikiuke yale yaliomo katika Katiba ya Muungano na kama kuna mambo yaliyohitilafiana basi Katiba ya Muungano ndio itakayokuwa na mamlaka ya mwisho, kama ilivyo Katiba ya Zanzibar katika kifungu cha 4.

Swali ni kwamba je, tukingojea mpaka Katiba ya Muungano ikatungwa, tukaitizame ilivyo na mambo saba hivi sasa si tunajua uzito wake, yakichukuliwa hatuna chetu tena. Je, hatuoni kuwa tutakuja kuunda Katiba ambayo haina maslahi kwa wananchi wa Zanzibar kama ni nchi iliyo na uhuru kamili.

Je, huoni kuwa suluhisho pekee la kujiepusha na matatizo haya ni kuwa na Muungano wa serikali tatu, Serikali ya Zanzibar, Serikali ya Tanganyika

ambazo kila moja iwe na mamlaka kamili na Serikali ya Muungano ambayo haitoathiri Katiba ya nchi hizi mbili zilizofanya Muungano.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwanza sikubaliani naye kwamba Katiba ya Muungano ya hivi sasa kuwa ni tofauti, yao iko juu zaidi kuliko Katiba ya Zanzibar. Hii ndio moja katika mambo ambayo siku zote tulikuwa tunasema .

Mhe. Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania…

UTARATIBU

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, mimi sikuzungumza Katiba iliyokuwa hivi sasa, lakini kama nizungumze inahitilafiana kweli. Ukifungua kifungu cha mwanzo cha Katiba ya Muungano kinasema,

"Tanzania ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano".

Katiba ya Muungano inaeleza, ukiona Rais ni Rais wa Jamuhuri ya Muungano na Amiri Jeshi Mkuu, ukiona kiongozi ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Katiba ya Muungano inacho kifungu kama Katiba ya Zanzibar kuwa kama kuna sheria zinatofautiana, kwa hivyo Katiba ya Muungano ndio yenye nguvu kuliko zote.

Ushahidi wa pili Mhe. Spika, kwa ruhusa yako, nilisikia watu wanazungumza siku moja kiongozi wetu mkuu hapa Makamu wa Pili wa Rais alikuwepo katika Bunge, lakini nasikia Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano alizungumza kuwa, hapa hatuna Makamu wa Pili wa Rais, hapa tuna Mbunge wa Jamhuri ya Muungano. Sijui kama ni kweli lakini nilisikia hivyo.

Kwa hivyo, kama wao wenyewe tayari wanaheshimu Katiba yao na wala hawajui marekebisho yetu kuwa ni halali, na wanaanza kuyapigia kelele, kwa nini waseme kuwa hii Katiba tuliyonayo hivi sasa ya Muungano haikidhi Katiba ya Zanzibar.

Mhe. Spika: Sasa taarifa yako iko wapi, naona sikufahamu.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Taarifa yangu ni kuwa Mhe. Spika, hasa hii Katiba iliyorekebishwa ya Muungano ina vifungu vinapingana na Katiba ya Zanzibar.

Mhe. Spika: Kwa hivyo, swali lako liko wapi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, swali langu ni kuwa akubaliane na mimi kuwa Katiba ya Muungano itakuja kukiuka Katiba ya Zanzibar, hilo ndio sikubali anitafutie jibu jengine. Vipi tutakuwa na uwezo wa Kikatiba kama Zanzibar ni nchi tukiingojea Katiba ya Muungano, Katiba ikimalizika halafu na sisi tukaunda Katiba yetu wakati imeeleza humu kama nilivyosoma ni kuwa baada ya Katiba ya Muungano kuundwa kama tutakuwa na Katiba ya Zanzibar iliyokuwa vifungu vyake vinapingana na Katiba ya Muungano, basi hii Katiba ya Muungano ndio itakuwa na nguvu, maana yake hata kama tukija kutunga vipi baadae itakuwa sisi kwa vile vifungu ambavyo vimo katika Muungano havipiti huko pengine vina athari kubwa juu yetu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, naomba nijibu ifuatavyo na namuomba Mhe. Mjumbe anisikilize vizuri. Katiba ya Jamhuri ya Muungano hivi sasa iliopo, sio rasimu, Katiba iliopo, mimi sikubaliani nayo kwa sababu ukitizama kifungu cha kwanza au cha pili, kinasema

"Jamhuri ya Muungano ni Muungano wa nchi moja, yaani ni nchi moja Jamhuri ya Muungano", hivyo sio kweli.

Jamhuri ya Muungano ni Muungano wa nchi mbili; yaani Zanzibar na Tanganyika. Hilo la kwanza. Lakini la pili hatuwezi kurekebisha Katiba ya Zanzibar hivi sasa kwa sababu hata kama tutarekebisha Katiba ya Zanzibar leo, katika hii Katiba ya Jamhuri ya Muungano mnaweza mkawa na mambo ambayo sote Wazanzibari na Watanganyika tunayakubali. Kwa hivyo ni lazima tuyaweke katika Katiba yetu. Ndipo nikasema kwanza tusubirini Katiba ya Jamhuri ya Muungano, hii rasimu tuikubali sote ipite, baada ya kwishakupita, sisi Wazanzibari tutajua kuna kitu gani cha kurekebisha katika Katiba yetu.

Mhe. Spika, ukitizama katika rasimu hivi sasa inasema kwamba kutakuwa na serikali tatu, kwa maana kutakuwa na Katiba tatu, Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Katiba ya Tanganyika na Katiba ya Zanzibar. Sasa hivyo ina maana hizo ni mamlaka ambazo zimepewa kwa nchi wenyewe wala haikusema Katiba ya Zanzibar itakuwa na kitu gani na kitu gani, hapana. Hilo nawaachia Wazanzibari wenyewe, na wala haikusema Katiba ya Tanganyika itakuwa na kitu gani na gani, hiyo wameachiwa Watanganyika wenyewe.

Mhe. Spika, unapofanya Katiba kuna mambo lazima uyatizame. Katiba yenyewe ni alama muhimu ya nchi, inaonesha njia na pia inaonesha mwanga wa maendeleo kwa nchi ile, ina malengo fulani na inaonesha dhahiri kwamba kutakuwa kuna mamlaka tatu ambazo zote zitakuwa na nguvu na kila moja

itakuwa na nguvu zake katika hayo mamlaka. Sasa sisi baada ya kupata hiyo Katiba ya Jamhuri ya Muungano tukishakuikubali, sisi ndio tutatizama je, Katiba yetu ya Zanzibar inapata mamlaka hayo, inapata nguvu hizo, sasa hapo ndio tutakuwa tuko tayari kwa kurekebisha Katiba ya Zanzibar.

Kwa hivyo, hivi sasa bado nasema kwamba ni mapema sana kufikiria kurekebisha Katiba ya Zanzibar, sisemi kwamba haitohitajia marekebisho, hataa lakini marekebisho hayo baada ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano kupita, kwa sababu tunaweza tukarekebisha hivi sasa, tukaona kitu katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano ambacho ni lazima tukirekebishe. Kwa hivyo, tusubirini hapo baadae na baada ya hapo tufuate utaratibu wa kifungu 80(a)(1) kinacholeta utaratibu wa kubadilisha Katiba yetu. Kuna mambo ambayo tukitaka kuyarekebisha ni lazima tufanye kura ya maoni kwa mujibu wa Katiba yetu na hayo ndio matakwa ya wananchi wenyewe wanavyosema. Kwa hivyo, ndio nikasema ni lazima tufuate utaratibu ambao upo na uliowekwa katika Katiba ya Zanzibar hivi sasa.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, katika kurekebisha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hivi karibuni ilitoka fursa kwa wananchi kutoa maoni yao kwa ajili ya marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kutoa maoni wananchi walio wengi walipendelea mfumo wa Muungano wa mkataba, pamoja na kuwa wananchi ndio wenye maamuzi na pamoja na kuwa rasimu haikuelekea kule walikoelekea wengi lakini hii rasimu bado haijawa maamuzi.

Sasa namuuliza Mhe. Waziri, kwa kuwa wananchi walio wengi wameshatoa maoni yao na mwelekeo wao walikoelekea imeonekana. Ni lini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itatoa rasmi kauli yake ili wananchi wa Zanzibar na wao wajue kwamba serikali yao ina maoni gani.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitoa zamani msimamo wake na ilisema kwamba itaheshimu maamuzi ya wananchi. Huo ndio msimamo wa serikali na bado upo hapo hapo kwamba utaheshimu maamuzi ya wananchi.

Hivi sasa rasimu imetoka na tumeona muna kitu gani katika rasimu, ni jukumu letu sasa kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa, katika hayo Mabaraza ya Wananchi au Mabaraza ya Katiba kusema yale ambayo mnahisi yana matatizo, baada ya hapo itakuwa hiyo ndio kauli ya wananchi na kauli ya wananchi bado tunasema kwamba serikali itayaheshimu.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato) ya 2013

(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi, Kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali na Mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika: Hati ziliwasilishwa jana na leo unawasilishwa mswada moja kwa moja.

Waheshimiwa Wajumbe, ninakumbushwa hapa kuhusu utaratibu wa miswada kama hii ambayo haikusomwa kwa mara ya kwanza kipindi kile cha mkutano uliopita kwa sababu mambo yake yote yanamalizika kwenye mkutano huu.

Mswada wa Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato) ya 2013

(Kusomwa kwa Mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi Kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali ya mwaka 2013, ambapo unakusudia kufanya mabadiliko katika sheria mbali mbali kwa lengo la kudhibiti na kukusanya mapato ya serikali.

Mhe. Spika, mswada huu unaopendekezwa umefanya marekebisho kwa sheria zinazosimamiwa na Bodi ya Mapato Zanzibar na Sheria nyengine Zinazohusiana na Mapato ikiwemo Sheria ya Uwekezaji Nam. 11 ya mwaka 2004, Sheria ya Usafiri Barabarani Nam. 7 ya mwaka 2003, Sheria ya Rufaa za Kodi Nam. 1 ya mwaka 2006 na Sheria ya Ardhi Nam. 12 ya mwaka 1992.

Mhe. Spika, Sheria za Bodi ya Mapato Zanzibar zilizofanyiwa marekebisho ni kama zifuatazo:-

1. Sheria ya Usimamizi wa Kodi Nam. 7 ya mwaka 2009.
2. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Nam. 4 ya mwaka 1998.
3. Sheria ya Ushuru wa *Stamp* Nam. 6 ya mwaka 1996.
4. Sheria ya Kodi za Hoteli Nam. 1 ya mwaka 1995.

5. Sheria ya Ada za Bandari Nam. 2 ya mwaka 1999
6. Sheria ya Kodi za Mafuta Nam. 7 ya mwaka 2001.

Mhe. Spika, kutokana na kuongezeka majukumu ya serikali pamoja na kuongeza usimamizi wa mapato na matumizi ya serikali ambayo yamekuwa yakiongezeka kila baada ya muda Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo imeona kuna umuhimu wa kufanya mabadiliko ya sheria mbali mbali zinazohusiana na ukusanyaji wa mapato. Hatua hiyo itatoa fursa ya kuweka misingi ya kufanya mabadiliko kutokana na kubadilika kwa hali ya uchumi na mfumo wa biashara ulivyo hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, waraka huu una madhumuni ya kuwasilisha rasmi ya mapendekezo ya Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi Zinazohusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali ya mwaka 2013.

Mhe. Spika, mswada huu wa sheria umegawika katika sehemu 11, ambapo ni kama ifuatavyo:-

Sehemu ya kwanza na mswada inahusiana na vifungu vya utangulizi, ambavyo vinaelezea jina la sheria na utumikaji wa sheria.

Sehemu ya pili ya mswada inahusiana na marekebisho ya sheria ya ada ya Bandari Nam. 2 ya mwaka 1999, ambapo inafanyiwa marekebisho yafuatayo:-

(a) Kifungu cha 10 kwa kufuta kifungu cha 3 na kuweka kifungu kipya cha 3, ambacho kinatoa mamlaka kwa Kamishna kupata msaada kwa taasisi zote za serikali, ambazo zinasimamia vyombo vya baharini au usafiri wa anga ili kusaidia katika ukusanyaji wa kodi.

(b) Kwa kuongeza kifungu cha 5 na 6 ambavyo vinatoa adhabu kwa taasisi yoyote itakayokataa kutekeleza wajibu wake katika kusimamia kodi ya serikali kwa kuitoza asilimia 10 ya kiwango cha kodi inayodaiwa.

Lengo la marekebisho hayo ni kutaka watu na taasisi mbali mbali za serikali kuwajibika na kushiriki katika usimamizi wa kodi kwa wote ambao wako chini ya usimamizi wa taasisi zao kiuendeshaji na kimamlaka.

Mhe. Spika, sehemu ya tatu ya mswada inafanyiwa marekebisho Sheria ya Kodi za Hoteli Nam. 1 ya mwaka 1995 kwa kufanya mambo yafuatayo:-

(a) Kufuta kifungu cha 3 na kuweka kifungu kipya cha 3, ambapo;

(i) Kijifungu cha kwanza kinaweka utaratibu mzuri zaidi wa utozaji wa Kodi za Hoteli pamoja na kutanua wigo wa kodi kwa hii hoteli, watembezaji wageni na mikahawa.

(ii) Kijifungu cha pili kinampa uwezo waziri kuweka viwango vyengine tofauti na kiwango cha asilimia 18 kilichopo kwa aina maalum za biashara ambazo zitaonekana zinahitaji kuwekewa kiwango tofauti na kilichoelezwa kwenye kifungu cha kwanza.

(iii) Kutoa uwezo kwa waziri kufanyiwa marekebisho jadweli kuibadilisha au kuiongeza.

Lengo la marekebisho ni kuweka utaratibu mzuri wa usimamizi wa Kodi za Hoteli na kuhakikisha kwamba walipa kodi wenye sifa zinazofanana wanatozwa kodi katika kiwango sawa.

Sehemu ya nne ya mswada inaweka marekebisho ya Sheria ya Kodi za Mafuta Nam. 7 ya mwaka 2011 kwa kufanya yafuatayo:-

(a) Kufuta kifungu cha 3 na kuweka kifungu kipya ili kutoza na kukusanya kodi moja kwa moja wakati wa uingizaji wa mafuta. Kwa mujibu wa taratibu za Sheria za Forodha pamoja na kutoa uwezo kwa waziri kubadilisha jadweli za bei za mafuta.

(b) Kutambua na kutumia masharti ya ukadiriaji kodi, ulipaji kodi na ukusanyaji wa kodi kama ilivyo katika Sheria za Forodha kwa bidhaa zinazoingizwa nchini.

(c) Kufuta kifungu cha 8(a) na kuweka kifungu kipya kinachompa uwezo Kamishna kuingia na kuangalia sehemu yoyote katika chombo na kwenye vituo vya kuuzia mafuta. Aidha kifungu kimetoa uwezo wa Kamishna kukamata bidhaa za mafuta wakati wa ukaguzi iwapo zitabainika kwamba hazijalipiwa kodi au zimeingizwa kinyume na utaratibu.

(d) Kufuta kijifungu cha kwanza katika kifungu cha 10(a) na kuweka kijifungu kipya kinachotoa adhafu kwa muingizaji wa mafuta atayeshindwa kulipa tofauti ya bei ya mafuta.

Sehemu ya tano ya mswada inafanya marekebisho ya sheria ya Kodi ya *Stamp* Nam. 6 ya mwaka 1996 kama sehemu hii:-

(a) Kufuta kifungu cha tatu na kuweka kifungu kipya cha 3 ambapo;

(i) Kinaeleza utozaji ushuru wa *stamp* kwa wale wote ambao hajasajiliwa kulipa kodi ya *VAT* au hoteli. Bidhaa zinazosamehewa kodi ya *VAT* zitalipiwa kodi ya *stamp* na kodi kwa hati mbali mbali zilizoelezwa kwenye sheria.

(ii) Kinatoa mamlaka kwa waziri kubadilisha kiwango cha kutozea kodi cha asilimia 3 kwa baadhi ya bidhaa ikiwa kutakuwa na maslahi ya umma katika kufanya hivyo.

(iii) Kutoa mamlaka kwa waziri kuvuta hati au kubadilisha viwango vya hati mbali mbali zilizoelezwa katika sheria ili kuhakikisha viwango hivyo vinakwenda sambamba na mabadiliko ya hali halisi ya uchumi.

(b) Kuweka kijifungu kipya cha 3(a) ili kumpa mamlaka waziri kuteua mawakala mbali mbali wa kukusanya ushuru wa *stamp* hasa katika hali zilizoelezwa katika sheria kama vile Ofisi ya Mrajis, Idara ya Mahakama, Benki Kuu na kadhalika.

(c) Kuweka kijifungu kipya cha 4(2) kinachompa uwezo Kamishna baada ya kuzingatia Sheria za Umiliki na Uhaulishaji wa Mali kutoa tamko kuwa hati hizo zimelipiwa kodi na

(d) Kufuta kifungu cha 13(b) ambacho maelezo yake yamewekwa wazi zaidi katika kifungu cha 3 cha sheria.

Sehemu ya sita ya mswada inaweka marekebisho ya sheria ya Kodi ya Uongezeko la Thamani Nam. 4 ya mwaka 1998 kama ifuatavyo:-

(i) Kurekebisha kifungu cha 6 cha kifungu cha 16 ili kuwaruhusu walipa kodi kudai marejesho yao ya kodi katika kipindi cha miezi mitatu mfululizo kulingana na risiti zilizotolewa.

(ii) Kufuta kifungu cha 74 ambacho kwa sasa maelezo yake yamewekwa wazi katika sheria ya Kodi ya *Stamp* ya kuwataka walipa kodi kulipa kodi ya *stamp* kwa bidhaa zinazosamehewa kulipiwa kodi ya *VAT*.

Mhe. Spika, sehemu ya saba ya mswada inafanya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi Nam. 7 ya mwaka 2009.

(a) Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo inaliomba Baraza lako tukufu kuondoa kifungu cha 20 cha mswada wa sheria kinachofanyiwa marekebisho kifungu cha 5 cha Sheria ya Usimamizi wa

Kodi ya mwaka 2009 baada ya kubaini kuwa kuwepo kwa kifungu hicho kunaweza kuathiri utekelezaji wa sheria nyengine za kodi.

(b) Mhe. Spika, baada ya marekebisho hayo katika sehemu ya saba ya mswada inafanyiwa marekebisho yafuatayo:-

(i) Kuongeza maneno katika kifungu cha 15(1) ili kuwataka wafanyabiashara kutoa taarifa iwapo watafuta biashara zao kwa muda maalum au kufunga biashara moja kwa moja.

(ii) Kurekebisha maelezo ya kifungu cha 18 ili kuweka marejeo ya kifungu sahihi cha 62 badala ya marejeo ya kifungu cha 63 yaliopo ambayo hayaleti maana iliyokusudiwa.

(iii) Kuongeza kifungu cha 31(a) kwa lengo la kuwataka walipa kodi watambue tafsiri ya malipo ya kodi ni kuwa baada ya risiti kutolewa, kufanywa malipo au kutolewa huduma ili kutanua wigo wa kodi.

(iv) Kurekebisha kifungu cha 32 ili kutoa uwezo kwa Kamishna kumtaka mlipa kodi kuwasilisha kodi mapema wakati wa kutoa kiwanda bidhaa zilizozalishwa au wakati wa kuingiza bidhaa nchi kwa lengo la kuhakikisha kodi haipotei na inakusanywa kutoka kwa mlipa kodi moja kwa moja.

(v) Kuongeza kijifungu cha 5 katika kifungu cha 45 kwa lengo la kutoa mamlaka Hati za Kamishna kutambuliwa kuwa ni kielezo cha kutoa ushahidi mahakamani ili kumfanya mlipa kodi kuthibitisha tuhuma zinazomkabili.

(vi) Kuweka vifungu vipya 46(a), (b) na (c) ili kumpa uwezo kwa Kamishna kutoa tafsiri na ufafanuzi katika vifungu mbali mbali vya sheria za kodi kupitia Tangazo Rasmi la Serikali kwa lengo la kutoa ufafanuzi zaidi kwa Sheria za Kodi na kuondoa utata wa tafsiri katika vifungu vya sheria vilivyojitokeza na vinavyoweza kujitokeza.

(vii) Katika kifungu cha 53(1) mbali ya mtu anayekwepa kodi aliyepo katika kifungu hicho kwa kuongeza maneno na mtu yeyote atakayeshirikiana na mlipa kodi kwa njia yoyote ile kukwepa kodi zinazotozwa chini ya sheria hii.

Mhe. Spika, sehemu ya nane ya mswada inafanya marekebisho katika Sheria za Rufaa za Kodi Nam. 1 ya mwaka 2006 kwa kufanya marekebisho yafuatayo:-

(a) Kwa kuweka maana ya neno kodi yenye mzozo na kodi isiyo na mzozo ili kutoa uelewa kwa walipa kodi katika kuwasilisha madai ya kodi katika pingamizi za makadirio ya kodi zinazotolewa na Makamishna.

(b) Kufanyia marekebisho kifungu cha 16 kwa kupunguza kiwango cha malipo ya asilimia 50 ya kodi inayodaiwa na kuweka malipo ya theluthi moja ya kodi, ili kuwawezesha walipa kodi kuwasilisha mashauri yao na pingamizi za makadirio ya kodi.

(c) Kuongeza muda wa kujibu maelezo ya Kamishna kutoka siku 14 hadi 21.

Sehemu ya tisa ya mswada inafanyia marekebisho Sheria ya Kodi ya Ardhi Nam. 12 ya mwaka 1992 kwa kuongeza maneno baada ya kushauriana na Waziri wa Fedha, ili kumtaka waziri anayeshughulikia masuala ya ardhi kushauriana na Waziri wa Fedha kabla kupunguza kiwango cha kodi ya ardhi.

Mhe. Spika, sehemu ya kumi ya mswada inafanyia marekebisho Sheria ya Usalama Barabarani Nam. 7 ya mwaka 2003 kama ifuatavyo:-

(a) Kijifungu cha 27(1) kwa kufuta kijifungu (f) ili kuondoa ruhusa kwa watu wanaoingiza magari nchini kuyatoa bandarini bila ya kusajili gari hizo.

(b) Kifungu cha 29 kwa kuongeza maneno kabla ya kukamilisha taratibu za Forodha ili kuwafanya watu wote wanaoingiza magari nchini kusajili na kuchukua namba za usajili bandarini kabla ya kutoa gari hiyo.

Mhe. Spika, sehemu ya kumi na moja ya mswada inafanyia marekebisho Sheria ya Ukuzaji Vitega Uchumi Nam. 11 ya mwaka 2004 katika kifungu cha 19 na 20 kama ifuatavyo:-

(a) Kufuta kijifungu cha pili cha kifungu cha 19 ili kutoa uwezo kwa Waziri wa Ardhi kwa kushauriana na Waziri wa Fedha kusamehe kodi ya ardhi ya wawekezaji kwa muda wa miezi 18 kwa maeneo maalum ya uwekezaji ambayo yatatangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali.

(b) Kutoa mamlaka kwa waziri kurekebisha, kubadilisha au kuweka jadweli mpya linalohusiana na vivutio kwa wawekezaji.

Mhe. Spika, kutokana na umuhimu wa mswada huu kama ni chachu ya kuongeza uwezo wa kukusanya na kusimamia mapato ya serikali, naomba mapendekezo hayo yajadiliwe na kupitishwa na Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja. *(Makofi).*

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hoja imeungwa mkono na kwa maana hiyo sasa hoja hii ijadiliwe. Kwa hivyo, naomba nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Ussi Jecha Simai (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti): Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti kuwasilisha muhtasari wa hotuba ya Wenyeviti wa Kamati kuhusu Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi, Kubadilisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi Kuhusiana na Ukusanyaji, Udhibiti wa Mapato ya Serikali na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujalia uzima, siha pamoja na nguvu zilizotufikisha hapa Barazani hadi tukaweza kufanya shughuli zetu kama tulivyopanga, hatuna budi kusema *Alhamdulilah*.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti shukurani za dhati zije kwako kwa kunipa nafasi hii ya kusimama hapa mbele ya Baraza lako kutoa muhtasari wa maoni ya Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kuhusu Mswada wa sheria ya kutoza kodi na kubadilisha baadhi ya sheria za kodi na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii pia kumshukuru Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo pamoja na watendaji wake wote kwa mashirikiano yao na kamati wakati wote tulipokuwa tukichambua na kujadili mswada huu wa sheria.

Mhe. Spika, sitakuwa nimetenda haki iwapo nitaendelea na hotuba hii bila ya kutoa shukurani za pekee kwa wajumbe wa kamati hii ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi ambao tumeshirikiana kwa umoja wetu kuupitia na kuuchambua mswada huo.

Mhe. Spika, pamoja na kutambua mchango wao mkubwa kwenye kamati hii hadi kufanikisha kazi hii, naomba sasa niwataje kwa majina wajumbe wa Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Mwenyekiti
2. Mhe. Salmin Awadh Salmin	-	Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	-	Mjumbe
4. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Mjumbe
5. Mhe. Ussi Jecha Simai	-	Mjumbe
6. Mhe. Omar Ali Shehe	-	Mjumbe
7. Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	-	Mjumbe
8. Ndg. Shemsa Maabad Mohamed	-	Katibu
9. Ndg. Khamis Hamad Haji	-	Katibu

Mhe. Spika, nchi yetu kama zilivyo nchi nyingi duniani tunaiendesha kwa kutumia kodi zinazokusanywa. Tafiti zinaonesha kuwa Zanzibar inakabiliwa na udogo wa wigo wa mapato kutokana na ukubwa na muundo wa uchumi wake na umasikini, bado umasikini unaendelea kukwaza uwezo wa serikali kukusanya mapato hata hivyo kiwango cha jitihadi za ukusanyaji wa mapato, pamoja kuwa leo tunakuja kuupitisha mswaada wa kuidhinisha kodi mbali mbali.

Lakini bado tunaishauri serikali yetu kuweka mkazo wa kuandaa mazingira mazuri kwa maeneo ya uekezaji, ili kuwavutia wawekezaji waje kuekeza kwenye viwanda kwa ajili kupanua wigo wa kodi ya serikali vyenginevyo kila siku tutaendelea kuwakamua wananchi wetu ambao na wao wako taabani. Pamoja na hayo kiwango chetu cha ukusanyaji kodi kimekuwa kikiimarika na kwa sasa ni zaidi ya wastani kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Mhe. Spika, sehemu ya kwanza ya mswada inahusu utangulizi na jina la mswada na tarehe ya kuanza kutumika, lakini sehemu ya pili inahusu marekebisho ya Sheria ya Ada ya Bandari Nam. 2 ya 1999, ambapo sheria imetoa uwezo kwa Kamishna kumzuia mmiliki wa meli, ndege au bidhaa kuondoka ikiwa hawajalipa kodi ambayo inastahiki kulipwa.

Fedha nyingi zimekuwa zikipotea kutokana na walipa kodi ambao wanakwepa kulipa kodi kupata fununu za kufuatiliwa. Walipa kodi hao hao husafiri na kuacha deni hilo bila ya kulilipa.

Mhe. Spika, kuna mifano hai ya baadhi ya makampuni ya ndege, meli na hata wenye mahoteli hukimbia baada ya kuona wanadaiwa madeni makubwa na kwa kuwa sheria ilikuwa haimpi Kamishna mamlaka ya kuwachukulia hatua ya kuwadhibiti kwa wakati huo ilikuwa hakuna la kufanya.

Lakini sheria hii imempa mamlaka Kamishna kuweza kumuagiza mtu au taasisi yoyote kumzuia mtu au taasisi yoyote ili kuweza kulipa kodi ya serikali. Tunaamini kuwa kifungu hiki kitawabana watu wa aina hiyo na kukomeshwa kwa udanganyifu huo.

Sehemu ya tatu ya mswada inahusu marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Hoteli Nam. 1 ya mwaka 1995. Katika kifungu hicho kimeweka masharti ya kutoza kodi ya hoteli kwa wanatoa huduma za hoteli, mikahawa na huduma za kuwatembeza wageni. Tunaipongeza sana serikali kwa kuliona jambo hili kwani tumekuwa tukishuhudia watu wengi hasa sehemu za vijijini wakikodisha nyumba zao na kuwaweka wageni ambao hawalipi kodi yoyote ya serikali, ingawa wale sisi tunawaita wazungu vishuka lakini fedha wanazo na wanalipa tena kwa dola.

Mhe. Spika, ni jambo la faraja kuona kuwa hata wao wanaowakodisha wazungu vishuka watalipa kiasi kitachoonekana kina kidhi mahataji kwa hali zao. Kwa muda mrefu tumekuwa tukiiambia serikali yetu kuwa kuna wageni wanakodishwa nyumba za kuishi na wenyeji kinyume na utaratibu bila ya kulipa kodi yoyote serikalini. Hata hivyo, wageni hao wanaishi katika majumba hayo bila ya kuwa na ulinzi unaoaminika.

Mhe. Spika, Mwenyezi Mungu atuepushie mbali pindi ikitokea mgeni ameuliwa na majambazi, hapo ndipo lawama inakuja serikalini na ni haki yao kulalamika kwani hakuna mgeni anayekuja bila ya kukata *visa* au kujaza *form* yoyote inayomruhusu kuingia nchini.

Kutokana na hali hii, inaonekena wenyeji hushirikiana na wageni kuingia nchini kwa njia ya udanganyifu, kwani pahala wanapofikia hapakusajiliwa, pia kuna hatari ya kuingiza wageni wabaya ambao wanaweza kuja kufanya vitendo vya ugaidi nchini mwetu. *(Makofi)*

Sehemu ya nne, inahusu marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mafuta Nam. 7 ya 2001. Kwa kweli mara nyingi tumekuwa tunalalamika suala la magendo ya mafuta ambalo limeota mizizi hapa Zanzibar tena linaleta madhara makubwa mbali ya kuingizwa kwa mafuta yaliyokuwa hayana viwango bali pia mafuta hayo hayalipiwi kodi yoyote inayostahiki.

Mhe. Spika, masharti ya kifungu hiki yaliyowekwa kwa uingizaji wa bidhaa za mafuta uambatane na hati ya kupakia na kushusha mafuta kila yanapoingizwa nchini, ni wazo zuri sana na pia litatuondolea udanganyifu wa uingizaji wa bidhaa hizo.

Aidha uwezo aliopewa Kamishna au afisa yeyote kuweza kuingia na kukagua sehemu yeyote au chombo chochote cha baharini ambacho anaweza kuamini kuwa kuna uwezekano wa kuhifadhiwa mafuta. Mhe. Spika, hii ni silaha nyengine ambayo ni muhimu sana, kwani kuna baadhi ya meli zinachemba za ndani kwa ndani ambazo kwa hali ya kawaida mtu hawezi kugundua kama kuna sehemu yamehifadhiwa mafuta na ndio hayo mengi yanauzwa katika vituo vya mafuta vilivyokuwa havijasajiliwa.

Sehemu ya tano ya mswada inahusu marekebisho ya Kodi ya *Stamp* Nam. 6 mwaka 1996. Vifungu hivi vinatoa fursa ya kulipa kodi ya *stamp* kwa wasambazaji wa bidhaa au huduma. Kodi hii itaongeza wigo wa kukusanya kodi, lakini ni vyema kabla ya kuanza kwa sheria hii ukafanyika utafiti wa kuzitambua bidhaa na huduma hizo na kuzipatia usajili ili iwe rahisi kuzitambua na kuzitoza kodi .

Mhe. Spika, sehemu ya sita ya mswada inahusu marekebisho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani. Katika kodi hii tunaliomba Baraza lako tukufu kukubaliana na kamati yangu kuwa pamaja na kuwa *VAT* imeridhia na kuikubali hapa katika Baraza lako. Hata hivyo, tungelishauri kuangalia na upande mwengine wa kupunguza au kuondoa *VAT* katika huduma ya umeme, ili unafuu upatikane kwa mwananchi wa kawaidi aweze kuutumia umeme kikamilifu na kupunguza matumizi ya kuni na kwa kufanya hivyo tutakuwa tunaokoa mazingira yetu. *(Makofi)*

Pamoja na marekebisho mengine mengi yaliyofanyika ambayo kamati yangu inayakubali na kuyaunga mkono. Hata hivyo, ningependa kuipongeza tena serikali kwa kurekebisha Sheria ya Ardhi ya mwaka 1992 ya kuweka uwezekano wa kutoongezewa muda wa (*grace period*) kwa wawekezaji wa mahoteli hadi wakutane na kushauriana kwa mawaziri wote wawili wa ardhi na wa fedha. Hali hii ni faraja sana, kwani panapo mashirikianao hakuharibiki jambo.

Mhe. Spika, pamoja na marekebisho haya ingawa tumechelewa lakini iko haja kwa serikali kuangalia upya Sheria ya Matumizi ya Ardhi kwa wawekezaji hasa wenye mahoteli kuwawekea masharti ya kujenga majengo ya ghorofa ambayo yataongeza idadi ya nyumba badala ya kuchukua maeneo makubwa na kujenga vibanda na nyumba za kawaida, jambo ambalo kutokana na udogo wa ardhi yetu inatukosesha mapato.

Kwa kweli, pamoja na marekebisho tunayoyafanya lakini bado serikali inapaswa kuwa makini na kuzitekeleza kwa uadilifu na uaminifu mkubwa na kutomuonea haya mtu yeyote ambaye atajihusisha na kusaidia kuikosesha

serikali mapato pamoja na wale watakaokusanya na kuzitia mifukoni mwao fedha za wananchi.

Mhe. Spika, kamati yetu imefanya baadhi ya marekebisha madogo katika mswada huu, ikiwa ni pamoja na kurekebisha makosa ya uandishi na kuviongezea baadhi ya vifungu ufafanuzi zaidi, ili viweze kufahamika kwa uzuri zaidi na wajumbe wako marekebisho hayo tuliyoyafanya tumeshawapa Wajumbe wako wote.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo yote naunga mkono hoja na pia nawasihi Wajumbe wako wote wauchangie mswada huu, pia wauunge mkono kwani una manufaa kwa wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kuweza kunipa fursa ya kuchangia mswada huu ambao ni mzuri sana. Lakini nadhani ni vyema tumsaidie Mhe. Waziri, kwa sababu na sisi ni Waheshimiwa Wajumbe ambao tunao uwezo wa kuangalia jinsi gani ya serikali yetu inaweza kufikia katika yale malengo yanayokusudiwa.

Kwanza nishukuru sana Mhe. Spika, nilipokuwa nataka kusema nichangie niliangalia juu kule na nikaona meza tu, lakini nashukuru hivi sasa Katibu amekuja na wengine japo kuwa wamejificha nyuma ya viti lakini tunaomba maafisa wakae mbele, kwani nilitaka kusema maafisa hatuwaoni, kumbe wameshakuja.

Mhe. Spika, mswada huu kwanza nakubaliana nao kwa baadhi ya vipengele niseme kwamba ninakubaliana navyo na yako mambo mengine niweze kusaidia fikra zangu na hasa vile walivyonituma wananchi wa Jimbo la Kitope, ili tuone hali halisi ambayo tunaisaidia serikali yetu katika suala zima la ukusanyaji wa mapato.

Kwanza naunga mkono ripoti ya kamati imetuelekeza vizuri na imesema kuwa tuiunge mkono na sisi hatutaweza kuitupa kamati yetu na tutaunga mkono.

Nianze mchango wangu katika ukurasa wa watatu kwenye sehemu ya sheria ya mambo ya mahoteli na mikahawa. Mheshimiwa mimi nikubaliana na wewe hapa na hasa hapa ndipo tunapokosa mapato yetu ya uchumi wa serikali yetu hapa. Nimshukuru sana Mhe. Waziri ameona katika sehemu moja itakayoiwezesha Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar kuweza kupata

uchumi wake kulinda utaalamu kwa mujibu wa sheria za marekebisho ya hapa na pale.

Mhe. Spika, sasa hivi tuna wimbi kubwa sana la ujenzi wa mikahawa kihole katika ukanda wa bahari na hasa ukihusishwa na hawa, kama alivyosema Mwenyekiti wangu aliyetoa ripoti yake kuwa kuna wazungu wengine vishuka. Hili tunamuomba sana Mhe. Waziri tusipoangalia hasa sheria zetu hizi ambazo tumezitunga katika Baraza na tukaweza kuzisimamia kilillah taala kwa kunusurisha wazawa na wao ili kuweza kufanya biashara za aina kama hiyo, sasa biashara hizo wanazikosa wanafanya hawa vishuka.

Mhe. Spika, tukenda katika ukanda kuanzia Kiwengwa, Pwanimchangani mpaka Matemwe na halikadhalika ,utakuta asilimia kubwa hawa wawekezaji vishuka wadogo wadogo wa kizungu, hoteli zile na mikahawa utawakuta wao ndio wengi ambao wanaomiliki sehemu hiyo. Kwa wao Mhe. Waziri ingawa hatutaki kumfukuza mtu lakini ningeomba sana ungeweka sheria kali sana dhidi ya wao na hawa wazalendo tukawawekea sheria ambayo itawabembeleza wawekezaji wadogo.

Mhe. Spika, sasa hivi tunasema kuwa wimbi kumbwa la kutokupata kazi, wimbi kubwa la kupata sehemu ya mzaliwa kuweza kuweka mikahawa yao ya kitalii ili kuweza kupata fedha na waweze kuendesha familia zao na kutia uchumi kwenye serikali, hilo linakosekana na ukifanya hesabu utakuta wazungu ndio wengi kuliko wazaliwa. Mhe. Spika, hilo mimi nakubaliana nae.

Tena nasema Mhe. Spika, usimamizi wake uwe wa mara kwa mara kwa sababu tunatunga sheria hatimae hatufuatilii nina vigezo vingi. Halafu isitoshe tuna mawimbi haya utakuta kwenye vibaa hivi, hao hao wana mikahawa na wana baa, hivi ni vitu tofauti. Utakuta kuna baa wanaoweka ndio hao wenzetu wazungu hawa vishuka, vishuka hawa anaweka yeye baa ile kutuongezea zogo tu kwenye mitaa na mambo yasiyokuwa na maana. Sasa ni moja ambalo nalo hili Mhe. Spika, tungeliona kwa makusudi tukawawekea sheria kali nao ili wakaweza kushindwa kuweka na hili suala likapotelea kabisa bora lisikuwepo. Mimi naomba sana kwa Mhe. Waziri aliangalie vizuri sana hili.

Lakini vile vile nikubaliane naye sasa hivi hawa wawekezaji wetu ambao wakubwa wanakwenda na wakati, nao sasa hivi kuna ushindani wa biashara ya utalii katika nchi zetu za *East Africa*. Wenzetu sasa hivi wanaendelea kupiga hatua hadi hatua. Tungejaribu kuangalia katika sehemu moja ambayo hiyo wanasema katika utoaji wa *Visa* wanasema imekuwa ni kubwa tofauti na nchi ya Kenya na nchi nyenginezo. Hili nalo nimesema nimuombe Mhe. Waziri ajaribu kuliona aneo hili la kuweza kutusaidia.

Sasa tunapopata kodi nyengine tuone ili tuwape na wao punguzo, sio tupandishe kodi zetu kwa pamoja na ziende kwa wakati mmoja, watatukimbia hatimae sheria yetu itabakia kwenye *briefcase* na itakuwa haijafanya kazi yoyote. Namuomba sana Mhe. Waziri aliangalie nalo hili, lazima tuwe na usawa kama kodi hii tunapandisha tutafute njia nyengine kodi nyengine tuweze kuipunguza ili waweze na wao kujisikia wajipe moyo. Lakini tusifanya kupandisha kodi zote kwa pamoja na kwa wakati mmoja, tutakimbiwa na tutaachiwa majengo yetu.

Mfano tumeuona pale Venta tunayo pale mpaka leo hii Mhe. Spika, tumekosa sisi na kakosa mwekezaji. Kama kungekuwa na sheria nzuri pale Mhe. Spika, basi mimi naamini mpaka leo tungekuwa tunapata sisi serikali. Haidhuru pale sheria itakuwa imeshamuondoa yule mwekezaji aliyekuwepo pale kwa sababu kashindwa kulipa kodi zote. Lakini sheria haikutupa uwezo huo, nilitegemea sana kuwa leo hii sheria ya *ZIPA* Mhe. Waziri ungetuletea katika ubadilishaji, kwa mfano kama ile kwa sababu pale tumekosa hatimae majengo yale yamegeuka msitu wa Serengeti.

Mhe. Spika, si hasha ukaambiwa leo Kiwengwa kumetokea simba au chui kutokana na msitu wa hoteli, kwa sababu hoteli imegeuka msitu. Sasa bora tungesema tungeweka katika hifadhi ya *forest*, tusingesema tena eneo lile ni la uwekezaji. Kwa sababu mheshimiwa mmeharibu sana unapoona picha zake ili hoteli halafu pia tumekosa mapato mengi, tunawatia hatiani wananchi wetu waliyokuwa wakivisambaza pale vitu, mpaka leo wanaishia Mahakamani wengine wabakie kununiana na wala hakuna wanachokipata. Mhe. Spika, nalo lile ningeomba sana, sheria hiyo ituletee haraka sana kumpa uwezo *ZIPA* ili likitokezea tatizo kama lile aweze kulitatua ili kuokoa watu wengine wasiathirike katika madeni haya tunayodaida.

Mhe. Spika, ukurasa huo huo katika sheria hii hii ya mafuta. Mimi nakubaliana naye Mhe. Waziri kuwekwa kwa sheria hii ya mafuta ya ongezeko la kodi nisingekuwa na tatizo kubwa sana. Lakini ninachosema pamoja na hayo yote, hapa nina wasi wasi nisichangie sana kwa sababu juzi tulipitisha sheria ya nishati hapa. Sijui ile itakuwaje na sheria hii, itakubaliana wakati ile nishati tumesema tutakuja kuwapa uwezo na watakuwa na uwezo wa kuangalia viwango vile vya *quality*, yaani mafuta yenyewe na kuweza kupanga bei. Sasa hili sijui itakuwaje Mhe. Waziri naomba uje unisaidie kidogo kunifafanulia pamoja kuwa naendelea kuichangia lakini baadae uje kunisaidia kuwa haitopingana na ile sheria tuliyoipitisha hapa ya nishati na hii. Ikiwa ni hivyo *final* hakuna tatizo lolote mimi nakualiana nalo, sina utata na hilo.

Mhe. Spika, niseme ukweli wimbi la kuingizwa mafuta kinyume na utaratibu limekuwa kubwa sana na linaongezeka siku hadi siku. Mpaka vichochoroni sasa hivi mafuta yanauzwa. Kwanza ni hatari kwa kuwa kile kitu kinaitwa *petrol* na sehemu nyengine nyumba zetu za makuti. Lakini pia si vizuri wakati serikali nayo tunategemea kupata kodi ili ituwezeshe katika kuendesha serikali yetu kutupatia madawa, kutupatia mambo mengine kwa jamii. Kama ilivyosema Kamati yangu na hasa ikipata upungufu wa masuala ya umeme kupunguzika bei nayo hiyo inaweza ikasaidia, ikaona serikali kwa kuwa inakusanya mapato mengi ya mafuta basi kuna vitu vyengine wananchi tuwapunguzie. Hilo nakubaliana nalo, hapa unatakiwa ukaze kamba si kitu cha masihara kabisa.

Mhe. Spika, kama nilivyokwambia kuwa meli zinakuwepo nje, watu wanakwenda kuchukua mafuta kinyemela, tena matangi kwa matangi. Hicho kitu sio cha masihara. Ukiangalia serikali imeshakosa kodi kabisa. Usiwaonee haya watu Mheshimiwa. Kuna wengine wanasema na wakubwa wanashiriki lakini ni nani, siwezi kumjua. Lakini hilo lipo tunalokwambia na itafika wakati wake tutaambizana kwamba mkubwa fulani anashiriki katika ubia ule au tenda ile ya kuwapa watu *power* kuweza kuingiza vitu kwa siri. Hilo nalo tulione, mambo mengine tupunguziane.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 4 huu kuna neno hili ambalo linanipa tabu sana. Sijui tuseme ndio mtepeto sijui au vipi, hapa katika kifungu kinasema bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha namba (1) Kamishna atakuwa na uwezo wa kuzuia au kutaifisha bidhaa yoyote ya mafuta ambayo atakuwa na sababu ya kuamini kuwa hayajalipwa kodi au yameingizwa kinyume na sijui kuna kitu kimeongezeka hapa "taratiobu". Hapa naomba Mheshimiwa unisahihishe hapa kwamba hii "o" imeingia kwa makosa au ni neno katika lugha ya usanifu. Maana siku hizi kuna watu wana usanifu wa lugha, naomba sana Mheshimiwa hilo unisaidie.

Mhe. Spika, hichi kifungu mimi nakubaliana nacho, tena nasema kabisa Kamishna sasa asikae kwenye meza tu, akazungusha kiti akapata *AC*. Kifungu hiki kishampa na tunakikubali na tutakipitisha kwa sababu waweze kufuatilia lile jambo tulilolipitisha hapa. Ni dhambi kubwa kama itakuwa hafuatilii suala hili.

Mhe. Spika, sheria hii kama itasimamiwa vizuri mimi naamini hata yale mafuta ya kiholela yale ambayo machafu tunayoletewa yataondokana. Mhe. Spika, tunapata dhiki sana ya kutokupata *quality* ya mafuta, hili suala linatuuma sana. Lakini jana au juzi nimesikia Mhe. Spika, Mhe. Waziri akisema kuwa bora aletwe mmoja tu aagizie mafuta. Mheshimiwa hili mimi sitokubaliani nalo kwa sababu moja kubwa, ukimpa fursa mmoja atajiona

yeye. Hilo Mhe. Waziri nakuomba sana lifikirie *effective* yake iko mbele kabisa. Tuliona mambo ambayo hapa karibuni suala hili nakuomba sana tusilijadili hapa, bado na wala tusilizungumze, bado kabisa, tuikamate sheria yao hawa hawa waliokuwepo sasa hivi.

Mhe. Spika, mimi nakubaliana na wewe moja tu, labda tuweke sheria ya kuwa hawa wanaoleta mafuta wasiwe na vituo, mimi hilo nitakubaliana nalo. Lakini ukiniambia kuwa Zanzibar nzima awe mletaji mmoja ndiye msambazaji, huo sasa utakuwa ulaji, kabisa. Hilo nakuomba sana Mhe. Spika, twende huu huu utaratibu tuliyokuwa nayo sasa hivi isipokuwa udhibiti tu uwe mzuri. Waachie hawa walete, watuingizie katika vituo vyao na ikiwezekana hawa wajigeuze kuwa kazi yao kuleta tu, wenye vituo wawe wengine, sawa hapo nakubaliana na wewe. Lakini kwa kuwa muda umeshutupita ndio hawa hawa wenye vituo, hawa hawa ndio waletaji, basi tuwaachie hawa isipokuwa tuwabane katika mafuta ambayo walete mafuta yaliyokuwa na *quality*.

Mhe. Spika, lakini kuna tatizo moja, utakuta mafuta, tena sheria hii ipo lakini mnaiacha. Wanangojea mafuta wakishasikia yanapanda bei huko wanafanya kwa makusudi kutokuyatoa, wanasumbua wananchi. Mhe. Spika, hakuna hata mmoja mpaka sasa hivi aliyedhibitiwa anayefanya mambo kama yale. Mhe. Spika, wafutie leseni watu kama hao, wanaleta usumbufu kwa sababu ameleta mafuta kwa kuwasaidia wananchi, lakini wakisikia kule mafuta yamepanda wakati huku nyuma wameshanunua mafuta yale kwa bei rahisi na wao wanayazuia. Hili kwa kweli tuliangalie sana hawa watu kuwa wanafanya kwa makusudi, wanapata faida mara tatu zaidi. Mafuta yakipungua inakuwa ni vigumu kupungua. Mimi nilishangaa hivi karibuni waliyapunguza kidogo tu, haikuchukua dakika mafuta yamepanda tena. Mhe. Spika, hapa tusicheze napo na kupafanyia masihara. Hapa lazima tuweze kudhibiti ili ifanyike kazi vizuri.

Mhe. Spika, kifungu hichi cha 10 kwenye sheria ya mama yenyewe hasa ya 10A. Kwa madhumuni ya kupata uhalisia wa kodi. Mhe. Spika, hili nakubaliana nalo na ni kweli kwa sababu wauza mafuta wengi hawasema hasa kwa uhakika kiwango halisi cha bei ambacho wametoka nayo huko walikonunulia. Lakini hapa wanakwambia uhalisia wenyewe wameutafuta hapa na mtaupata, ndipo watakapopata kuweka kiwango chenyewe cha asilimia. Mimi nakubaliana nacho Mhe. Spika. wafanyabiashara wengi ndio mchezo wetu huo. Hatukwambii ukweli kwamba mimi gari hii nimenunua dola elfu nne, sikwambii ukweli, hupati uhakika kumbe mambo unayajua. Mimi naomba sana kifungu hicho sina tatizo nacho na nakubaliana nacho.

Mhe. Spika, ukurasa wa 11 hapa kidogo kwenye kifungu cha 38, Waziri anayeshughulikia masuala ya ardhi baada ya kushauriana na Waziri

anayeshughulikia masuala ya fedha atasamehe kodi za ardhi kwa kipindi cha ujenzi wa miradi maalum kama inavyoainishwa na kutangazwa na Waziri. Kwa nini tusiipe Kamati yetu hapa ya wataalamu. Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri kwa nini msiingie nyinyi nakuombeni sana. Tuwaamini hawa wataalamu wetu kwa sababu wataalamu wetu ndio wataweza kufanya tathmini ya hivi viwango vya kuweza mtu kumuongezea hiyo kodi yenyewe kwa kuona taaluma, kwa sababu pale katika wataalamu wapo wa kila aina.

Mimi naomba sana mawazo yangu nasema kuwa kifungu hichi Mawaziri mmengejiondoa mkaweka watalamu hao Kamati ya Wataalamu ili iweze kutizama suala hili, kwa sababu hapa inawezekana Waheshimiwa Mawaziri hamna fani hiyo nyie mtakuwa na hapa ndio kuna mchezo ambao unachezwa. Kuna ambayo mtu kwa makusudi anakuja huko kumbe hana uwezo wa kujenga hoteli lakini basi tu, akifika hapa anajitia angalau kutafuta viwanja kuwanyima wale ambao wana uwezo wa kuja kujenga wanakuja kupewa wao. Watu wa aina hii iwe mara moja tu waweze kusamehewa sio tena mara mbili mpaka mara tatu.

Lakini kuna wengi ni kweli wana haki na wao kuongezewa zaidi kwa sababu ardhi zao wanakuwa wananyang'anywa na wamo kwenye Mahakama. Hawa Mhe. Spika, haki yao kuweza kuwatizama kwa jicho la huruma kwa sababu bado wanakuwa wanatafuta haki yao kwa mujibu wa sheria na wao utakuta wamenyang'anywa kwa mujibu ambao sheria imeona hivyo. Kwa sababu kuna kunyang'anywa mtu kwa mujibu wa sheria na kuna kunyang'anya mtu sio kwa mujibu wa sheria basi tu kuitengeneza sheria. Sheria unaweza kuitengeneza kwa kumnyang'anya mtu, lakini sio uhalisia halisi kuwa ni sheria ambayo inayoeleza kuwa jinsi gani unaweza ukamnyang'anya mtu.

Mhe. Spika, kwa kuweza kusaidia zaidi namuomba sana ili aweze kuwasaidia hawa wawekezaji wote waliokuwa wana matatizo kutokana na kesi zao wapewe kipaumbele kabisa ili kuweza kupewa muda kama huu unaojielekeza humu.

Mhe. Spika, nimalizie mchango wangu kwa kumuomba sana Mhe. Waziri hapa kwenye sehemu ya vitega uchumi. Sasa tubadilike na kubadilika kwetu tulikauka sauti kubwa sana kwa kupitisha sheria ya vitega uchumi Zanzibar. Lakini bado nasema hatujawapa uhuru zaidi, utakuta mtega uchumi analeta wawekezaji anawapitisha kwa mujibu wa sheria, lakini Idara ya Ardhi inawafutia wale watu kinyume na utaratibu. Hebu tuangalie ipi tuipe *power* hapa kwenye sheria zetu hizi mbili kati ya Idara ya Ardhi na watu wa Uwekezaji, kwa sababu mwekezaji *ZIPA* anamuangalia kwa mambo yake yote mpaka mwisho anampitisha kwa Tume ya Wataalamu kwamba

wameridhika naye lakini hatimaye unakuta hajachukua muda mtu yule kishanyang'anywa ardhi.

Mimi naomba sana Mhe. Spika, tuiangalie sana sheria hiyo, tuwaachie hawa, tuwape *power* hawa *ZIPA*, ndio watatuletea uchumi sasa hivi Zanzibar. Tuwape kabisa fursa na tuwaachie kila kitu, tusiwabane, tumuachie Mkurugenzi na Kamati yake ya Taaluma. Hivi karibuni nasikia kuna mradi unataka kuletwa wa kutengeneza nyumba nzuri pale Bwawani. Mhe. Spika, tuwaachia wao maamuzi anayo yeye, anajua utaalamu, anajua vipi tutavyoiweka na vipi tutahitimisha kodi Zanzibar kuna pesa chungumzima. Mimi naomba sana tumuachie Mkurugenzi na wataalamu wake waone huyu ndiye anayefaa kuleta maendeleo katika nchi yetu na kuibadilisha.

Mhe. Spika, nakushukuru sana ahsante sana naunga mkono mia kwa mia.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma na Utukufu ambaye anaendelea kuturuzuku neema zake tukiwa hai na wazima, tukiwa tunavuta pumzi tukiendelea na shughuli zetu zilizotuleta katika Baraza letu tukufu Mhe. Spika.

Pili Mhe. Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa fursa hii na mimi asubuhi hii kuwa mchangiaji wa pili wa Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha Baadhi ya Shughuli za Fedha na Kodi Kuhusiana na Ukusanyaji wa Udhibiti wa Mapato ya Serikali na Mambo Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Spika, naomba vile vile nimpongeze Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa kuwasilisha Mswada huu hapa Barazani. Mhe. Spika, Mswada huu lengo lake ni kutoa uhalali kwa hatua mbali mbali ambazo zilitajwa katika hotuba ya bajeti ambazo zitapelekea kuimarisha ukusanyaji wa mapato. Lakini vile vile kama kuna haja ya kutoza kodi basi kuhalalisha utozaji huo wa kodi mpya; na kabla sijaingia katika maudhui ya Mswada, mimi nilikuwa na malalamiko fulani ambayo nataka niyaseme hapa.

Mhe. Spika, kwanza ni tofauti na hotuba ambayo ni maneno tu, hapa tunajadili Mswada wa Sheria, tunapoujadili tunatakiwa tuwe makini sana, kwa sababu neno moja linaweza likatoa athari kubwa au tofauti na ilivyokusudiwa. Sasa tungepewa *draft* ya serikali, ni jadweli ambalo mara nyingi huwa tunaliomba lije kutuonesha sheria iliyokuwepo na inayorekebishwa, wanachelewa tumepewa asubuhi hii, waraka wenye kurasa 25 unaorekebisha sheria nafikiri kwa jumla ziko kama 10.

Mhe. Spika, kwa muda mchache ambao umeshapitia ule waraka unataka kujikumbusha halafu uje upitie na haya kidogo inakuwa kazi kubwa sana. Kwa hivyo nasema ili tutumie haki angalau siku moja kabla tupewe wajumbe wako ili tuupitie kwa kina, kwa sababu mara nyengine hasa kwa wajumbe ambao pengine si wana sheria ambao inaweza ikawa ndio wengi humu ndani, inaweza ikawa ni kazi kubwa zaidi kuwaelimisha mambo haya kwa wakati mmoja.

Lakini, moja nataka nipongeze huu utaratibu aliokuja nao Mhe. Waziri wa kuja na huu waraka kuhusu mapendekezo ya kubadilisha sheria mbali mbali zinazohusiana na Mswada wa Udhibiti wa Mapato ya Zanzibar ambayo imefafanua. Sasa maelezo sio katika yale ya kisheria, yale malengo ya sheria ambayo imekusudiwa kufanyiwa marekebisho.

Mhe. Spika, jengine la jumla ambalo nilikuwa nataka nilizungumze katika hotuba hii ya bajeti hizi hatua za kuimarisha mapato zilitajwa katika ukurasa wa 38, kwenye hotuba ya Waziri hadi ukurasa wa 54. Kimsingi utaona kwamba kwa sababu hotuba hii inatoa muelekeo wa kuongeza mapato serikali labda mambo mbali mbali ambayo yataletwa pale na lugha iliyotumika katika hatua mbali mbali.

Kuna mambo ambayo yameguswa na sheria Mhe. Spika, lakini kuna suala jengine la ada au kodi ambazo mamlaka yake imewekwa kwa zile za kuamua viwango. Sasa humu Waziri kapendekeza lakini sisi katika utaratibu huu tutakuwa hatuna mamlaka yoyote ya kuweza kuzikubali au kuzikataa kwa mujibu wa utaratibu wa kisheria. Katika hatua zilizopendekezwa humu kwa mfano katika hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi alikuwa na maeneo mawili. Moja lilikuwa linahusu marekebisho ya utaratibu wa malipo ya leseni ya njia ilikuwa kifungu (f). La pili kwenye kifungu (g) marekebisho ya viwango vya malipo ya leseni za udereva.

Mhe. Spika, haya Waziri kapendekeza lakini sisi hatuna njia ya kusema kama tunayakubali au tunayakataa. Njia yetu pekee ilikuwa ya jana katika kupitisha hotuba ya bajeti. Sasa nilikuwa nataka kusema hili kwamba sijui tutaangalia mfumo gani mpya wa kuweza kutupa na sisi sauti katika haya, kwa sababu hotuba ya bajeti haidhinishwi kwa vifungu, sasa unapoidhinisha yote kwa pamoja na huwezi pengine ukaipinga kwa sababu hutokubaliana na eneo dogo kama hili tu pengine,

Mhe. Spika, nilikuwa nataka kusema kwamba tusijenge utaratibu kwamba yale mambo ambayo hayaguswi moja kwa moja katika marekebisho ya sheria katika kurekebisha viwango vya kodi au utozaji wa ada inakuwa sisi hatuna

sauti, inabidi tupitishe tu. Baada ya kusema hayo sasa naomba niende katika Mswada.

Kwanza mimi nawapongeza kwa hatua ya jumla ya serikali ya kufikiria kuja na hatua za kudhibiti ukusanyaji wa mapato ya serikali katika maeneo mbali mbali. Kimsingi marekebisho yaliyokuwa yametajwa katika sheria hizi yamelenga huku na hili linaonekana ni jambo la kupongezwa kwa sababu sisi Wawakilishi wa wananchi mara nyingi katika Baraza hili sisi wenyewe tulikuwa tunaiambia serikali kwamba idhibiti sehemu ya uvujaji wa mapato. Lakini kusema hivyo Mhe. Spika, nadhani maeneo mengine ni kuungana na yale misingi ya utawala wa sheria ambayo inatambulikana duniani lakini vile vile ambayo itapelekea kuimarika kwa uchumi. Mimi nina maeneo machache Mhe. Spika, naomba kuyatolea maoni na mengine ambayo sijayaelewa hadi nipate ufafanuzi wa Mhe. Waziri.

Kwanza nipongeze marekebisho ya Sheria ya Bandari ambayo sasa yametoa ruhusa kwa Kamishna kuomba hata msaada katika kuzuia au kuondoka au kuchukua hatua yoyote ambayo itapelekea ulipaji wa kodi, ada, malipo, faini au riba, imelipwa kama inavyotakiwa kwa vyombo vikiwa kwenye Bandari au Uwanja wa Ndege.

Mhe. Spika, naomba nipongeze kwa sababu karibuni kumejitokeza suala ambalo nadhani labda lilikuwa ni msingi wa marekebisho hayo kwamba bodi ya Mapato ya Zanzibar (*ZRB),* imetoa toleo la kuitaka mamlaka ya viwanja vya Ndege Zanzibar kuzuia ndege za *Precision Air* kwa sababu zinadaiwa fedha nyingi hapa. Lakini ukatokezea mvutano katika suala hilo, baina ya Mkurugenzi wa *ZRB* na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ambaye yeye alikwemda kwa maslahi ya kibiashara hakuona haja ya suala lile kwa sababu ni mambo ya kibiashara mnaweza kuzungumza mpaka hicho chombo cha *ZRB* ambacho chenye mamlaka ya kukushanya kodi kimeshapewa lakini kakwamishwa.

Mhe. Spika, sisi katika Kamati tulilihoji hili, lakini maelezo yalikuwa ni hayo. Sasa pengine kwa sababu Kamishna haina nguvu za kisheria alikuwa hana uwezo sasa wa kutaka au wakutoa maelekezo kwa Mkurugenzi Mkuu kwamba asiweze kukwepa kwa sababu sasa ni suala la kisheria. Sasa nawapongeza kwa hatua hii kwa sababu nadhani itatupelekea pale kupata yale malipo yetu.

Mhe. Spika, haya mambo ya msingi palikuwa na malimbikizo pale ya deni la *ITC*, mpaka nimeliuliza katika Kamati yako ya Maslahi na Ujenzi, tukaambiwa sasa lile kama liambiwe basi tu, limekufa. Sasa haiwezekani Zanzibar ikatumika hapa kwamba sisi kila siku tunaimbiwa nyimbo, deni la

TANESCO wee! lakini wao wanavyodaiwa wala hawakumbushwi kwamba labda wanadaiwa. Mimi nilipotoa habari baina ya *Precision Air* kama hawatochukua na wengine, kwa sababu kama hakuna (*incentive)* hakuna nguvu ya kutengeneza sheria na kwamba kila mtu akiona kwamba anaweza kuja pale ikawa kama ngarawa ya Juma Faraji Uwanja wa Ndege wetu anakuja anaondoka hakuna cha kulipa Mhe. Spika, hatuwezi kufika. Kwa hivyo naipongeza sana serikali kwa kuliona hili la kuleta marekebisho haya.

Lakini upande wa pili Mhe. Spika, sehemu ya tatu ya sheria hii inarekebisha Sheria ya Kodi ya Hoteli.

Sheria hii Mhe. Spika, mimi kidogo nilikuwa nataka ufafanuzi, katika marekebisho yaliyoletwa kifungu cha 5 cha mswada kinasema,

> "kifungu cha 5 cha sheria mama kinafutwa na kuweka badala yake kifungu kipya cha 3 kama ifuatavyo"

Sasa mimi nataka niulize zaidi masuala yangu katika kifungu cha 3 (3) kinasema mapendekezo,

> "Waziri anaweza baada ya kushauriana na Kamishna chini ya jadweli la sheria hii kupanga viwango maalum vya kodi ya hoteli mbali ya viwango vilivyowekwa chini ya kifungu kidogo cha kwanza cha kifungu hiki".

Sasa Mhe. Spika, kijifungu cha 1 cha kifungu hicho kimezungumzia asilimia 18 ambayo tunayoijua. Hapa inatoa mamlaka kwa Waziri baada ya kushauriana na Kamishna kuweza kupanga viwango maalum, hebu atufafanulie zaidi hapa kwamba nini vitakuwa vigezo. Kwa sababu sisi Mhe. Spika, tuna uhalali huo katika Baraza hili sasa lazima tujue uhalali huo tunataka kumpa Waziri na Kamishna kuweza kupanga viwango nje ya vilivyokusudiwa hapa nini vitakuwa vigezo vyake na lengo lake nini? Kutoa unafuu au kuongeza mapato kwamba kuna mengine yatakuwa labda anazalisha zaidi hatujaambiwa kuwa hoteli ziko tofauti viwango. Lakini ninajiuliza vigezo vitakuwa hivi hofu yangu Mhe. Spika, na wanasheria watanifahamu kwamba mara nyingi unatoa mamlaka kwa mtu mmoja kuamua chini ya ile ndio inaitwa *decision power*, ninafikiri mwenyewe unaelewa, maana ni mtaalamu wa fani hii kwamba unapoiachia tu ile nafasi kama ina vigezo vya kuweza kutumika vibaya.

Sasa hapa hofu yangu mimi ukimuachia Waziri na Kamishna kunaweza kuja kukafanyika mambo fulani watakubaliana huko, kwa sababu hapa Waziri hatumtizami alivyowekwa katika nafasi hii sasa hivi, Waziri atakuwa yeyote.

Kesho Mhe. Rais anaweza akafanya mabadiliko akasema badala ya Mhe. Omar Yussuf Mzee kuanzia sasa Mhe. Mussa Ali Hassan kwa sera zake zile nzuri alizotutolea jana awe Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, sasa Jussa akakataa, basi anasema katika hili najiuliza anaweza kuja kutu-*work out* tusimtazame mtu tunapotunga sheria. Kwa hivyo hii nasema tuekewe vigezo hasa vilivyokusudiwa hapa. Lakini zaidi Mhe. Spika, kwa sababu haimalizii hapo tu kijifungu hicho nne cha hicho hicho cha tatu kinasema,

"Waziri anaweza baada kushirikiana na Kamishna kwa tangazo litakalochapishwa kwenye gazeti kurekebisha, kubadilisha, kuongeza kwenye jadweli la sheria hii".

Sasa atusaidie pia hapo kwamba madaraka haya makubwa mmempa Waziri kwa kushirikiana na Kamishna najua ni utaratibu wa sheria kwamba unaweza kubadilisha *schedule* lakini kwa kiasi gani naona kama mambo yaliyotolewa hapa ni makubwa sana, kwa hivyo naomba nielezwe ili niridhike na mimi nije niyapitishe marekebisho haya.

Mhe. Spika, lile la kupinga kanuni naweza niseme hapa linafaa kuwepo hili ninalipongeza kwa sababu na mimi nimeshtuka nilikuwa sikujua kwamba kuna baadhi ya sheria zetu zilikuwa zinamnyima Waziri uwezo wa kutunga kanuni. Ni lazima na ni kawaida kwa sheria zetu kuwa na utaratibu kama huu kwa sababu kuna mambo mengine ambayo ni ya undani hayawekwi katika sheria, yanaweka utaratibu Waziri kutunga kanuni, kwa hivyo hili ninalipongeza.

Jengine Mhe. Spika, ninalolipongeza ni sehemu ya nne ambayo inarekebisha sheria ya kodi ya mafuta namba 7 mwaka 2001. Hili ninalipongeza kwa sababu sina wasi wasi, sina haja ya kutoa maelezo zaidi wenzangu wameshasema sote tunajua kwamba kumekuwa na ukwepaji mkubwa wa kodi za mafuta. Lakini hapa pamezungumzwa suala la magendo ya mafuta, hili hatutoliweza kwa kurekebishwa sheria tu Mhe. Spika. Hili naomba Waziri na Serikali kwa ujumla basi tutajadili kwa pamoja humu ndani na litazamwe kwa ujumla wake.

Kuna wajumbe walizungumza na mimi nashawishika kuamini hivyo kwamba inawezekana kuna wakubwa katika serikali hii wananufaika na masuala haya. Mhe. Spika, nitatoa mfano mmoja tu katika hii Kamati uliyonipeleka karibuni ya Mawasiliano na Ujenzi, tulikuwepo Pemba mara hii ziara yetu yote tumeifanya Pemba ya ukaguzi. Kuna maagizo ya kamati tangu ilipokuwa inaongozwa na Mheshimiwa Mwanasheria mkubwa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, walitoa maagizo mazuri kwamba uongozi pale wa Polisi, *ZRB, TRA*

na Wizara kupitia Ofisi Kuu ya Wizara ya Ardhi Makaazi Maji na Nishati na wale watu wa *GAPCO* wakae pamoja watafute ufumbuzi lakini utapatikana vipi ufumbuzi ikiwa Polisi wenywe leo watakwenda kubeba mafuta katika vituo visivyofahamika. Wameturipotia wenyewe watendaji kwamba magari ya Idara za Serikali wanakwenda kutia mafuta katika vituo visivyofahamika. Sasa hapo ukisema kuna maslahi ya baadhi ya watu itakuwa unakosea Mhe. Spika. Kwa hivyo nasema hili ninalipongeza lakini mimi siamini kwamba tutaweza kuongeza mapato kwa kurekebisha sheria hii, kunahitajika usimamizi wa sheria.

Nasema Mhe. Spika, bado serikali ikae izingatie na kama nilivyosema mimi nastaajabu kwamba tunaweza kuyadhibiti magendo ya karafuu hapo ikawa karafuu watu wanakwenda kuanika kutoka upande mmoja au upande wa pili lakini vyombo hivyo hivyo, umati ule ule hauonekani katika kudhibiti magendo ya mafuta, kuna nini hapa Mhe. Spika, na kwa babu hili pia linapelekea Mhe. Spika, athari kwa wananchi mafuta yanayoingi chini ya viwango, vyombo vya watu vinaharibika, mwananchi maskini alikuwa akiwakamua kila siku anapata hasara kwamba hivyo hili serikali ilitizame kwa upana wake.

Mhe. Spika, naomba vile vile nipate maelezo katika marekebisho ya sheria kodi ya stempu. Hapa imeelezwa kwa jumla jumla tu haidhuru ninayoyazungumza yanahusu kifungu cha 12. Mhe. Spika, utaratibu ni mzuri kwamba yule ambaye hakusajiliwa katika *VAT*, basi awe analipa kodi kwa kutumia njia ya ushuru wa stempu. Lakini hapa hebu nimuulize Mhe. Waziri, moja ambalo tulilizungumza sana katika kuchangia bajeti tulisema kwamba bajeti nzuri huwa inatoa motisha kwa watu wengine kuweza kukuza vipango vyao kwa njia fulani. Kwa hivyo kwa serikali kuwalea kwa kuwapa pengine unafuu wa kodi ili baadae wakuze biashara na zikifikia kiwango fulani serikali itakuwa inapata nia ya kukusanya kodi kubwa zaidi.

Mhe. Waziri analijua kwa sababu ikiwa Naibu Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano alichukua hatua kama hii kwa upande wa Bara kulitangazwa biashara nakumbuka ilikuwa mpaka milioni 20 kwamba hii hailipwi kodi ya aina yoyote. Leseni zile ziliachiwa ili wapate kujikuza. Lakini mwaka jana au mwaka juzi ikaondoshwa hii kwa sababu gani wameshapewa motisha ya kutosha, wamenyanyuka sasa biashara imekuwa sasa serikali ikiamua kutoza kodi inapata kodi kwa wingi zaidi na kwa viwango vikubwa zaidi.

Sasa katika hili ushuru wa stempu wafanyabiashara wetu wa Zanzibar wanapiga kelele sana na wakati ule lililopotokezea walijilinganisha wakasema kwa nini kule wanapewa unafuu lakini hapa Zanzibar hawapewi unafuu kama huu, na ndio ninapokuwa na suala Mhe. Spika, kwamba inapokuja

kusawazishwa kodi au marejesho sote sisi tumesababisha kodi, lakini katika kusawazisha unafuu wa kodi Zanzibar hainufaiki. Kwa hivyo nasema, hebu atwambie Waziri anafikiria nini katika masuala hayo nilikuwa naomba atupe maelezo.

Mhe. Spika, katika sheria ya kodi ya ongezeko la thamani kwa jumla sina matatizo nayo, katika marekebisho ya sheria ya usimamizi wa kodi ninafurahi kwamba kuna kifungu kimeongezwa hapa katika kifungu cha 20 cha mswada ambacho kinasema kifungu cha 5 cha sheria mama kinarekebishwa kwa (a) kuongezwa kijifungu kidogo cha 5 kama ifuatavyo:

"Mtu yeyote atayesajiliwa kulipa chini cha ya sheria ya kodi kwa bidhaa na huduma hatolipa kodi nyengine kwa bidhaa na huduma hizo hizo".

Hili naomba lisimamiwe tu Mhe. Spika, ili ile nafuu iliyokusudiwa kupatikana isiwe mtu anatozwa kodi zaidi ya moja kwa bidhaa ile ile basi ipatikane kwa mlaji, nilikuwa naomba lisimamiwe vizuri.

Mhe. Spika, nilikuwa naomba vile vile kuzungumzia hili la kifungu cha 24 cha mswada kinachorekebisha kifungu cha 32 cha sheria mama kwa kuongeza vifungu vipya vya 3, 4, na 5. Hapa vile vile naomba nisaidiwe tu kwamba kifungu hiki kinasema,

"Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha 1 cha kifungu hiki, Kamishna anaweza kutaka malipo yoyote yafanywe kabla ya tarehe ya malipo kwa muda ambao Kamishna ataweka kwa mtu yeyote anayetengeneza bidhaa ambazo zinatozwa kodi chini ya sheria za kodi au anaingiza bidhaa au huduma zinazopaswa kulipiwa kodi".

Mhe. Spika, mimi nataka nipate maelezo kwa sababu kwa jumla kodi inalipwa kutokana na kufanyika mauzaji na manunuzi. Sasa hii tunaposema tunataka mtu alipe kodi kabla ya bidhaa umesema hapa kwamba bidhaa zinazotengenezwa mara tu baada ya bidhaa kutolewa kiwandani kabla haijauzwa na bidhaa zinazoingizwa wakati inaingizwa kabla haijauzwa. Sasa hebu tusaidiwe hili kwamba linaendana na misingi ya usimamizi wa kodi.

Mhe. Spika, vile vile kwenye kifungu cha 26 cha mswada kwenye kifungu cha 26 kwa jumla yake kuna marekebisho hapa kwa sababu ya muda wako sitaki nikisome kimoja kimoja, lakini vile vile ameweka utaratibu wa kumuweka madaraka makubwa Kamishna kwamba yeye anaweza kuamua na akarekebisha na jadweli. Lakini vile vile kuna kwa mfano kijifungu cha 46(c) kinachoongezwa, kifungu kidogo cha 3 (a), (b), na 2 (a), (b), hapa yametolewa madaraka makubwa kwa Kamishna peke yake kutoa tafsiri ya

sheria kuhusiana na kodi ambayo imempa mamlaka. Sasa nilikuwa ninajiuliza huu ni utawala bora Mhe. Spika, kwamba tunampa mtu mmoja tu kutoa tafsiri ya sheria na yeye ndiye msimamizi wa sheria hiyo halafu akaichapisha ndani ya gazeti tu ikawa tayari tafsiri imekubalika hiyo. Nilikuwa naomba kwamba hili liwekwe wazi vizuri zaidi.

Mhe. Spika, naomba nitoe indhari ndogo vile vile katika sehemu ya 8 ya mswada huu, marekebisho ya sheria ya rufaa ya kodi, hapa ndio lile lile swali kwamba tukipewa ghafla tutapata tabu sana, lakini hiyo kupewa ghafla nimegundua kitu hapa kinaleta matatizo. Katika mswada aliotuletea Mhe. Waziri Kifungu cha 31 naomba akitizame cha mswada kinasema:

"Kifungu cha 16 cha sheria mama kinafanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:

a) Kwa kufuta maneno asilimia kumi na tano yaliyopo baina ya maneno kulipa na ya kwenye kifungu kidogo cha (2) na kuweka badala yake neno thuluthi moja".

Lakini nikija nikisoma maelezo yaliyotoka kataja marekebisho kutoka asilimia hamsini kuwa elfu moja. Mimi jana niliposoma hii nilishtuka kwamba vipi tunampandishia mtu kodi ambayo hatukuombwa, lakini leo niliposema naona kwamba tupunguze kutoka asilimia 50 mpaka thuluthi moja. Sasa hii sisi tunapitisha mswada hapa, tukiiachia hii Mhe. Spika, inatupa matatizo, kwa hivyo nikasema hicho pia akitizame.

Mhe. Spika, nimalizie vile vile kupongeza hii hatua ya sheria ya ardhi marekebisho yake kwamba tunasema kuanzia sasa sio tu Waziri wa Ardhi aamue peke yake, lakini ashauriane kwa maandishi kukubaliana na Waziri wa Nchi Anayeshughulikia Fedha katika kutoa punguzo la msamaha wa kodi katika masuala haya. Hii ninalipongeza na vile vile kupunguza ule muda Mhe. Spika, kwamba ukiwa mswada huu ni kwa miezi kumi na nane, ikiwa baada ya hapa hajaendeleza basi bila shaka serikali itakuwa na uwezo wa kuchukua hatua nyengine.

Ninalipongeza na nitofautiane kidogo na Mwanasheria mkubwa aliposema kwamba tuwaachie wataalam. Mimi nadhani kimsingi madaraka katika chombo yanatolewa kwa Waziri kwa sababu ndiye anayesimamia sera ya serikali. Sasa wao bila shaka na wataalam wao watakuwa wanashirikiana nao lakini kimsingi ni kwa Waziri lakini ile kwamba imeondoshwa kwa mtu mmoja na sasa wamepewa angalau watu wawili, inanipa imani Mhe. Spika, hasa sehemu ya pili inayoshughulikia fedha kwamba pale patalindwa.

Kwa hivyo Mhe. Spika, niseme baada ya hayo ninauunga mkono mswada nategemea nitapata maelezo kwa yale ambayo nimeyaeleza kidogo, sijayazungumza kifungu kimoja kimoja kwa sababu yanafanana kwamba vifungu vile vingi vimepewa madaraka makubwa kwa mtu mmoja mmoja wawili, lakini havijawekwa uwazi kwamba vitahakikisha kwa sababu Mhe. Spika, katika masuala ya fedha tunaambiwa ni muhimu kuwa na *certainty of tax regime* lakini vile vile kusiwe na *surprises* katika masuala ya kodi, hayo ndio yanayowavutia wawekezaji. Kwa hivyo nataka haya tuweke wazi ili tusiwape madaraka mtu mmoja au wawili wakaamua peke yao.

Mhe. Spika, ninakushukuru sana kwa kunivumilia niseme naunga mkono hoja baada ya kupata ufafanuzi huo. Ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, na mimi nataka nikushukuru kunipa nafasi hii na mimi nikazungumza machache katika kuingiza nyama mswada huu wa sheria ya kutoza na kubadilisha baadhi ya sheria za fedha za kodi. Lakini vile vile na kusimamia ukusanyaji na udhibiti mapato ya serikali.

Mhe. Spika, mimi nataka niendelee kumpongeza sana Mhe. Waziri wetu anayeshughulikia masuala ya fedha na uchumi kwa kazi nzuri aliyoifanya, lakini vile vile kwa usikivu wake, bajeti ya serikali tumeichangia hapa, Mhe. Waziri alionesha ufundi mkubwa sana wa kutoa ufafanuzi sio wa kujibu, wa kutoa ufafanuzi wa hoja za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Jana alitoa staili ya aina yake hakumtaja mtu mmoja mmoja, kwa sababu alijua kwamba ile hoja siyo ya ile mjumbe aliyoitoa, zile hoja zilikuwa ni za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar.

Kwa kweli kuna rafiki yangu mmoja ninafikiri sasa hivi ananisikia, akanambia yule Mhe. Omar Yussuf ni mtu hatari sana, hatari yenyewe sio hatari kwamba umuogope lakini mtu makini anayejua akili za watu na anayejua wanataka nini na wanakusudia nini na nini awafanyie. Maana jinsi zile hoja mlivyokuwa mkizizungumza, jinsi alivyokuja kujibuni kijumla jumla, kwa kweli yule mtu bwana anafaa kuwa Waziri anayeshughulikia masuala ya fedha na uchumi. Sasa Mhe. Spika, sifa hizi sio zangu maana yake mimi ninazungumza kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura na wananchi wote wa Zanzibar. Mhe. Waziri ninakupongeza.(*Makofi*).

Mhe. Spika, mimi ninashukuru sana kwa kusema kwamba pamoja na hizi kodi tunazokushanya tunaangalia leo tukamue wapi, kesho tubane wapi lakini kitu kikubwa ambacho tulikuwa tunahisi kama hatujakifanya hicho, basi bado kwa kuingia katika ushindani wa kiuchumi katika Bara la Afrika kama hatujaweza kufanikiwa kitu hicho basi bado tutaendelea kujikamua sisi wenyewe hivi hivi. Sasa nilifurahi sana niliposikia kasema kwamba si muda

mrefu, sio kwamba wako mbioni maana hizo mbio zishafikia ukingoni kwamba mchakato wa ujenzi wa bandari ya Mpigaduri nadhani umefikia pahala pazuri.

Mhe. Spika, mimi nataka nimwambie Mhe. Waziri wetu wa Fedha, wananchi wa Zanzibar hawana matatizo, wananchi wa Zanzibar hawana mashaka yoyote, tatizo lao kupata rizki ya kula, kusomesha watoto wao, pamoja na pahala pa kukaa hilo ndio tatizo la wananchi wa Zanzibar. Sasa serikali yetu imeanza kulizungumza hili kwa muda mrefu tokea awamu ya pili, ya tatu, ya nne, ya tano, tunashukuru serikali hii ya awamu ya saba kama wataweza kusaini mkataba ujenzi wa bandari ya Mpigaduri Mhe. Spika, yale maneno tuliyokuwa tunazungumza humu mpaka leo mwaka wa pili na nusu hatujaona jambo jipya. Mhe. Spika, unaweza ukafanya mambo mapya 10 wananchi wasione umefanya chochote cha maana. Lakini ukifanya moja tu lakini wananchi watajua kwamba hapa jamaa walijitahidi. Kama mtafanikiwa hili mtakuwa mmejitahidi kweli kweli.

Na kwa sababu gani? Eneo hili litaweza kufungua lango na kuitangaza Zanzibar kiuchumi kama hapo ilivyokuwa mwanzo kwamba Zanzibar ni kitovu cha biashara katika nchi za Afrika Mashariki. Mhe. Spika, nataka Mhe. Waziri aendelee na jitihada na tunamuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu basi kipindi hiki aache shughuli nyingi alimalize hili ili tuweze kuwa na kianzio kikubwa zaidi cha uchumi katika nchi yetu.

Lakini jengine Mhe. Spika, kabla sijenda moja kwa moja katika mswada, unajua hapa tunazungumzia tunatunga sheria ya kurekebisha baadhi ya kodi, kama tungekuwa tuna mambo ambayo vianzio vyengine vya kodi, basi kodi hizi tungezibakisha hivi hivi wala isingekuwa na matatizo, lakini kwa kuwa hatuna mahitaji yanayooongezeka inabidi sasa tuangalie je, tutanyokoa wapi ili kuweza kujazia nyama hii.

Sasa kuna eneo Mhe. Spika, jengine ambalo tumelizungumza sana nataka nilizungumze zaidi, Mhe. Waziri kama ataweza kujitahidi ndani ya kipindi hiki kilichobakia, kuweza kumaliza *master plan* na vile vile kuweka miundombinu katika maeneo huru ya kiuchumi, Fumba na Micheweni. Mhe. Spika, humo ndio kwenye uchumi. Juzi Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alikuwepo nchini China kwa bahati sisi tulimtangulia sisi tulikwenda kaja kamaliza shughuli zake kaondoka sisi katubakisha kule kule. Tulikuwa tunafuatilia ziara ile. Mhe. Spika, naamini kuna wawekezaji kutoka China wameahidi watakuja kuekeza Zanzibar.

Sasa leo Mhe. Spika, ikiwa wamekuja wawekezaji wa viwanda kutoka China wanataka kuja kuekeza hayo maeneo yetu huru hakuna *master plan*

hatujaweka miundo mbinu wanakuja kuekeza wapi? Kwamtipura tushajenga kote sisi. Sasa wakati tuna maeneo huru tumeyaweka tena mkakati wa muda mrefu lakini bado katika ile mipango yetu katika MKUZA *vision 2020*, yote imo lakini bado katika ule mpango wa muda mfupi. Mimi ninafikiri mpango huu kwa ndani ya mwaka ujao japo ile miundombinu atakuwa hajakamilisha lakini naamani akiweza kukamilisha ile *master plan* basi alau akija mwekezaji unamwambia pale na kuna mwenzangu mmoja aliwahi kuzungumza hapa kwamba wenzetu China anakuja mwekezaji anapeleka barua ya kutaka kuekeza anajibiwa siku ile ile au siku ya pili yake.

Kwa sababu wenzetu wameanzisha maeneo huru ya kiuchumi, wameweka tayari wewe ukenda unakuta *carpet* imeshatangazwa siku ya pili unaekeza. Sasa Mhe. Spika, ninamuomba sana Mhe. Waziri wetu kama wananchi wanavyomsifu hebu ajitahidi na hili la kumaliza hii *master plan* ya maeneo huru halafu tuangalie katika fedha tunazoziomba kwa washirika wa maendeleo na zile za ndani tuanze kuweka maeneo ya miundombinu ya kiuchumi.

Mhe. Spika, jengine kama wataweza kujitahidi katika kipindi hiki kilichobakia nilizungumza sana suala la uekezaji katika ujenzi wa nyumba za makaazi na wananchi. Ninashukuru sana tayari serikali hii wameshaanza kuwa na huu mpango na wameshazungumza na *ZSSF* katika suala zima la uekezaji katika *real estate.*

Mhe. Spika, nimemsikia sana Mhe. Waziri lakini bado sijui uwezo wa mfuko wa hifadhi ya jamii na taasisi za kifedha zilizokuwepo hapa nchini kwetu, kwa kweli wameweza kuwa na fedha ya kuweza kubadilisha sura ya nch wetu Zanzibar, ninapozungumza Zanzibar ni Unguja na Pemba. Mhe. Spika, wenzetu China sasa hivi mfumo wao wa serikali umekuwa kama serikali za Mikoa au serikali za Majimbo kama kila *pages* wana mipango yao ya kuendesha nchi yao. Mhe. Spika, sasa hivi wenzetu China kila mji unapokwenda kuna *construction* zinaendelea, kuna ujenzi unaendelea wa makaazi ya wananchi. Mhe. Spika, leo wananchi wa China mpaka yale maeneo ambayo ya kuendea vijijini sasa hivi wanaishi katika nyumba za kisasa tena za ghorofa.

Mhe. Spika, nimeshauri vile vile katika hii sheria ambayo tunaifanyia marekebisho sheria ya kodi ya ardhi. Mhe. Spika, Zanzibar ardhi yetu ni ndogo, leo hatujaweka masharti ya kulazimisha wawekezaji kujenga majengo ya ghorofa. Leo Mhe. Spika, tumewahi kuzungumza na *tours guide,* mmoja tulipokuwepo China aliyekuwa anatutembeza katika miji mbali mbali, tukajaribu kumwambia kuhusu suala la je hayana connection yoyote ya Zanzibar? Alipata tabu sana kuitafuta yeye Zanzibar. Sasa tukajaribu

kuzungumza nae tukajaribu kumshauri tukamuelezea Tanzania, halafu kuna kidoto kidogo ndio kuna Zanzibar, sasa akatwambia Wachina sasa hivi wana pesa nyingi sana. Kama tutaweza kufungua utalii Mhe. Spika, sisi hatuna hoteli sasa za kuwalaza Wachina, hatuna kabisa kwa sababu ukiangalia hoteli zetu zina maeneo lakini nyumba zenyewe nyingi za kawaida. Sisi Mhe. Spika, tulikaa China hoteli tuliwekwa ghorofa ya 29 Mhe. Ali sijui yuko wapi, sasa leo hakuna hata hoteli moja Zanzibar alau ina ghorofa tano sijui kama ipo.

Sasa leo ukiangalia China ukubwa wake yaani lile Bara kubwa, yaani sijui mara mbili Afrika lakini wanalazimisha wale wawekezaji kwenda juu ili kuweka matumizi mazuri ya ardhi. Sasa Mhe. Spika, katika kuongeza kodi leo ukiangalia ukipiga mahesabu mita za mraba na vyumba vilivyokuwemo katika mahoteli Mhe. Spika, kwa kweli ardhi yetu tunaitumia vibaya. Mimi ninafikiri pamoja na kuwa tunayo sheria lakini bado tunayo nafasi ya kurudi tena sasa kuwaambia tunataka ujenzi wa aina gani.

Mhe. Spika, nakuja suala jengine katika suala ambalo litaweza kutusaidia kuongeza mapato lakini vile vile na kuinua kipato cha wananchi. Mhe. Spika, moja katika masomo tuliyosoma China, tulisoma somo ambalo wanaita *intellectual property.* Kwa bahati nzuri kuna sheria tuliipitisha kipindi kilichopita tulipokwenda kule tukenda tukasema sheria ile ile kumbe tukasema kumbe tumechelewa, tumeambiwa kule kwamba wenzetu hizi sheria zilianza tokea mwaka 1914 na zilianza Marekani na nchi nyengine za Ulaya. Sasa na hizi sheria zinasaidia nini? Katika kulinda ubunifu na ajira Mhe. Spika, leo sisi tunalalamika Zanzibar ajira hakuna kwa vijana, Mhe. Spika, ajira zipo nyingi lakini hatujatumia akili ni namna gani vijana wetu tutaweza kuzilinda hizi ajira zao. Nitatoa mfano mdogo, Mhe. Spika, kuna hapa vidogo vidogo vinatengeneza sabuni, laiti tungelikuwa tumeweka masharti kwamba haya wenye mahoteli waekezaji kwa sababu hawa wanapokuja kuekeza kuna misamaha ya kodi wanapata wakati wa ujenzi wao.

Sasa ile misamaha ya kodi tunayowapa zile ni fednha za wananchi kama wangalitakiwa walipe fedha zile zingalikwenda kwa wananchi. Lakini Mhe. Spika, leo hoteli hizi tushakwenda sisi tunakogea sabuni za chokaa kabisa labda ukiangalia zile *material* kwa sababu Mhe. Spika, mimi najua kupika sabuni. Kwa hivyo sabuni nilipoiona nikasema hii hawa akinamama wetu wenye viwanda vyao vidogo vidogo wana uwezo wa kupika, kwa nini tunashindwa kuwapa *condition* hawa wenye mahoteli. Kwa sababu leo unapoleta wawekezaji wasaidie kutoa ajira. Leo Mhe. Spika, wananchi wanahangaika na sabuni, wanahangaika na madawa ya kusafishia vyoo wanauza, ukenda pale Mwanakwerekwe kwenye jengo la *PBZ* utawakuta wale wananchi wajasiriamali. Kama tungeliweka *condition* ya kusema kwamba mahoteli yatumie *just* kama viwango vidogo wafahamishwe namna

ya kuweka viwango, wangeliweza kuuza sabuni za kukogea, wangeliweza ku-*supply* zile dawa za kukoshea vyoo na vitu vyengine. Sasa Mhe. Spika, tunalalamika ajira, ukifungua mlango kila kitu kiingie nchini bila ya kuangalia kudhibiti biashara zinazotengenezwa na wananchi wako hatuwezi tukaileta juu.

Mhe. Spika, kama tutaweza kudhibiti kitu hiki tungeliweza hata wale wajasiriamali kufanya *order* za mahoteli zingekuwa kubwa wangeliweza kufunga mikataba na wataingia katika mabenki wakapata mikopo wakaweza kutengeneza sabuni yenye kiwango na wakaweza kutoa kiwango kikubwa cha ajira. Sasa tatizo letu tumeachia huru kila kitu hatukujua kwamba tumeruhusu utalii na sisi katika utalii kutahitajika nini na nini na sisi tuweze kujiandaa.

Mhe. Spika, wenzetu China wameanzisha maeneo huru na moja katika kitu walichotwambia kwamba uchumi wao umebadilika baada ya kufungua milango ya biashara na kuweka maeneo huru wakaweka miundombinu. Sasa kitu walichokifanya nini, kwanza walisomesha vijana wao. Mhe. Spika, tunashauri ijengwe Bandari ya Mpigaduri, maeneo huru ya kiuchumi yawekwe miundombinu, je wakija hao wawekezaji wa viwanda tumeandaa vijana wetu kuajiriwa. Mhe. Spika, Zanzibar *population* kwa mujibu wa takwimu tupo 1,300,000 na kidogo karibu 1,400,000.

Mhe. Spika, wenzetu Tanzania Bara nimesoma takwimu za mwaka uliopita wanafunzi ambao wamemaliza karibu laki saba, tena wamemaliza vyuo, nusu ya Wazanzibari wote.

Sasa leo hivi viwanda vikubwa vikija vikiwekeza tumesema hapa sijui viwanda vya samaki, sijui viwanda vya nini, wakija wakiekeza kama hatukusomesha vijana ambao watakuja kuchukua hizo kazi tatizo la kulalamikia ajira litakuwa hakuna, umasikini wa kipato bado utaendelea kuwepo na umasikini wa kipato ukiendelea kuwepo tutaendelea tena kurudi kukamua mifuko yetu au mashati yetu. Mimi nadhani sasa hivi umefika wakati lazima tutengeneze wataalamu

Mhe. Spika, Mhe. Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania mimi nampenda sana Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, aliposikia kwamba Bara wameanza kupata gesi ametoa nafasi karibu elfu mbili kwa ajili ya kusomesha vijana katika fani ya ufundi, katika kufanya kazi katika mazingira ya viwanda vya gesi au viwanda vya mbolea, sisi tumejiandaa na nini? Sasa mimi nadhani na sisi tuende huko, Waziri wa Elimu nafikiri hayupo hapa ajiandae katika hilo. Sasa Mhe. Spika, kwa sababu unapozungumza hizi kodi tunazozirekebisha tutafute na maeneo mengine ambayo tutaweza kuongeza kodi kupata vianzio vyengine na kuweza kuondoa tatizo la wananchi.

Mhe. Spika, sasa nije katika suala la eneo jengine la kuongeza mapato. Mhe. Spika, tulipokuwa China kule tulisoma masuala ya sheria hizi za hatimiliki, kuna suala la *trade mark law*. Mhe. Spika, mpaka leo sijui kama kuna sheria ambayo ya kudhibiti karafuu, yaani ile sheria ya kudhibiti mauzaji ya zao la karafuu. Wenzetu Mhe. Spika, hii karafuu yetu tuliyokunayo basi wangekuwa wameitungia sheria ambayo mtu yeyote akiweza kuuza nje basi tunayo haki ya kumshitaki. Karafuu yetu sisi inauzwa na Kenya. Sasa hapa wanatengeneza ajira lakini chengine Mhe. Spika, moja kinachoinua mapato katika nchi ni kulinda ubunifu na ndio maana wenzetu hizi sheria *copyright law*, *trade mark law* wamejitahidi sana na kuna vijana wengi ambao wanafanya kila mwaka sherehe ya kuwazawadia wabunifu. Sasa Mhe. Spika, haya ni maeneo ambayo yanaweza kutusaidia vile vile kuongeza uchumi.

Mhe. Spika, jengine tumefanya marekebisho ya kodi ya petroli. Mhe. Spika, na Mhe. Waziri ametoa ufafanuzi mzuri, alieleza kwamba amejaribu kuangalia kwenye *litres* atakayetumia *litres* nyingi za mafuta ndiye atakayelipa kodi hiyo mimi hili sina tatizo nalo.

Mhe. Spika, mimi nataka nimpe mfano mdogo, katika eneo ambalo barabara inatumika sana ni barabara Amani-Mtoni, na kama tulingelikuwa Mhe. Waziri angetupa ruhusa tukaweka geti pale Mtoni na hapa Amani *round about* kwamba ile *road toll* tukusanye wenyewe. Mhe. Spika, barabara ile ndani ya mwaka mmoja tungeijenga lakini leo barabara Amani-Mtoni inajengwa kwa muda wa miaka mitano aibu, barabara ya kilomita 5 miaka mitano hiyo haishi. Tumepita kwenye daraja China, daraja kilomita 42 juu ya bahari tumetoka mji mwengine tumekwenda mji mwengine limejengwa kwa muda wa miaka mitano tu tena juu ya bahari na chini zinapita meli. Leo barabara ya kilomita 5, sasa hivi mambo haya tunazungumza Baraza liko *live* watu wakisema kwamba Waheshimiwa wanasema barabara kilomita 5 Zanzibar imejengwa kwa miaka mitano watashangaa, hatuna mipango ambayo madhubuti. Wenzetu Mhe. Spika, kitu ambacho wamefanikiwa, Wachina wametuambia kwamba wanapotunga sheria kwanza wanaiamini na wanaitekeleza na mtu anayekabidhiwa dhamana anatakiwa atekeleze kama vile alivyo, tatizo letu sisi hatupangi mipango kwa muda maalumu.

Mhe. Spika, mimi nadhani Mhe. Waziri, najua suala hili linamuudhi anajitahidi ni suala la ujenzi wa uwanja wa ndege. Sasa hivi hebu malizeni uwanja wa ndege kwa sababu ili tuende na mipango na tunaomba hii mipango inayokuja hapa tukiambiwa tunataka kujenga barabara kwa muda wa miaka fulani basi muda fulani umalize, hakumaliza Waziri aje hapa tumning'inize na tai yake, tumuulize ulikwama wapi, wenzetu ndio wanavyofanya ndio maana wakawa wanakwenda.

Mhe. Spika, naomba sana suala la hii kodi ya mafuta, tunaomba sana basi itumike kama ametumia mafuta mengi ndio anakamuliwa zaidi basi na ile barabara inayotumika sana basi imaliziwe.

Mhe. Spika, niangalie katika mpango ule wa maendeleo bajeti kuu ya Serikali pana ziro pale. Nikampigia simu Mkurugenzi UUB ananiambia aah! imo katika mfuko wa barabara na mwaka jana tuliambiwa imo katika mfuko wa barabara. Sasa leo miradi kama ile Mhe. Spika, ndio inaturudisha nyuma kwa sababu leo barabara ile ile gharama ambayo ilitengwa kumalizia ina gharama kubwa itaongezeka karibu mara mbili au mara tatu. Sasa hapa watendaji wetu kama tunashindwa kupanga mipango tukaingiza pesa kwa wakati na wanafanyakazi nusu wanaondoka wanakwenda kwengine wanarudi tena pale haitambulikani wanafanya nini.

Mhe. Spika, mimi naomba sana katika hii kodi ya mafuta basi mimi nadhani kama alivyosema Mhe. Waziri, labda akija kunijibu ataniambia basi tutakuruhuru muweke lango la *road toll*. Kwa sababu Japan kule ziko barabara kuna geti pale ukipita unalipa na tunaambiwa barabara kama kuna kampuni zinajenga halafu wanakusanya ile *road toll* yao. Sasa Mhe. Spika, hili pia nilikuwa najaribu kulizungumza kwa ajili ya kusaidia zaidi katika kumaliza ile barabara.

Mhe. Spika, nataka nizungumze suala moja ambalo rafiki yangu Mhe. Mshimba amelizungumza. Suala la uingizaji wa mafuta nchini kwa kutafuta kampuni moja kubwa. Mhe. Spika, mimi hili nakubaliana na wazo linalokuja la Serikali na nina sababu zangu za msingi. Mhe. Waziri kajitahidi sana kututolea ufafanuzi, leo tukimtafuta *giant*, kuna makampuni humu duniani wana pesa zao wanatafuta pahala pa kwenda kuwekeza, sisi tunalalamika wanakamuliwa wananchi wadogo wadogo wanakamuliwa wananchi wadogo wadogo, leo wanataka kuja watu ili tuwakamue wao tunasema hatutaki tunataka tuendelee na mtu kuleta mafuta kwenye mkoba.

Mhe. Spika, tumeshuhudia hapa Mhe. Jaku siku zote alikuwa anazungumza sasa hivi sijui yuko wapi hayupo, alikuwa anazungumza siku zote gari yake inazima njiani kwa sababu ya mafuta mabovu, lakini leo uki-*sign contract* na *giant* mkubwa akileta *bulk* za mafuta katika nchi yetu Mhe. Spika, hiyo ni neema, kwanza hiyo moja peke yake ni kuitangaza nchi kwamba watu wanajua kuwa nchi fulani ina-*supply* mafuta waleteni waje waweke matenki ili kuweza kuweka huo uwekezaji.

Mhe. Spika, nataka nizungumzie suala la mwisho kabisa suala la hii sheria tuliyompa uwezo Kamishna wa kuweza kuzuia aidha meli au ndege au kumpa amri mtu au taasisi yoyote kuweza kufanya kazi ya kuzuia au kushikilia

kulazimisha mtu ili kuweza kulipa kodi. Hili ni jambo zuri kwa sababu kweli tumesikia katika baadhi ya vyombo vya habari mbali mbali kuna baadhi ya makampuni wanadaiwa fedha nyingi lakini wanafanya ujanja. Lakini sasa kuna maeneo yetu ambayo ya Serikali ambayo wanayotumia lakini Kamishna anashindwa kuwadhibiti. Kwa hivyo mimi nafikiri sheria hii itaweza kumsaidia Kamishna kuweza kumpa nguvu ya kuweza kukusanya kodi.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa ni suala la hizi nyumba ambazo ninaweza nikasema *guest bubu* au hoteli bubu au nyumba za wageni ambazo wananchi wetu wanakuwa wanawaweka wageni. Mhe. Spika, tulipokuwa katika kamati zetu za Baraza na hili pia tuliliandikia ripoti, nafikiri na ripoti na wewe vile vile uliipata. Mhe. Spika, kuna wageni ambao ni watalii wanaishi katika nyumba za watu binafsi, hakuna sheria yoyote inayowalinda watu wale usalama wao pia unakuwa sio mzuri. Sasa na hii kwa sababu wale wananchi au wale waliokodishwa wanakuwa hawalipi kodi Serikalini. Kwa hivyo Mhe. Spika, hata Serikali hawajui kwamba kuna mgeni fulani kaingia wapi na anaishi. Sasa kwa sheria hii naamini sasa hivi wataweza kutusaidia sana kwa wale ambao waliokodisha watalii au waliokodisha wageni nyumba zao binafsi bila ya kutozwa kodi hii, kwa kweli wanahatarisha usalama wa nchi yetu lakini vile vile hii itaweza kusaidia kuongeza kodi ya Serikali kama litafanikiwa.

Mhe. Spika, baada ya haya machache nataka nikushukuru na nataka nimshukuru zaidi Mhe. Waziri pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura tunaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru ili niweze kutoa mchango wangu kwenye mswada huu ambao Mhe. Waziri ametuletea asubuhi hii kwa ajili ya kumsaidia ili aweze kufikia ufanisi kwa hayo malengo aliyodhamiria kama ni Waziri aliyepewa dhamana ya kutafuta uchumi. Mhe. Spika, kimsingi sina maneno mengi sana na nakubaliana na mswada huu lakini naomba nizungumze machache mno kama tahadhari Mhe. Waziri aweze kuangalia.

Mhe. Spika, ukiangalia mswada huu madhumuni mbali mbali yameelezwa kwenye mswada huu na yote lengo lake ni kuongeza mapato ya Serikali. Lakini ningeomba nimwambie Mhe. Waziri kwamba hata kama Serikali itarekebisha kila siku, maana kila siku ya Mungu sisi tuna kazi ya kurekebisha sheria, kama hakuna umakini wa usimamizi wa sheria hizo tutaendelea kupunguza mapato kwa kasi mno. Kwa hivyo pamoja na ujasiri wa Serikali wa kutunga sheria kwa nia safi kabisa nadhani Serikali iwe na ujasiri tena wa kusimamia sheria hizi ili sheria hizi ziende na uhalisia wenye madhumuni ya Serikali.

Mhe. Spika, duniani kote ili ufikie katika maendeleo yaliyokusudiwa na Serikali wakati mwengine unakuwa si udhaifu wa Serikali kwa Mwanasheria au mipango ya Serikali, mipango ipo lakini udhaifu wa usimamizi na urasimu ndio unasababisha upungufu wa mapato ya Serikali siku hadi siku.

Mhe. Spika, Waziri Mkuu wa Mauritius alimuagiza waziri wake wa fedha kwamba akamilishe mipango fulani ndani ya wiki mbili, mipango hiyo ilikamilika ndani ya wiki mbili hatimae ikachangia pato kubwa la taifa. Sisi hapa Zanzibar mipango inashughulikiwa kwa miaka arubaini, sheria ipo nzuri lakini mipango inakuwa na urasimu. Mimi nilifanya utafiti mmoja nataka nimwambie Mhe. Waziri kwamba juzi kwenye ukurasa wa 11 sehemu ya madhumuni na sababu kifungu cha 5 naomba ninukuu:-
"Kwa kuongeza kijifungu cha (5) ambacho kinatoa adhabu kwa taasisi yoyote itakayokataa kutekeleza wajibu wake katika kusimamia kodi ya Serikali kwa kuitoza asilimia 10 ya kiwango cha kodi inayodaiwa".

Mhe. Spika, hapo imezungumzwa kwamba kama kuna udhaifu katika taasisi za Serikali ambayo itakataa au ita-*delay* kutoa kodi ya Serikali basi taasisi hiyo asilimia 10 ya kodi inayodaiwa.

Mhe. Spika, mimi nakubaliana nalo hili suala lakini vile vile aweke mkakati kwa mujibu na kanuni kwa maafisa wa *ZRB* watakao-*delay* kukusanya kodi kwa wakati muafaka hili ndio ambalo litakuwa linapunguza kodi za Serikali.

Mhe. Spika, nimefanya utafiti mdogo na naomba nimsaidie Mhe. Waziri, kuna kampuni fulani hivi naomba nisiitaje lakini imekusudia kuweka *depot* ya mafuta na imedhamiria kwamba itaweka matangi manne, mafuta ya ndege, petroli, dizeli na mafuta ya taa na kila *tank* litakuwa na lita milioni moja na nusu kwa hesabu ya haraka haraka ni mita milioni sita, na ukiangalia mapato ya *ZRB* na *TRA* kila anapotozwa si chini ya shilingi mia tano. Maana yake kwa lita hizo milioni sita *ZRB* au *TRA* ingeingiza shilingi bilioni tatu ndani ya *depot* moja hiyo, leo hii ni miezi zaidi ya kumi hakuna majibu. Sasa nchi za wenzetu hazifanyi hivyo, inazikataza kuingia ndani ya bilioni mbili au mbili na nusu ndani ya miezi kumi kwa sababu mambo ya urasimu.

Mhe. Spika, nadhani Mhe. Waziri kwa sababu sheria hii ilimpa msingi na uwezo wa dhamana ya kusimamia wale wanaoshindwa kufanya hivyo lazima awaondoshe na aite wengine wanaoweza kufanya kazi. Vyenginevyo Waziri kila atakafanya mabadiliko ya sheria lakini usimamizi kama ni udhaifu basi mapato yanaweza kushuka na kama alivyosema jana kwamba Wazanzibari wanazaliana na Serikali inaongeza mitaji hii ya fedha na haitozuiliwa watu wasizae kwa sababu ya udhaifu wa watu wengine. Jana kidogo Mhe. Waziri aliteleza kwamba anawashajiisha watu wasizae, kuzaa sisi ni asili yetu

tutazaa, awadhibiti watu wake wa Serikali wafanye kazi na waondoshe ile *business as usual*, tuzae kwa kasi na kazi zifanywe kwa kasi vile vile.

Mhe. Spika, nadhani Mhe. Waziri nikuombe sana na mimi nakuamini sana kwamba tunga kanuni ambazo zitawabana watendaji wako wasi-*delay* katika kufanya kazi hizo, ikiwa mradi umekubalika basi uwende haraka, wasimamizi wapate pesa na ziingie katika mfuko wa serikali.

Mhe. Spika, wenzangu walizungumza masuala ya Fumba, ni kweli Fumba imekosa wawekezaji kwa sababu hakuna *master plan. Master plan ZIPA* wanatuambia kama wangepata shilingi milioni mia sita basi wangekamilisha *master plan* ya Fumba, Serikali ndani ya miaka 20 imeshindwa kutoa milioni mia sita za kuwapa *ZIPA* kukamilisha *master plan*. Niwaomba Wawakilishi wenzangu bajeti hii Wizara ya Fedha ikifika tuzitafute milioni mia sita popote ilipo tuwape *ZIPA* ili tatizo hili lao liondoke ili mwakani tuje tuzungumzie lugha mpya ya wawekezaji.

Mhe. Spika, niende kwenye mswada moja kwa moja, nina vifungu vyangu vimebakia nimuombe Mhe. Waziri, kwenye kifungu cha 29 ambacho alifanya marekebisho katika hotuba yake ninaomba nimnukuu kwenye kifungu 27(1) kwenye kifungu cha (f) kifungu cha Sheria ya Bandari Mhe. Spika,

(a) "ili kuondosha ruhusa kwa watu wanaoingiza magari nchini kuyatoa bandarini bila ya usajili gari hizo na

(b) kifungu 29 kuongeza maeneo kabla ya kukamilisha taratibu za Forodha ili kufanya watu wote wanaoingiza magari nchini kusajili na kuchukua nambari za usajili bandarini kabla ya kutozwa gari hizo".

Mhe. Spika, lengo hili la Mhe. Waziri ni zuri lakini pia akimbuke kwamba Wazanzibari wengi wetu wanaingiza magari bandarini si kwa kutumia hapa nchini wanaingiza kwa ajili ya biashara. Sasa unapoweka kifungu hiki kwamba mtu lazima asajili bandarini, maana yake unamuongezea gharama ya gari, maana yake hizi gari ni *transit* tu zinaingia bandarini halafu zinakwenda sehemu nyengine. Sasa ukiweka kifungu hiki maana unawaruhusu watu waongeze gharama za magari. Ni wachache mno magari yanayoingia wanayouza magari hapa nchini. Sisi sote humu ndani wengi wetu magari tunakwenda kununua wenyewe Dubai, wanaoingiza magari hapa ni magari ambayo yanakwenda Tanzania Bara na Mikoa mengine kwa ajili ya biashara. Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri pamoja na nia hii nzuri ya Serikali naamini kwamba lengo ni kwenye mapato lakini kwa hawa wanaoingiza magari wafanyabiashara nadhani sheria hii haitowasaidia na bora kifutwe

tuachiwe wale ambao wanaoingiza magari binafsi kwa matumizi na wanajulikana.

Mhe. Spika, mimi kama Hija ninaonekana mtu wa kawaida ninaingiza gari moja ya matumizi, gari hii inaweza kusajiliwa pale bandarini, lakini anayeingiza biashara basi naomba alizingatia hili ili tuwape mwanya wenzetu wafanyabiashara kwa ajili ya kupata kipato, na kwa msingi huo kama tutafanya utaratibu huu nafikiri mapato ya Serikali yatapungua kwa sababu watu watakwepa kuingiza hapa magari yatapitishwa Tanzania Bara na hatimae tutapunguza mapato kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo ningelichangia ni kuhusu ukurasa wa 12 na 13 wa mswada huu kwenye "madhumuni na sababu". Mhe. Spika, Mhe. Waziri amesema kifungu cha 6(2) kifungu kinasema kwamba mamlaka kwa Waziri kubadilisha kiwango cha kutoza kodi cha asilimia 3 kwa baadhi ya biashara ikiwa hakitokuwa maslahi ya umma katika kufanya hivyo na tatu kinasema kwamba kutoa mamlaka kwa Waziri kufuta au kubadilisha viwango vya hati mbalimbali zinazoelezwa katika sheria ili kuhakikisha viwango hivyo vinakwenda sambamba na mabadiliko ya hali halisi ya uchumi.

Mhe. Spika, kifungu hichi bado sijakielewa kwamba Serikali inakusudia kuongeza kodi hapa au inakusudia kupunguza gharama. Kama inakusudia kuongeza kodi maana yake tunakusudia kumuongezea gharama Mzanzibari wa kawaida. Sasa Mhe. Waziri naomba hapo unifafanulie kwamba hilo linakusudiwa kuongeza gharama za kodi, lakikni ufahamu kwamba ukiongeza gharama za kodi hapa maana yake unamuongezea Mzanzibari gharama ya maisha.

Mhe. Spika, nimalizie tu kusema kwamba mswada huo una malengo mazuri kwa niaba ya Serikali lakini tatizo letu ambalo tutajikwaa ni usimamizi wa sheria zetu. Nimuombe Mhe. Waziri na nimuombe tena usiwe kama Mawaziri wengine, kanuni huchukua miaka mitatu, Baraza limempa uhuru kutunga kanuni na tumempa mafunzo ya kutunga kanuni lakini anakaa miaka mitatu basi mimi nikuombe kwa umakini wako basi angalau miezi sita hizi kanuni zimalizike na hichi ndicho kipimo cha Waziri bora, Waziri makini ni yule ambaye anaonesha kwa vitendo. Kwa hivyo tukupe jukumu hilo kwa niaba ya Baraza nachukua nafasi hiyo kwamba angalau miezi sita hii tukijaaliwa ukamilishe kanuni ili kesho kutwa ukija hapa utuambie kanuni zipo. Kuna watu wanatunga kanuni zinachukua miaka mitatu, kisingizio aah! Mwanasheria Mkuu hajapitia, Mwanasheria Mkuu anapitia na anawakabidhi. Kwa hivyo Mhe. Waziri nikuombe mimi kwa busara zako tuma kanuni haraka sana ili sheria hizi ziende sambamba na usisahau kuweka kipengele kwamba

watu ambao watakao-*delay* wao walipe gharama ya mapato yaliyopotea kwa asilimia angalau 2 ya mapato yale.

Mhe. Spika, naomba kuunga mkono mswada huu.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, na mimi sina budi kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia mswada ambao ni uti wa mgogo wa taifa letu. Pia nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake ambao wameutengeneza mswada huu kwa dhamira na malengo mazuri tu ya kuisaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kukuza mapato yake na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Lakini Mhe. Spika, niseme tu kwamba tunapitisha miswada mbali mbali ambayo ni miswada ya kusaidia katika sehemu mbali mbali na mimi niungane na wenzangu kwamba kitu muhimu ni usimamizi. Kwa kweli kama hatukusimamia basi inakuwa kazi yetu ni ya bure lakini ni imani yangu kwa mswada huu ambao unaleta matumaini makubwa na mambo yetu ya kila siku ili kufanikisha dhamira na makusudio ambayo tumeyaweka.

Mhe. Spika, mimi niende kwenye suala la utalii, makusanyo ya suala la utalii. Mhe. Spika, kwa kweli bado iko haja kwa Mhe. Waziri kuangalia mapato ambayo yanatokana na shughuli za utalii, kuna mambo mengi yanajitokeza ambayo bado nadhani Serikali haijapata hasa hali halisi ya shughuli hizi za utalii katika mahoteli. Niungane na mheshimiwa ambaye alizungumza suala la mambo ya utalii kwa hizi nyumba za watu binafsi. Mhe. Spika, ukizunguka kuanzia mjini huku hasa katika ukanda wenye utalii ambapo utaona watu wengi wamejenga nyumba ndogo ili kukodisha watu kwa namna moja au nyengine ni kuipunguzia mapato Serikali kwa kweli. Sasa ninamuomba Mhe. Waziri katika suala hili nalo litupiwe jicho la huruma.

Mhe. Spika, niende moja kwa moja kwa sababu wenzangu wameshachangia mambo mengi lakini na mimi nina wajibu, niende katika shughuli za uwanja wa ndege. Tegemeo kubwa ni kwamba uwanja wa ndege ni kioo cha nchi kwa wenzetu wanaotoka nje ya nchi ile ambayo wanataka kufikia. Lakini niuangalie uwanja wa ndege wa Unguja na mimi niseme kama walivyosema wenzangu tu kwamba kwa kweli Mhe. Waziri, hebu tufanyieni yale mambo ambayo yataitangaza Zanzibar.

Ninakuomba sana Mhe. Waziri, pale *Airport* Unguja pawe na sura nzuri kwa sababu ukiangalia sasa hivi sura yake sio nzuri na tunakiita kiwanja cha Kimataifa. Maana mimi nitasema kimataifa kwa sababu ndege nyingi sasa hivi zinatua pale. Sasa ni vyema katika mikakati yoyote ile ambayo inafanywa na Serikali pale patatuletea tija kubwa saba, lakini mandhari ya mazingira ya

ndani mule kwenye jengo naomba mufanye tena utafiti makusanyo ya mule yanapenya sana. Kwa hivyo nilisema na mimi hili nilitilie mkazo ili tuende sambamba na mambo yetu ya mswada huu.

Mhe. Spika, sijaishia hapo pamoja na kwamba juzi nilichangia ingawa Mhe. Waziri alinijibu masuala si mabaya yale aliyonijibu, lakini bado sijaridhika na uwanja wa ndege wa Pemba na sasa hivi ukiangalia Pemba bado ni *virgin* haujaingiliwa sana katika mambo ya utalii. Ni vizuri tukaweza kupanga mipango yetu kama alivyosema msemaji mwenzangu Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti kwamba sasa hivi tuangalie na tupige jicho letu mule mwahala ambapo mutasindikiza na kutaka kufanya utalii kwa upande wa Pemba, basi tupigie jicho ili tuanze kupeleka miundo mbinu. Wanapokuja wenzetu wawe wameona kwamba hapa hata nikaweka mitaji yangu basi tunaweza tukafanyia haraka. Nakuomba sana Mhe. Waziri suala la utalii Pemba tusije tukalifanya kama hapa Unguja siku za mwanzo. Unguja walikuja watu hapa kuwekeza wakatukaanga hapa kwa mafuta yetu. Sasa naomba sana Pemba kwa sababu hakujaanza mchafuko mkubwa naomba tupange mipango yetu vizuri ili iwe ni *parallel.*

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, niseme tu kwamba ni imani yangu kwa mswada huu ambao umeleta matumaini kwa serikali pamoja na kwa wananchi, lakini nisisitize tena usimamizi. Mhe. Spika, usimamizi ni kitu muhimu. Baada ya kuzungumza hayo naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia mswada huu muhimu sana. Mhe. Spika, kwanza nataka nimpongeze Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa mswada huu ingawa ni mswada wa kila mwaka.

Mhe. Spika, mswada huu ni wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi kuhusiana na Ukusanyaji wa Udhibiti wa Mapato ya Serikali na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, serikali yoyote duniani inaendeshwa kwa mapato yanayotokana na kodi, ruzuku lakini sijasikia kwamba kuna serikali inaendeshwa kwa kufanya biashara yenyewe. Kwa hivyo, umuhimu wa mswada huu unakuja pale tunapozungumzia hapa suala la kodi, kuna kodi mapato, huna matumizi, kwa hivyo serikali hiyo itaanguka. Sasa mimi nampongeza rafiki yangu Waziri wa Fedha kwa kuleta mswada huu.

Mhe. Spika, kazi ya Waziri wa Fedha ni kubwa mno na yeye asipojitahidi pamoja na watendaji wake akakusanya mapato basi hakuna wizara yoyote

itakayoweza kufanya kazi zake hizi zinazojulikana. Lakini Mhe. Spika, kuna kukusanya, kuna kugawa ulichokipata, kuna kupitilia ulichokipata na kuna kudhibiti hicho ambacho umekikusanya, ukakigawa, ukakitumia. Sasa ni vizuri tuelewe sote hapa kwamba mambo haya manne na mengine madogo madogo kama hatukuwa makini basi hata utoze kodi, ikija nchi ikisimama itakuwa hatujafanya kazi yoyote. Mhe. Spika, kama kodi itakusanywa vizuri hata iwe ndogo lakini matumizi yake yakawa mazuri basi kila mtu anajua kwamba tumepata kidogo lakini kimetumika vizuri, vyenginevyo utakuwa unapata kikubwa lakini hakuna kinachoonekana kinafanyika. Kwa hivyo, mimi nataka kuchangia *general* katika mswada huu. Mswada huu ni suala la kubadilisha sheria au kufanya marekebisho ya sheria fulani zinazohusiana na kodi.

Mhe. Spika, katika ukusanyaji wa mapato ya kodi kuna mapungufu mengi mno na ni vizuri haya mapungufu yakajulikana ili tukajua kwamba sisi hasa tatizo letu nini, miongoni mwa mapungufu ni taratibu za ukusanyaji kodi au mapato.

Mhe. Spika, katika mawizara yetu, mashirika na mamlaka mapato mengi yanakusanywa kwa kupitia njia za kikawaida *pay to cash*, utamkuta mtu kajitwika mkoba ana shilingi milioni mia moja zinakwenda kuhesabiwa, mtu anakaa pale tangu *accounting machine* ibaridi mpaka inapata moto, mpaka ina *jam*, utahesabu shilingi milioni mia mbili? Marobota mia mbili ya shilingi milioni moja moja unaitia moja moja pale mimi naamini kabisa ingekuwa wakusanyaji wa kodi wakubwa wanakwenda tu benki wana *deposit*, anapewa risiti kutkoa benki anaipeleka kule anataka kuhudumiwa hakuna kazi kubwa. Nimegundua kwamba mashirika mengi, taasisi nyingi za serikali zinapokea mapato *pay to cash*, na hii *pay to cash* ni kichocheo cha wizi.

Mhe. Spika, kuna mashirika yanakusanya *pay to cash* wanaingia kwenye *safe* wiki nzima fedha hizo hazijapelekwa benki. Sasa mtu ana ufunguo wa *safe* tajiri asiuchukue? Nina harusi ya mwanangu Ijumaa basi pesa hizi Jumamosi au Jumatatu nitazirudisha, ndio zimekwenda hizo. Kwa hivyo, mimi ningeshauri nendeni na njia nzuri ya kukusanya mapato yetu yanayotokana na kodi mbali mbali basi ni njia hii ya benki unapewa risiti na risiti utaipeleka kwa watoa huduma. Namuomba sana rafiki yangu hili aliangalie.

Mhe. Spika, matumizi hapa ndio tumekaa kitako, matumizi hayana *priority* lakini tumegundua humu, semina na makongamano na safari ndio *priority* hiyo kwa sababu ukienda Dar es Salaam siku tatu posho la nauli ya ndege lakini nakwenda kwa boti alimradi hali ni hiyo. Tena hata matumizi yana matatizo Mhe. Spika, ukija udhibiti ndio kabisa. Tunae Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ripoti zake tumeziona, yaani kuna mapungufu

mengi. Sasa mimi nashauri kwamba chochote tutakachokusanya iwe ni kikubwa au kidogo, basi mambo haya tuyaangalie vizuri vyenginevyo tutakuwa tunakusanya tu.

Waziri wa Fedha alitwambia katika bajeti ambayo tumeizungumza juzi kwamba miongoni mwa mambo ambayo yamesababisha *inflation* ni bei ya samaki. Samaki wamekuwa ghali hapa huamini kwamba sisi tumezungukwa na bahari lakini sasa wengi wa wavuvi wanatumia boti, boti zina mashine na zinatumia mafuta. Kwa hivyo, ukisema uongeze bei ya mafuta Mhe. Waziri si boti tu, ule ni mnyororo, mwenye boti kaongezewa asilimia moja tu sikwambii asilimia tano au sita yeye ilo pembe lililoongezwa linamtosha, mtu wa kawaida hataki kujua ni asilimia ngapi anataka kujua imeongezwa au haikuongezwa. Sasa hilo pembe lililoongezwa bei ya samaki hapa ambayo inasababisha miongoni mwa vigezo vya *inflation* ni bei ya samaki. Kwa hivyo, tutegemee tena kwamba Waziri wa Fedha mwaka unaokuja atatwambia posho limeongezeka kwa sababu ya hilo.

Lakini mafuta yanamhusu kila mtu, mtu wa Matemwe anataka kuja mjini, mtu wa Mjini anataka kwenda kwao Donge haendi kwa miguu. Kwa hivyo huyu huyu anayeongezewa mafuta nasema hata kama kwa asilimia moja basi kama ulikuwa unakwenda Donge shilingi mia sita yeye anakuwekea 1,200. Kwa hivyo, badala ya kwamba tunaangalia namna ya kupunguza umasikini tunazidisha umasikini. Mimi sikatai kuongezwa bei lakini nasema hakuna nyengine hizo njia zote zimeshindikana za kuongeza kodi hizi hizi isipokuwa haya mafuta?

Jengine ambalo katika udhibiti wa fedha hizi ni gumu sana lakini linawezekana ni *corruption*. Mhe. Spika, kuna *corruption* za aina mbili kubwa. Kuna *corruption* kubwa mradi wa US$ 500 milioni, huyu akichukua asilimia kumi ni *corruption* lakini athari yake ni ndogo kuliko rushwa ya udoho udoho. Hospitali hupewi dawa, hufanyiwi operesheni mpaka utoe shilingi elfu kumi. Sasa hii rushwa ya udoho udoho imezagaa kote na huyu ni adui mkubwa kuliko hii *corruption* ya mtu anayepata shilingi milioni 50 peke yake. Kwa sabahbu huyu atakwenda kujenga nyumba yake, lakini rushwa ya udoho udoho iliyoenea kila pahali na kila sekta inamuathiri yule mtu wa chini kabisa anayetaka kufanyiwa operesheni ambapo asipofanyiwa ama ataaga dunia au itamgharimu zaidi. Sasa inabidi hapo tena wakauze kama shamba, *foundation* au nini basi, lakini kaambiwa hapa kama huna shilingi arobaini elfu hapana kitu kumbe hata pesa ilikuwa haitakiwi pale. Katika masuala haya nasema ni udhibiti na watu wengi wanasema kwamba *corruption* katika sekta zote za serikali na hasa zile zinazotoa huduma ndio zimehamia huko, wanataja afya, elimu.

Mhe. Spika, elimu wanatajwa kati ya Bodi ya Mikopo. Sisi ndio Wawakilishi wanatujia. Mheshimiwa nimekuja, haya unasemaje? Kwa sababu mimi nimeambiwa nitoe shilingi laki mbili ndipo nipewe mkopo. Kwa hivyo nakuomba nikatoe maana nisipokuwa na mkopo huu mimi nitashindwa kusoma *qualification* zangu zinaniruhusu. Sasa mwakilishi wewe utoe shilingi laki mbili kwa wangapi, aliyekwambia nani? Aah! mimi kama unazo nipe tu kama huna basi. Lakini kaambiwa kweli kwa sababu inasema ile ruhusa yake ilivyo sio kama anakuja pale kukutapeli.

Sasa mimi nasema vitu kama hivi Mhe. Spika, vyote nasema ni udhibiti, tunaweza tukachangisha kodi hapa kila mtu akatozwa kodi lakini kama hazina udhibiti hakuna msimamizi, hakuna matumizi mazuri maisha tutakuwa ya kunguru na mwewe.

Mhe. Spika, watu wengi hawafahamu kwamba mfanyabiashara siye anayelipa kodi, mfanyabiashara ni wakala anayelipa kodi ni mtu wa chini kabisa. Mimi nikileta kontena langu kama mfanyabiashara naweka faida yangu kabisa na kodi ninayotozwa na Mhe. Waziri wa Fedha, gharama zangu zote mimi pale ni shilingi 10,000. Sasa anayetoa ile kodi ni mwananchi wa kawaida anayetaka kununua mapembe, anayekwenda kununua dira, anayekwenda kununua chochote ile kodi yake naichukua mimi na mimi nakwenda kuikabidhi kwa Waziri wa Fedha. Kwa hivyo, ni vizuri elimu hii itolewe watu wengi hawafahamu kwamba anayelipa kodi si mfanyabiashara mkubwa anayelipa kodi ni mtu wa kawaida, mtumiaji wa mwisho kabisa na ndio maana kwa sababu wananchi wengi hawaelewi kwamba yeye ndiye anayelipa kodi, anaambiwa pale unataka nini, Hii *flat fee?*, ndio, hii ni shilingi laki saba, lakini kama unataka risiti na kama hutaki risiti toa shilingi laki tano. Kwa hivyo anatoa shilingi laki tano hapewe risiti na yule mfanyabiashara aliyemuuzia kwa shilingi laki tano hakuna *record* kwamba kauza kwa shilingi laki tano. Sasa huyu huyu anayeambiwa ndio mlipaji kodi na mfanyabiashara ndiye wakala wa kodi huyu anaumia mara mbili, serikali haipati mapato ya kumhudumia yeye kwa hospitali au kwa jambo jengine lolote lakini mfanyabiashara katulia hana hasara anayopata, yeye kapata faida yake.

Sasa ni vizuri Wizara ya Fedha, *ZRB* kuwe na kipindi cha kila wiki, "hapo kwa hapo kwa sababu kamba hukata jiwe". Mwanzo watu wataona kipindi gani hiki, lakini kikisisitizwa basi watu wataelewa na naamini kabisa wengi sana watakubali, ni vizuri kwamba nimlipe hizo shilingi laki sita lakini kodi ipatikane ili kodi hiyo na mimi inisaidie, vyenginevyo Mhe. Spika inawezekana kabisa, Mhe. Jaku ananitizama sana, ninazo dakika tano.

Mhe. Spika, mwaka jana tulipewa kazi mimi na Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwenda *airport* kuangalia ni utaratibu

gani unaotumika katika kukusanya mapato yanayotokana na *visa*, hee! Hukuwepo Mhe. Spika, lakini malaika wako walikuwepo, kila unavyowaambia watu wa *immigration* basi wana sababu lukuki. Waziri anawaambia utaratibu tutakaouweka hapa ni kwamba ulipaji sasa si *cash*, tena anakuja pale ana-*process* analipa benki *PBZ* pale pale, halafu tena huko *bill* inaendelea. Wakasema hiyo ngumu sana watalii hapa kama tulikuwa tukitumia dakika 15 kumhudumia itachukua masaa mawili. Kwa hivyo, watakuja hapa toka asubuhi wataondoka saa tisa, watu wamechoka yaani yeye anayehudumia wale watalii wakishafika pale kwa kupinga tu kwamba lazima apate pesa *cash*.

Nilipokuwa Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano kuna mtu *airport* aliniambia mheshimiwa hebu siku moja njoo pale *airport*, nije nifanye nini? Akanambia uje pale siku ya Jumatano maan yake ndio ndege kubwa kutoka Ulaya zinaingia pale, halafu mpaka ndege zote zishamalizika uwaite watu wote wa *immigration* uweke mkoba pale, uwe na askari ananambia halafu kila mmoja apekuliwe mifukoni na kila alichonacho atie mle kwenye kapu. Nikamwambia kazi kubwa hiyo, ananambia hutakosa na US$ 5,000 au 6,000. Nikamwambia hizo ndio wanazozileta wao wakitoka majumbani mwao? Akasema wapi, na ndio maana hawa pale *immigration airport* hupelekwi ovyo ovyo *is a syndicate*, ni mtandao, huyo anayekupeleka na yeye jioni anasubiri mapato yake. Akaniambia ndio maana mfanyakazi hapa wa *immigration airport* miezi mitatu ana gari, nyumba na kila kitu. Mimi nasema si suala la choyo au kumtilia mtu fitna, lakini anasema mheshimiwa haya mapato yangekuwa yanaingia serikalini kusingekuwa na haja kubwa sana kuongeza gharama hizi za mafuta zaidi.

Mhe. Spika, umenipa dakika tano lakini mimi nataka nimshauri sana Waziri wa Fedha aangalie vyanzo vipi vya mapato vinavyovuja, aache muhali hana muhali lakini atie kalafati, awe na *airtimes system*, kama alikuwa anapoteza asilimia 60, ifike angalau awe anapoteza asilimia 20, hizi asilimia 40 tuzipate ili ili mwakani *Inshaallah* kodi inayotokana na mafuta ama isiwepo kabisa kwa kuongezwa au hata kama ikiongezwa basi iwe imeongezwa kwa sababu tu ya kuongezwa kwamba tunakwenda na wakati, lakini vyenginevyo Mhe. Spika, itakuwa ngumu sana.

Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima nashukuru sana lakini na mimi naunga mkono kwa asilimia mia moja mswada huu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa fursa kuchangia mswada huu ulioko mbele yetu Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha baadhi ya Sheria ya Fedha za Kodi Zinazohusiana na

Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Sheria na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kwanza na mimi niungane na wenzangu kusema kuwa ukusanyaji wa kodi serikali inapenda kuwe na ukusanyaji wa kodi hizo katika nchi na mambo mengine ambayo ni ya kisheria yanayopatikana katika nchi.

Lakini Mhe. Spika, mswada huu umeletwa kwa ajili ya kurekebisha sheria mbali mbali ambazo ni za ukusanyaji wa kodi. Sasa kama walivyoanza kusema wenzangu na mimi napenda niazie hivyo, kuwa nchi yetu ina ukusanyaji wa kodi sehemu nyingi mno lakini bado tunamuomba Mhe. Waziri asimamie udhibiti wa mapato hayo yanayopatikana. Kwa sababu kama walivyozungumza walionitangulia kuwa bado mapato yanavuja, hizo kodi zenyewe zinazokusanywa zinavuja. Kwa hivyo, lazima Mhe. Waziri ajipange vizuri sana kudhibiti mapato hayo.

Mhe. Spika, suala jengine ni kuhusu maeneo ya vitega uchumi. Mhe. Hamza Hassan Juma amezungumza kwamba maeneo yale bado hatujafanya kama ni maeneo ya vitega uchumi hasa na wawekezaji wakashawishika na kuvutiwa kuwekeza, ambapo uwekezaji ule ungetusaidia ukusanyaji wa mapato na hata hizi kodi ndogo ndogo basi wananchi wetu tungewapunguzia kama ukusanyaji wa mapato ungekuwa mzuri. Ingawa ni mzuri lakini kama wazidishe zaidi.

Mhe. Spikta tumetangaza maeneo ya vitega uchumi lakini maeneo yale tumeyatangaza tu bado hatujataka yawe maeneo ya vitega uchumi. Kwa sababu mfano ulio hai mwekezaji wetu wa ndani Ndugu Bakhressa amechukua eneo kule Fumba na akathubutu kujenga barabara yeye mwenyewe. Yeye ni mtu wa ndani, ni mwananchi haoni tabu kwa sababu anafanya vile ili kusaidia nchi yake. Lakini mwekezaji mgeni ukimchukua ukienda naye kule kumuonesha yale mapori hayana barabara, hayana umeme, hayana maji hawezi kukubali kuwekeza. Suala hili kila siku tunalisema kuwa ili yale maeneo yaonekane kwamba ni maeneo kweli ya uwekezaji na sisi wenyewe tumeshakuwa tayari basi yawekewe miundombinu, kunatakiwa kuwe na umeme, maji, barabara na mambo mengine. Sasa mwekezaji akija akipaona anaona pashakuwa tayari anavutiwa na anashawishika kuwekeza.

Suala jengine Mhe. Spika, amesema Mhe. Waziri kwamba tunakusudia kuweka mfanyabiashara mmoja tu muagiziaji wa mafuta kuleta katika nchi yetu. Mhe. Hamza kasema kwamba hili suala nizidi kulibariki kwa sababu sisi tunapiga kelele lakini leo tukipata watu wenye pesa zao wakaja kuwekeza, wakawekeza kama kituo cha mafuta cha kuuza kwa Afrika Mashariki nzima au na nje ya Afrika Mashariki ni jambo la busara na ni zuri. Lakini tatizo letu

sisi Mhe. Spika, tunasema katika vitabu tu utekelezaji wake unakuwa mzito. Kila siku tunapiga kelele kwamba utekelezaji tunazungumza sana kwenye vitabu lakini utekelezaji wake unakuwa mzito.

Siku za nyuma Mhe. Spika, nakumbuka kulikuwa na mwekezaji wa humu ndani ya nchi yetu, alitaka kuweka chelezo kama kile ambacho watu hukimbilia Mombasa kwenda kupandisha meli kubwa. Yeye alitaka kuwekeza kule sehemu za Makakani kwa Mhe. Mlinde Mbarouk Juma, wale jamaa walitutumka wakaja na nguvu nyingi lakini baadae ghafla walisitisha kufanya ile kazi. Walipositisha ile kazi bahati nzuri mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, tukaenda kule tukakagua vizuri tukaona, tukarudi tukaja tukamwita Katibu Mkuu wa Fedha, tukawaita watu wa *ZIPA* tukauliza tatizo nini, mbona mnamzuia huyu mtu na wakati huyu ataleta mapato katika nchi yetu? Yeye alitwambia hapa pakimalizika panaweza pakaajiri vijana zaidi ya 2,000, lakini ghafla nilisikia kuwa pamezuiliwa sijui anachafua mazingira. Sasa labda Mhe. Waziri aje atueleze yeye kwa sababu analijua suala hili kiundani zaidi, tatizo hasa lilikuwa nini mpaka mwekezaji yule akawekewa vikwazo na lile suala mpaka sasa halikuendelea?

Kwa sababu ni moja ambalo lingeongeza mapato na lingeleta ajira kwa wananchi wetu, wale wananchi waliouza maeneo yao kule waliuza kwa sababu ya kutegemea kuwa suala lile likiwa vijana wao watapata ajira, ile azma yao pia ilififia. Sasa Mhe. Waziri tuna azimia kuweka kitu ambacho kitaingiza mapato katika nchi yetu tusimameni imara nafasi ile ile tuwekeze ili mapato yawe makubwa zaidi katika nchi yetu. Lakini tukizuia tukiwa tunabanabana tu, basi azma yetu itakuwa haifikii malengo, siku zote mimi huwa natoa mifano, kila siku nasema kuchukua mzigo kama umemsaidia mtu ukauchukua ukifika njiani ukauweka kabla ya kumfikishia nyumbani kwake ni sawa sawa na kuwa hukumsaidia, kwa ule mzigo kuuchukua halafu usimfikishie unakokusudiwa hata kama pamebakia kama pale alipo Mhe. Spika, lakini ndio hukuufikisha, ni sawa sawa na kuwa hukuuchukua, kwa sababu lengo ni kufika pale alipo Mhe. Spika lakini hukufika.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba azma ikiwa nzuri basi tuufikishe vizuri ili kodi zikusanywe na mapato yapatikane. Tunazo azma nzuri kweli kweli na tukiweka vitega uchumi vingi au taasisi nyingi za biashara basi hata hizi kodi ndogo ndogo zinazowabana wananchi tutawapunguzia. Kwa hivyo, naomba azma yetu Mhe. Spika, iwe nzuri kama inavyokusudiwa kuwekwa na tuiendeleze ili tufikie malengo.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nizungumze azma ya mswada wetu huu. Nimetizama kwenye madhumuni nimeona kwamba lengo na madhumuni ni kurekebisha marekebisho ya sheria na kutaka watu au taasisi mbali mbali

za serikali kuwajibika na kushiriki katika usimamizi wa kodi na walio chini ya usimamizi wa taasisi zao kuziendesha au uendeshaji au kimamlaka.

Mhe. Spika, tumezungumza lengo na madhumuni ni lile lile la kukusanya kodi na kudhibiti, lakini bado nataka niulize, tunataka kukusanya kodi kutokana na hivi vyanzo vyetu vya ukusanyaji wa kodi? Kwa sababu nimeangalia katika marekebisho haya ya kukusanya kodi za bandari nikaona kwamba kuna marekebisho ya kifungu cha 10. Sasa marekebisho haya ya kifungu hicho nimeona huku katika kifungu ambacho kitakuwepo sasa hivi badala ya kile kilichokuwepo kinasema kwamba, "uwezo wa kuzuia au kuondoa kifungu cha 10 (1) iwapo anayewajibika kulipa ada anakataa au kudharau kulipa ada hiyo Afisa yeyote wa Polisi, wakala wa ukusanyaj,i Kamishna au Afisa wa Umma anaweza kumtoa ndani ya meli au ndani ndege kwa sababu hajalipa hii ada. Sasa mimi pia nilikuwa nataka Mhe. Waziri anifafanulie kidogo ili nielewe zaidi, kwa sababu mimi nimeona ninavyoelewa mimi sasa anifafanulie zaidi ili nipate kuelewa ziadi.

Mhe.Spika, ninavyoelewa mimi kama ada kwa watu wa kawaida wote, mfano kwenye ndege kama mtu anasafiri malipo haya ninavyojua mimi yanaingizwa katika tiketi yake akiwa anasafiri kwenye bandari au akiwa kwenye ndege anakatwa kwenye tiketi yake, bila ya yeye mwenyewe kuambiwa lete ada hii au lete ada ile. Sasa humu naona kama atatolewa kwenye ndege au atatatolewa kwenye meli kama hajalipa hii ada.

Sasa mimi nilikuwa nataka ufafanuzi je, hii ada itakuwa haitozwi tena kwenye tiketi atakuwa mtu analipa hivi hivi mkononi au kutakuwa na malipo gani. Kwa hiyo, naomba ufafanuzi ili atufafanulie zaidi nielewe kwa sababu hapa kidogo sikufahamu. Kama ataambiwa sasa hivi lete maeneo yako ya ada au kutakuwa na utaratibu gani. Ninavyoelewa mimi analipa kwenye tiketi yake ya ndege au meli. Sasa kama kutakuwa na utaratibu mwengine basi naomba kidogo akija anifafanulie hili ili nifahamu zaidi.

Suala jengine Mhe. Spika, nilitaka ufafanuzi kwa Mhe. Waziri tunarekebisha Sheria hiyo Kodi kwa Stempu ili ziingize mapato. Lakini naomba ufufanuzi anisaidie Mhe. Waziri kwa sababu sasa hivi tuko katika utandawazi ninavyoelewa mimi stempu sasa hivi matumizi yake yamekuwa ni madogo mno kutokana na utandawazi. Kwa sababu mambo yote yanatumia *computer*, *E-mail*, *Internet* na zile stempu. Ninavyojua mimi zilikuwa zinatumika kwenye barua, taasisi lakini kwa sababu ya utandawazi mambo haya yamepungua sana.

Sasa labda tu Mhe. Waziri atueleze kama je, katika kurekebisha sheria hii na ili hayo mapato yetu tunakusudia kuwa hizi stempu hasa sasa hivi matumizi

yake makubwa ni yepi, nataka anifafanulie kidogo ili na mimi nipate nielewe, labda mimi kwa fikra zangu naona kama kidogo hizi stempu matumizi yake yamekwisha kupungua.

Mhe. Spika, baada ya mchango wangu huu mdogo namuomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi akija kufanya majumuisho ili nipate uelewa zaidi. Mimi naunga mkono lakini nasisitiza kama tunapotunga sheria zetu, tunapanga ukusanyaji wa kodi lazima tuwafikirie na wananchi wa chini. Tunapoongeza mafuta kama wanavyosema wenzengu basi na mambo yote katika nchi yanaongezeka na ni sawa sawa kama walipa kodi ni hawa wenyewe, yule tajiri mkubwa yeye hakusanyi kodi, yule analipa lakini analipa kwa ajili ya kuwatoza hawa wananchi kama ni mtu anakwenda kuagizia mchele akitozwa kodi ya mchele yeye pia halipi hiyo, mwananchi akenda kununua kilo ya mchele analipa.

Mhe. Spika, kwa hiyo tunapopanga lazima tunataka fedha lakini na hawa wananchi wa chini tuwafikirie kwa sababu ngo'mbe ukimkamua mno basi lazima anatoka damu. Ahsante sana Mhe. Spika. naunga mkono hoja.

Mhe. Spika: Ahsante sana Subeit Khamis Faki ni zamu yake Mhe. Jaku Hashim Ayoub, tumia dakika 8 kama ulivyoomba. Wakati Mhe. Fatma Mbarouk Said anajitayarisha.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nikushukuru wewe kwa kunipa fursa hii mchana huu kuchangia hotuba hii iliokuwa mbele yetu hapa. Lakini kabla ya hapa Mhe. Spika, nataka nirudie maneno uliyoyazungumza tarehe 19 Oktoba 2012 ilikuwa siku hiyo Ijumaa.

Lakini kabla ya kuhoji nataka niseme maneno yafuatayo. Waheshimiwa Wajumbe nataka niwasihi sana kwamba chombo hichi ndicho kinachotoa uongozi wa nchi, Baraza la Wawakilishi hiki ni chombo cha wananchi na wananchi tunawawakilisha sisi kufanya shughuli zao kwa ajili ya mamlaka na hasa mamlaka ni yao wananchi. Sisi uheshimiwa wetu tunaitwa umetokana na wananchi kwa kukubali Katiba hii na ndio tukaitwa Waheshimiwa Wajumbe, tumeitwa Waheshimiwa Wajumbe kwa ajili hiyo wananchi wameamua kutuchagua nendeni huko mkatuzungumzie masuala yetu.

Mhe. Spika, itakapofika pahala kama hatutimizi wajibu wetu narudia yale maneno ambayo tunasema humu Barazani kwamba tutakwenda kuulizwa Waheshimiwa Wajumbe maneno yale kila mtu ajihusie mwenyewe kwamba iko siku tutakwenda kuulizwa namna gani tumetimiza wajibu wetu katika kuendeleza maisha ya wananchi. Haya maneno si yangu mimi Mhe. Jaku Hashim Ayoub ni maneno umeyazungumza wewe Mhe. Spika.

Mhe. Spika, bila ya kupoteza muda nianze na ukurasa wa 3 kifungu namba 3 kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii kutakuwa na kodi itakayojulikana kama Kodi ya Hoteli. Lengo la Serikali ni zuri kuna miradi kama nikahawa inatembeza wageni, sheria hii ipo haja ya kuangaliwa upya kwa makini kwa sababu biashara ya mikahawa hutozwa kodi ambayo itaathiri wananchi wetu.

Mhe. Spika, leo hii tutatangaza watalii, huyo mtembeza watalii anatakiwa alipe kodi, nini anachokipata baada ya Serikali kukaa na kuwafikiria wenye mikahawa kuwaendesha huo ni wajibu wa Serikali, si wajibu wa mtu kwenda kulipa kodi. Kwa hivyo, Serikali kifungu hiki Mhe. Waziri kiangaliwe upya, mpango wa kutangaza watalii huku tunawabana waendesha watalii.

Mhe. Spika nikitoka hapo nije kwenye ukurasa wa tano. Hili nilisema toka wakati wa kuchangia kwamba kuna usambazaji wa bidhaa za huduma, Serikali itamuumiza mwananchi kwa sababu kodi yote inayohusu huduma ya mwananchi ndiye atakayeamua suala hili liangaliwe upya.

Mhe. Spika, baada ya hapo nije kwenye kifungu ambacho ni kizito kwa muda huu namba 9.2. Mamlaka aliyopewa Kamishna makubwa hasa kwa kutumia bidhaa yoyote ya mafuta katika nchi inayofuata msingi wa utawala bora ni vizuri mamlaka za kisheria zikapewa nafasi kufanya kazi yake baada ya Kamishna kugeuka yeye ni mkamataji, yeye mtunga sheria, yeye hakimu huu si utawala bora Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, hichi kifungu Mhe. Waziri akiangalie uzuri ikiwa huko nyuma kifungu namba 9.2 bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha namba 1, Kamishna atakuwa na uwezo wa kuzuia kutaifisha bidhaa yote ambayo itakuwa na sababu ya kuamini kuwa haijalipiwa kodi au imeingizwa kinyume na taratibu wakati wa kuingia au kuangalia haya mamlaka makubwa yamepewa Kamishna wa *ZRB* tena mazito. Kama *power* hii anapewa Kamishna, Mahakama itafanya kazi gani Mhe. Spika, shahidi yupo Khamis Mussa, Katibu Mkuu yupo juu hapo. Kuna kampuni hapa hapa mafuta yalikuwa yanatafutwa, kuna kampuni inakopesha mafuta ilikuwa kuna meli imekodiwa ikachukue Tanzania Bara, ukimwita Katibu wako Mkuu atakwambia kuna kampuni imekopesha mafuta imetiwa meli yake kuisaidia Serikali baada ya muda akaja kulipwa.

Kwa hivyo, sheria tusiangalie upande mmoja tu tuangalie kote kote tuangalia hasara zake na nini faida zake. Hili litakuwa zito mtu analeta mafuta kwa nini Mhe. Spika, anafanya hivyo kuna taratibu za uongozi uko asilipishwe faini leo yale mafuta wataifishwe chombo kinataka kutaifishwa imekuwa vitisho, mtu kaleta mafuta kafata *process* wanaotafuta kodi wache walipe kodi.

Kuhusu suala la kupandishwa mafuta Mhe. Hamad Masoud Hamad kalizungumza hapa ukipandisha mafuta maisha yatakuwa makali, wewe jana ulipiga kelele watu wasizae tutazaa watoto wawili kama tuko China hapa. Mhe. Spika, basi moja linapakia abiria 28 kila lita shilingi 35 hebu tuangalie daladala inafanyakazi kwa siku ngapi na wakiweka gharama za njia hapa itakuwa shilingi laki nne kwa mwezi tumefanya nini tunawafanyia haki wananchi, leo mvuvi anaekwenda kuvua baharini hakupa samaki mafuta yake yamekwenda bure. Hii sifikiri mimi hapa ni pazito Mhe. Waziri paangaliwe upya na barabara vile vile tuangalie vyote vyote.

Mhe. Spika, Mhe. Hija Hassan Hija kazungumza suala zito sana tena na hili Mhe. Waziri wala usipoteze muda ufute tu hicho kipengele kuhusu magari bandarini. Mhe. Spika, wewe shahidi ushuru umepanda Bara magari yamekuwa yanaoza. Ndio biashara kubwa tu tulizobaki nazi hizo Mhe. Waziri, hatuna kitengo chengine hili liondoshwe bila ya kupoteza muda Mhe. Waziri nakushauri na ushauri wa bure tu huo.

Mhe. Spika, mimi hapa nna barua kutoka .....

Mhe. Spika: Mhe. Jaku Hassan Ayoub zimebakia dakika mbili.

Mhe. Jaku Hassan Ayoub: (anaendeela) hii leseni hapa ukitaka kukata *ZRB* milioni tano kwa mwaka keshakamilisha masharti yote anaambiwa kuwa mwisho sehemu ya matangi. Sasa mtu anataka kwenda kukodi kukopa pesa benki hajamfahamisha taratibu atazipa vipi, hili anabahatisha tu kupata au kutokupata.

Mhe. Spika, leo chombo cha Meli kina lita ngapi mafuta Dar-esa Salaam rahisi kuliko Unguja kwa tafauti ya shilingi 200 maisha haya yatakuwaje hatuwezi kukuza uchumi namna hiyo Mhe. Waziri iwe sababu gani leo Zanzibar maafuta yawe ghali kwa shilingi 200 kuliko Tanzania Bara halafu *ZRB* wapige kelele.

Mhe. Waziri mimi nakunasihi sana utakapokuja hapa uteeleze chombo cha meli kinatumia lita ngapi kule baharini hakuna mzambarau, hakuna mpera, hakuna mdinu angalau ukaifunga ile meli, leo mtakuja kuuwa wananchi.
Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, sitounga mkono hoja mpaka nitakapopata maelezo ya kina kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Jaku Hassan Ayoub. Zimebaki dakika 15 nadhani Mhe. Fatma Mbarouk Said uzitumie dakika hizo.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia machache tu na sitakuwa na mengi kwa sababu mimi sijenda China.

Mhe. Spika, vile vile nichukuwe fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri kwa kuleta Mswada huu mbele yetu. Mswada huu wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi kuhusiana na Ukusanyaji na udhibiti wa Mapato ya Serikali na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa niaba ya wananchi wangu wa Amani kabla sijenda na tatizo hili nililoliona niseme naunga mkono mswada huu mia kwa mia.

Lakini licha ya marekebisho ambayo yamelofanywa na Kamati ya Wenyekitiviti kuhusu mswada huu niseme basi na mimi nimeona tatizo ambalo liko kwenye huu Mswada wa Sheria ya Kodi ya Bandari ambayo iko kwenye sehemu ya pili inasema marekebisho ya kifungu cha 10 ambacho kwa kufuata marekebisho ya kifungu kidogo cha 3 na kuunda baada yake kifungu kidogo kipya cha 3 kama ifuatavyo:

Bila ya kujali sheria yoyote itakayokwenda kinyume na sheria hii Kamishna kwa amri ya maandishi anaweza kumteua mtu yoyote anaeongoza na anaesimamia na anaedhibiti au ana mamlaka ya kisheria. Ningependa Mhe. Spika, likawa hapa mwenye mamlaka ya kisheria kushughulikia bidhaa au abiria wa meli yeyote, mwalimu wangu wa kiswahili alinambia lugha hii yeyote unaweza kutumia kwa mtu haiwezekani kwamba meli yeyote na hata huku nyuma nilivyoiona imekuja hivyo hivyo meli yeyote au ndege kwenye bandari yeyote ni mtu peke yake ndio anaeweza kutumia kwamba mtu yeyote si bandari yeyote.

Mhe. Spika, kama nilivyokwisha kusema kwamba huu mswada ni mzuri na kwa sababu unataka kuboreshwa ili mapato yaweze kuleta ufanisi zaidi. Nasema ni hayo tu kutokana na nilivyoisoma.

Kwa niaba ya wananchi wangu na kwa niaba ya mwalimu wangu wa kiswahili alienisomesha. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante sana na ujumbe kuhusu safari ya China pia umefika.

Mhe. Assa Othaman Hamad: Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii.

Naomba niseme machache tu juu ya mswada huu mzuri na baada ya kumpongeza Mhe. Waziri mwenye dhamana.

Mhe. Spika, binafsi mswada niseme kwamba nataka niiunge mkono kwa asilimia 80. Nabakiza 20 mpaka Mhe. Waziri atakaponiridhisha kwenye suala la Kodi ya mafuta. Mhe. Spika, bado sijaona sababu kwa sasa najua adhma nzima ya Mhe. Waziri ya kufanya hivi, lakini kwa sasa hivi itakuwa tunawapa watu adhabu ya bure ambayo kosa sio lao.

Mhe. Spika, kodi hii ya mafuta Mhe. Waziri alipofafanunua atakaetumia barabara zaidi kwenda na kurudi atalipa zaidi. Atakaetumia kidogo atalipa kidogo, lakini aliwahisabu wenye magari je, wanaopanda magari kwa sababu wenye magari kwa tatizo lile lile linalotusibu la usimamizi mbovu watajipangia bei wanazotaka wao wenyewe na wenye vyombo vya baharini watapanga bei wanazotaka wenyewe atakaeathirika ni mwananchi mnyonge asiekuwa na chochote *"Dhul-Jalal wal iqram"* . Hili ndio mimi ninalotaka maelezo ya kina uniridhishe nikumalizie ishirini zilizobakia, sijakubaliana nalo bado.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wameshazungumza mazuri ya kutosha lakini nisema kuwa sitawatendea haki Wazanzibari kama sitosimama. Mhe. Spika, tatizo lipo na labda baada ya mswada huu kupita na Mhe. Waziri atasaini kuwa sheria sasa ile lugha iliyozoeleka tubadilike. Maana sasa kama ni zumari waitikiaji wasikilikaji linasikika hili zumari peke yake. Sasa tubadilike lakini najiuliza anaesema ni nani wanaoambiwa ni wapi kwa sababu imekuwa kuwa pande mbili moja anasema na mwengine anaitikia lakini hili halipo, *Airport* kila siku tunasema pana wizi. Labda kwa kuwa anasema Assaa Othaman Hamad, Bandarini kuna wizi na rushwa kimnya asubuhi ukienda pale pale.

Mhe. Spika, mengine hatutakiwi tuzungumze kwa jazba kwenye chombo hichi lakini yanakera na yanaudhi. Kwa sababu adui wao asikie, Serikali itusikie sisi tuliochukuwa dhamana ya watu waliotuchagua waliotuleta hapa. Mhe. Spika pale bandarini kwa sababu tu mwenye chombo kuna bahasha wahusika wa ile bandari wenye dhamana ya watu wanakubali wanakubali na wenye chombo abebe watu zaidi ya kiwango kwasababu yeye kapewa bahasha, haya yapo na hivi sasa wiki hii ya Alhamis yametokea tena haya. Watu wamepakiwa mpaka wamebakizwa wale wenye dhamana ya bandari ile wapo pale pale. Sijui anakomolewa Mhe. Rashid Seif Suleiman au anakomolewa Mhe. Rais, sijui anakomolewa Mhe. Omar Yussuf Mzee kifanyikacho hapa hatuelewani kwa nini. Sasa nasema kama mswada huu utapitishwa na utapita na Mhe. Rais kuusaini hebu tunataka Mhe. Waziri wa Fedha tuone mabadiliko ya makusanyo *Airport.* Kwanza hii mambo ya

kupeleka watu kwa sababu ni mtoto wa nani shemegi nani ukisema unaambiwa ni kelele za vyura ni kweli kelele za vyura na mvua hainyeshi. Lakini tutaendelea na kelele hizi hizi za vyura na maneno haya yanajibiwa pale pale *Airport* ati sie ni kelele za vyura, wao watabaki na msimamo wao kuibia watu kuinyanganya Serikali hii na sie tuendelee kupiga kelele tunaambiwa ati kelele za vyura.

Mhe. Spika, na Bandarini ni wizi mkubwa upo rushwa haijatikisika pale lakini kuna taasisi kadhaa. Juzi Mhe. Mohamedraza Hassanali katwambia *Zanzibar Beach* pale kampuni inadaiwa mamilioni sasa hatua zichukuliwe anatokea mwengine anasema hapana. Mimi nilitegemea kwamba Mhe. Mohamedraza Hassanali ataambiwa ushahidi ule auwasilishe Serikalini kuona hatua zinazochukuliwa za huyo mtu. Lakini wapi!

Mhe. Spika, Mhe. Hamad Masoud Hamad alitaja hili suala la ulipaji wa pesa mfukoni na kwenye mkoba wa ukili. Mhe. Spika, hapa ni ku- *bargain* baina anaekusanya na anaetoa. Leo nakuamini sana mimi na Wazanzibari wanakuamini kama anavyokuamini Mhe. Rais hebu tuone haya tena yawe basi. Mhe. Spika, fedha ipo na kwa haja tuliokuwa nayo inaweza kukidhi kwa kiasi fulani. Lakini bado gonjwa ni usimamizi, ufuatiliaji, uaminifu na uadilifu na *serious* ile inayozungumzwa ya Serikali bado katika suala hili mianya ni mingi mno wananchi wanateseka kwa dhiki uliyokubwa ndani ya nchi hii.

Mhe. Spika, muda uliobaki nauheshimu lakini nataka nimwambie Mhe. Waziri tuna imani kubwa na Ofisi yako uko karibu na Mhe. Rais katika suala hili la makusanyo la walipa kodi ni Wazanzibari kwa heshima kubwa na taadhima tunakuomba Ofisi yako waone Wazanzibari sasa kwamba kumebadilika na Serikali yao. Mhe. Spika, nakushukuru. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Waheshimiwa nakushukuruni kwa michango hiyo na kutupa mashirikianao makubwa kuendesha shughuli zetu. Jioni tutakuwa na wachangiaji wawili kwa mujibu wa orodha yangu ambae ni Mhe. Salma Moh'd Ali pamoja na Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Nimeombwa niwatangazie Waheshimiwa Wajumbe kwamba kesho siku ya Ijumaa ile hitima ya mamaake mwenzetu Mhe. Amina Idd itakuwa wakati wa laasiri pale pale nyumbani kwake Mhe. Amina Idd, kwa upande wa wanawake.

Kwa upande wa wanaume hitima hiyo itasomwa katika msikiti ule ule tuliomsalia maiti baada ya sala ya ishaa. Kwa hiyo, tunaombwa Waheshimiwa Wajumbe tushiriki kwenye shughuli hiyo wanawake itakuwa wakati wa

laasiri kesho siku ya Ijumaa wakati wanaume itakuwa baada ya sala ya ishaa siku hiyo hiyo ya Ijumaa.

Baada ya hayo basi Waheshimiwa Wajumbe sasa naakhirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni.

(*Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka saa 11:00 jioni)*

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tumebakiwa na wachangiaji wawili, majadiliano yanaendelea. Tukamilishe basi na Mhe. Salma Mohamed Ali na baadae Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mhe. Salma Mohamed Ali: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia mswada muhimu sana katika nchi yetu, yaani mswada wa kutoza kodi. Vile vile naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa kutuletea mswada huu.

Mhe. Spika, kwanza huu mswada hauna ufafanuzi wa maneno muhimu yaliomo katika vifungu mbali mbali, kwa hivyo mimi sitokuwa na mchango mkubwa, isipokuwa kuna mambo madogo madogo ambayo naomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 2 kifungu cha 3(a) kumetajwa kamishna. Swali langu ni kuwa huyu kamishna gani, kwa sababu nchi hii ina makamishna wengi, kwa hivyo ni vyema tungefafanuliwa ni kamishna yupi aliyekusudiwa.

Mhe. Spika, vile vile katika kifungu hiki kumetajwa naomba kunukuu,

Kifungu cha 3(a)

"bidhaa au abiria wa meli yoyote au ndege kwenye bandari yoyote ya Zanzibar"

Mhe. Spika, naomba hapa patiwe ufafanuzi, palipotajwa abiria wa meli pametajwa na bandari, lakini abiria wa ndege hapakutajwa uwanja wa ndege. Je, abiria hawa nao wataondokea bandari hii.

Mhe. Spika, yote hayo ni maeneo ambayo naomba nipatiwe ufafanuzi. Sehemu nyengine ambayo namuomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi ni katika

ukurasa wa 3 kifungu cha 5(1) na cha (2), kuna marekebisho yaliyofuta sheria ya mwaka 1999 na kuweka kifungu hiki cha 5.

Swali langu Mhe. Spika, ufutaji huo na marekebisho yaliyofanywa yanakusudia kuingiza mapato ya jumla ya shilingi ngapi kwa mwaka huu wa fedha. Vile vile unaleta unafuu gani kwa walipa kodi waliokusudiwa au wao baada ya kutoa kodi hizo wanategemea kuimarishiwa kitu gani. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi wa maeneo hayo. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, baada ya kukushukuru na mimi kwa kunipa nafasi hii, naomba nichukuwe fursa hii kwa sababu najua muda wenyewe sio mrefu sana. Kwanza niishukuru kamati ambayo ilinisaidia sana katika kuupitia mswada huu na kuuboresha. Lakini pia ambao wamesaidia humu ndani kutuelimisha katika baadhi ya maeneo ya mswada huu, najua wamesaidia ya kutuelimisha kwa sababu wamepata fursa ya kuuelewa madhumuni ya huu mswada, madhumuni ya marekebisho mbali mbali ambayo yameelezwa, pamoja na kwamba madhumuni na sababu yameelezwa kwa urefu, lakini nikubali kwamba sio rahisi kwa maneno tu yaliyoandikwa, pengine mtu akaweza kuyafahamu kila kitu ambacho kimeelezwa katika huu mswada.

La pili, nadhani wachangiaji wameeleza mambo mengi sana, lakini katika walioeleza na ambayo mengi yatatusaidia katika kujenga ufanisi katika ukuzaji na ukusanyaji wa mapato, lakini wameeleza changamoto ambazo ziko katika ukusanyaji wa mapato. Mimi naomba niwe shuhuda wa yale baadhi ambayo wameyasema.

Mhe. Spika, katika ukusanyaji wa mapato kusema kweli kuna changamoto mbili kubwa. Changamoto ya kwanza ni kwamba kwa maumbile yake ukusanyaji wa mapato ni jambo ambalo linahitaji uaminifu wa hali ya juu.

Lakini la pili, ukusanyaji wa mapato unahitaji pia ujuzi wa hali ya juu. Nasema hayo kwa sababu mengi yamepigiwa kelele hapa na Waheshimiwa Wajumbe wengi katika kuchangia hoja hii. Nasema linahitaji uaminifu wa hali ya juu kwa sababu zenyewe sheria za kodi, zina mianya mingi ambayo anaweza kutumia mtu kukwepa kodi na wakati mwengine ukwepaji huo ukawa halali. Kwa sababu kwenye kodi tunasema kuna mambo mawili. Kuna *tax avoidance* na *tax evasion*. *Tax avoidance* ni kutumia ile mianya iliomo kwenye sheria mtu akaweza kukwepa kodi na ambapo huwezi kisheria kumshika. *Tax evasion* ndiye yule ambaye sasa amefanya kosa.

Kwa hivyo, ukiangalia ndio maana nasema kwamba hili linahitaji uadilifu, kwa sababu yule yule ambaye anakusanya kodi, anaweza akampa mtu mianya iliomo na akaweza kukwepa kodi pengine kihalali. Sasa huu mswada ulioletwa kama mara hii, kuna maeneo mengi ya kiutawala ni kwa sababu ya kuziba hiyo mianya ambayo pengine kisheria mtu angeweza kuitumia kihalali akaweza kukwepa kodi. Ndio maana sheria za kodi kila mwaka na pengine ndani ya mwaka ikarekebishwa mara mbili, ni kwa sababu sheria yenyewe ina sehemu ambazo inaweza kumruhusu mtu akaweza kukwepa kodi.

Mhe. Spika, mimi nashukuru nilibahatika katika moja kati ya yale niliyosema, nilisomea masuala ya kodi. Mwalimu wetu pale Chuo Kikuu London alipokuwa akitusomesha alikuwa anasema, tumewafundisha wizi, kwa hivyo ni lazima muwe waadilifu sana katika kuitumia elimu hii. Ni kweli katika watu ambao hammalizi kusoma pale, mnakuja kupata watu wakutaka kuwaajiri ni katika fani hii ya kodi na makampuni, mkimaliza nyote mnaajiriwa au mnapata watu wa kuwaajiri, kwa sababu watu wanatafuta hawa wataalamu wa kwenda kuwasaidia katika huo wizi kwa kutumia sheria ziliopo.

Kwa hivyo, ni jambo ambalo linahitaji kusema kweli uadilifu wa hali ya juu. Mimi nakumbuka nilibahatika kuwa mwenyekiti wa mwanzo wa bodi ya mapato ilipoanzishwa mwaka 1997, na nilikuwa mwenyekiti kwa miaka 6 mpaka mwaka 2003. Wakati ule tuliandaa maadili ya wafanyakazi. Nakumbuka Mhe. Suleiman Nyanga akaja kuzizindua zile kanuni za maadili ya wafanyakazi, wakati ule akiwa ni waziri anayeshughulikia fedha mwaka 2002. Sina hakika labda Mhe. Waziri tumuombe kama zile zimekufa au zimezimia, basi ni vizuri kuzifufua, kwa sababu kusema kweli zitasaidia. Kama ziliachwa hazikutumika tena ni jambo la lazima katika taasisi yetu ya kodi kuwa na kanuni za maadili na tena zisimamiwe kwa umakini wa hali ya juu.

Mhe. Spika, jengine alizungumza sahibu yangu hapa mwanasheria mkubwa Mhe. Mshimba Mbarouk, kuhusiana na suala la Venta Club na alitaka ufafanuzi wa hili suala likoje. Mhe. Spika, labda hili liwe ni moja katika semo. Kwanza alifanya mambo mawili, lakini sitaki nizungumze sana kwa sababu suala lenyewe liko mahakani, lakini tumeshamaliza na kufikia mwisho ingawa ile hukumu haijatoka, lakini kusikilizwa limeshamaliza kusikilizwa, nadhani kama sio leo basi kesho tunaweza kupata hukumu ya suala hili.

Mhe. Spika, kwanza waliokuwa na ile hoteli ni wengine na waliokuwa wakiendesha ni wengine. Kampuni ya Ventaglio ilikuwa ndio wenye hoteli, lakini waliwapa wenzao waliokuwa wakiendesha, wenye share ndio hao hao, lakini ndio hii ninayosema ujanja wa kufanya mambo kwa kupitia sheria za

makampuni ili kila mmoja katika wao aondokane na hii dhima ya kodi. Mpaka wanaondoka pale kusema kweli madeni waliokuwanayo ni makubwa na hata madeni ya wananchi. Maana yake ukitizama madeni ya wananchi ni karibu milioni 702, wana madeni ya wafanyakazi karibu milioni 199 na wana madeni *ZSSF* nadhani milioni 19 na ukiachia mbali madeni mengine ya akina *ZECO* na wengineo.

Mhe. Spika, naomba nimuhakikishie Mhe. Mshimba pale kwamba serikali imechukua juhudi, baada ya kupokea ile ikaunda kamati Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na ikaja na mapendekezo ofisi yetu ikayafanyia kazi na ikafungua shauri la kuifilisi kampuni ile na sasa hivi tuko katika hatua za mwisho. Kwa bahati mbaya kampuni yenyewe imefilisika hata huko imefilisiwa. Kwa hivyo, kitakachopatikana tunachoweza kuwahakikishia angalau ni wale wananchi waliokuwa na madeni kwamba watapata kisheria tunasema *prorata,* tutatazama kilichopatikana na tutatizama kila mtu apate asilimia ngapi ya kile anachodai, kama ni asilimia 60 au 70 au 80. Ukitizama kisheria hasa basi mtu mwengine angesema labda hawastahiki, lakini tunajua kuwa mengi yamefanyiwa kutokana na wenyewe kutokuwa na maarifa katika masuala hayo.

Kwa hivyo, nimuhakikishie tu kwamba hiyo kazi tumeikamilisha na tuko katika hatua za mwisho na wananchi ambao tayari tume waorodhesha tunao majina yao, lakini na chao wanachodai basi watapata kiasi cha haki ile ambayo kutokana na kile ambacho tutakipata, juhudi hiyo imo na tumo katika kuikamilisha.

Jambo jengine alilozungumza Mhe. Hamza Hassan, kazungumza jambo kubwa na la msingi kweli kweli, ambalo linahusiana na sheria za haki miliki. Aliuliza kuwa je, tuna sheria ya kuilinda karafuu. Nadhani akija Mhe. Mazrui atakuja kuieleza, lakini niieleze kidogo kwa ufupi.

Kwanza nimuhakikishie kwamba katika nchi yetu kweli kama yeye mwenyewe anavyokumbuka kuwa sheria hiyo tunayo na bahati nzuri, tumekuwa na sheria ya namna hii tokea mwaka 1911, lakini matumizi yenyewe ndio ambayo pengine Mhe. Haroun katika suala la uwezeshaji itabidi nalo liingizwe katika mpango wa kuwasaidia watu kutumia kwa ukamilifu sheria hizi, ili ziweze kuwafaidisha.

Mhe. Spika, kusema kweli Mhe. Hamza Hassan kasema jambo la maana sana, kwamba kama sheria zile tutazitumia vizuri basi zitaweza kulinda ubunifu wa wananchi, zitaweza kulinda haki zao mbali mbali ili waweze kuzitumia katika soko hili la ajira ndani ya nchi yetu na hata nje ya nchi yetu, kwa sababu vipo

vitu ambavyo havipatikani isipokuwa Zanzibar, lakini na wengine wanaigiza kwa sababu hatuna sheria ya kuweza kulinda.

Mhe. Spika, kwa mfano suala la karafuu alilolisema, juhudi ya suala hili imefanywa. Kwa sababu ulinzi wa karafuu au mazao ya kilimo kama karafuu, yanafanywa chini ya sheria hii ya *Industrial Property*, chini ya kitu tunaita (GI) yaani *Geographical Indication*. Tunachosema ni kwamba karafuu yetu ya Zanzibar basi ina upekee wa namna fulani ambayo haiwezi kuzalishwa popote duniani.

Kwanza ni kuthibitisha hivyo kwamba ina upekee wa namna fulani na kanuni za kufanya hivyo zipo zimeshaandaliwa chini ya sheria. Wataalamu wa kufanyakazi hiyo kwa kushirikiana na (*WIPO*) yaani *World Intellectual Property Organization*, wameshakuja, mpaka aina za *package* na masharti ya kulifanya hili, basi hiyo kazi iko katika hatua kubwa na kwa msaada wa shirika hili la kimataifa la *World Intellectual Property Organization*. Kwa hivyo, niwaambie kwa ufupi tu, labda Mhe. Mazrui siku atakayokuja, suala hili nadhani atakuja kulieleza kwa urefu.

Mhe. Spika, jengine ni lile ambalo alilizungumza Mhe. Ismail Jussa kuhusiana na uwezo wa waziri katika kubadilisha yale majadweli. Aliuliza kwamba kama waziri atakuwa na mamlaka hayo Baraza litakuwa na mamlaka gani. Mhe. Spika, labda nikumbushe tu, mwaka jana hapa serikali ilikuja na mapendekezo ya kutaka kuweka ada ya bandari kwa zile meli za ndani hapa. Zile ada kusema kweli hazikuwa kwenye sheria, waziri alichokuwa anatafuta ni idhini ya Baraza, alileta mapendekezo yale mbele ya Baraza ingawa angeweza kufanya bila ya kulishirikisha Baraza, lakini kwa sababu hizi ni sera za kibajeti alikuja nayo mapendekezo hayo na mara nyingi ndivyo inavyokuwa, kwamba zinaletwa hapa na lile ambalo linakubaliwa hapa ndilo ambalo waziri anakwenda kulifanyia kazi. Kwa kawaida haya majedweli huwa yanabadilishwa baada ya kupitishwa mpango au hotuba za bajeti kama tulivyofanya hii leo.

Kwa hivyo, moja katika udhibiti mkubwa wa Baraza ni huo, mara nyingi haya yanaletwa baada ya kukubaliwa yale mapendekezo ya serikali ya bajeti halafu ndio waziri anakwenda kufanya marekebisho. Lakini kama kuna haja ya kufanya udhibiti zaidi ya hapo kama alivyopendekeza Mhe. Ismail Jussa, nadhani ni jambo la kuliangalia hapo baadae na nadhani ni wazo hili la kuangalia namna gani hilo linaweza kufanyika.

Jengine ambalo aliuliza Mhe. Ismail Jussa lilikuwa ni suala la kwenye sheria ya kodi ya hoteli, yaani uwezo wa waziri kuweka viwango maalum. Sasa

atauliza kwamba hivi viwango maalum kwa nini viwekwe na vigezo gani ambavyo vinatumika.

Mhe. Spika, viwango maalum hivi ni kwamba kwa kawaida katika soko hili la mahoteli na mikahawa hasa la mahoteli. Ziko hoteli ambazo zinajulikana kwamba hizi ni hoteli nyengine za daraja gani, viwango vyake vinatumika hakuna tatizo, tunakwenda kukusanya kwa mujibu wa vile viwango vilivyowekwa.

Mhe. Spika, kwanza kuna kundi la kwanza la nyumba za kulala wageni za kienyeji. Kwa mfano katika maeneo ya mashamba mengi sasa hivi ya utalii, kuna mtu ana nyumba yake analaza wageni na hii ukitizama sio hoteli, sio nyumba ya kulala wageni, lakini nina hakika kwamba kweli analaza wageni.

Kwa hivyo, njia ya kwanza ni kusema kwamba lazima apate leseni na njia ya pili kwa sababu ukisema asilimia 18 wakati mwengine ni shida, ndio inaitwa viwango maalum. Hata hapa mjini kuna nyumba za kulala wageni nyingi ambazo kusema kweli pengine mtu ana nyumba yake ina vyumba vitano, wengine saba na wengine nane. Sasa huu ni utaratibu ambao umekuwa kwa muda mrefu ukitumika kwa zile kazi zinawekewe vingo maalum.

Mhe. Spika, nakumbuka ziliwahi kuwa dolla 3, kwa sababu kwanza hawatangazi, ukenda wanasema mimi natutoza 5,000. Sasa 5,000 hiyo ukimwambia asilimia 10, ukitizama serikali itakachokifanya ni kitu kidogo, lakini hiyo nina hakika kwamba hatozi Shs. 5,000. Lakini ukenda kumshika ukimwambia akuletee asilimia 10 au asilimia yoyote basi atakuletea Shs. 1500 au Shs. 500, atakuambia hii ndio ninayokusanya. Sasa kwa hivyo sikuviwekea utaratibu wa kuviwekea ada au viwango maalum. Ilikuwa dolla 3 wakati fulani, ikapandishwa ikaja dolla 5 na ikapandishwa nadhani sasa hivi ni kati ya dolla 7 na dolla 8. Sasa kama yeye mwenyewe kama atatoza Shs. 5,000 shauri yake, au atatoza 2,000. Lakini serikalini tunavyojua sisi inakuwa huduma hii mfano wewe tuletee dolla 5 au dolla 7 au dolla 8 kwa kadiri ya kile kiwango ambacho kitakuwa kimewekwa na hii inaondoa usumbufu wa kila mtu kumfanyia *assessment.* Huu ni utaratibu uliokuwepo tokea mwaka 2002 nakumbuka ulikuwa unatumika, sasa hivi hii sheria imeimarishwa kwa kuwekwa bayana katika sheria.

Mhe. Spika, jengine ambalo liliulizwa ni kuhusiana na ule uwezo wa kamishna kutoa tafsiri. Mhe. Spika, kusema kweli labda hii ya Kiswahili ndio tunatumia kutoa tafsiri, lakini ni kawaida katika usimamizi wa sheria za kodi kwa kamishna kutoa kitu tunaita *practice notes*, yaani muongozo wa utekelezaji.

Kwa mfano hata hapa Barazani, tunasema tu labda hili litapelekwa mbele ya Baraza, lakini wakati mwengine halina ufafanuzi, ukilipeleka mbele ya Baraza utalipeleka kwa utaratibu gani. Sasa kwenye sheria za kodi hayo yapo mengine, sheria inaeleza tu kwamba hili litafanyika namna hii. Lakini utaratibu wake wa kulitekeleza unakuwa haupo katika sheria, lakini inajulikana kuwa utaratibu wa kukodi jambo lile unalipeleka namna gani.

Kwa mfano, *fine of return* namna ya kuzijaza na mambo mengine ya namna hiyo. Sasa haya kwa kawaida sheria zetu za kodi zinatoa mamlaka kwa kamishna msimamizi mkuu wa sheria zile kutoa maelekezo ya usimamizi, ndio hizo tunaziita *practice notes*, sio kwamba ni ufafanuzi wa sheria yenyewe, lakini ni kutoa muongozo sheria ile itatekelezwa namna gani. Kama kuna mtu anaona kuwa maelekezo yale hayakuwa sahihi bado anaweza kwenda mahakamani kutaka tafsiri ambayo ni sahihi juu ya utekelezaji wa sheria hii. Lakini hii ni *standard practice*, na sio kwamba ni jambo ambalo limeanzishwa kwa mara ya kwanza chini ya mapendekezo haya, isipokuwa ilikuwa ni kuliweka bayana.

Vile vile Mhe. Ismail Jussa Ladhu alizungumzia kuhusiana na suala la kodi ya ardhi na mimi nikubaliane naye. Kusema kweli tatizo ambalo tulikuwa nalo Mhe. Spika, kwa muda mrefu ni kwamba tumeichukulia kama ardhi ni kitu mbali peke yake, wakati ardhi ni sehemu muhimu sana katika uwekezaji, ardhi ni kitu muhimu sana katika uchumi vile vile. Lakini tulivyokuwa tunaifanya ardhi hatukuiweka kama kwamba imo katika ile milolongo, yaani katika ile cheni ya uwekezaji, katika ile cheni yenyewe ya uchumi. Sasa kwa kujiingiza hapa Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kushauriana katika hili, ni kusaidia kuleta ushirikiano na kuchukua ardhi nayo kuitia kama ni sehemu ya uwekezaji, pia kuipitia kuiweka kama ni sehemu ya uchumi katika nchi. Kwa hivyo, itasaidia hata serikali yenyewe kuweka sera nzuri zaidi. Maana yake waziri wa ardhi yeye kapewa kazi ya kuisimamia ardhi kama ilivyo, lakini ardhi kama uchumi mwenye mamlaka hayo ni waziri anayehusika na uchumi na mipango ya maendeleo. Kwa hivyo, kuwaweka pamoja hawa ni ku-*mis* ardhi katika masuala ya uchumi na uwekezaji kusema kweli. Hayo hasa yalikuwa ndio madhumuni yake.

Mhe. Spika, jengine ambalo Mhe. Waziri hapa ameniomba nizungumzie ni mchango ambao ingawa hakuuleta hapa Mhe. Farida, yeye ametoa indhari katika mchango wake wa maandishi, kwamba kifungu cha 9 katika ile sheria ya marekebisho ya kodi kwamba katika hiki kifungu cha 9, yeye alitoa indhari kwamba kuna wavuvi ambao wanakwenda kuvua, lakini wanachukua mafuta labda kama Kenya, kwa sababu mafuta ni rahisi. Kwa hivyo, anaporudi pengine hakuyatumia yote, sasa hawa watu wanaweza kukamatwa kwamba wameingiza mafuta kinyume cha utaratibu na hii sheria ikawashika.

Mhe. Spika, mimi naomba nimtowe wasi wasi Mhe. Farida Amour kwamba hiyo ndio tunaita *tax avoidance*. Yaani hili ukiliachia mwanya ndio inakuja hiyo *tax avoidance*, kwamba mtu anatumia mwanya huo wa kisheria kukwepa kodi. Kwa sababu mtu anayetumia unajua kwamba kwa kiwango hiki ndio matumizi yake, lakini mtu hawezi kuwa na madumu 20 akasema haya ni mafuta natumia. Kusema kweli hicho kiwango cha kwamba mtu anadumu moja hawezi kushikwa na kuambiwa kaingiza mafuta, labda mafuta ya taa au mafuta ambayo yeye hatumii. Lakini kwa mafuta anayotumia inajulikana hiki cha akiba na hiki sio cha akiba. kwa hili ni muhimu na yeye mwenyewe ndio atajishtaki au yeye mwenyewe ndio atajitoa kwenye hatia kutokana na ule ukweli wake na udhati wake na udhati utauona kwa kile ambacho anacho katika chombo chake. Hawezi kuwa na dumu 20 akasema kwamba mimi hizi natumia, pengine matumizi yake yote pengine ni dumu moja na hata akienda safari mara mbili na kurudi. Kwa sababu haya yanapimika sasa hivi na haya yanafanyika sasa hivi.

Jengine Mhe. Spika, labda lile alilozungumza Mhe. Subeit Khamis Faki, kwanza alichozungumza ni kitu cha kweli, kwamba kwa utaratibu wa sasa hivi ile ada ya kiwanja cha ndege inaingizwa kwenye tiketi. Sasa hii ambayo atakuja kukamatwa chini ya kifungu hicho tunamkusudia nani na wakati mtu atakuwa tayari ile ada imeshalipwa kwenye tiketi.

Waheshimiwa Wajumbe hayo yanatokea kwa namna mbili. Kwanza tujuwe wale wenye ndege wao ni wakala tu wa kukusanya hii kodi, kwa hivyo inawezekana pengine baada ya kukusanya halipi serikalini na anapokuwa halipi serikalini na serikali ina haki ya kumfutia ule uwakala wenyewe. Kwa hivyo abiria akatakiwa alipie mwenyewe *cash* pale uwanja wa ndege. Hili ndilo linalotokea sasa hivi kwa *Precission Air* kwamba baada ya kuvunja hayo masharti ya uwakala, wakawa serikali hawailipi, serikali imefuta uwakala. Kwa hivyo, kila abiria sasa hivi wa Precission analipa, na wengine wakaidi wanasema mimi ninavyojua kwamba hii imo kwenye tiketi, kwa hivyo mimi silipi wapo na wanatokea pale uwanja wa ndege sasa. Mtu anasema mimi ninavyojua hii imeshalipwa, mimi silipi tena. Anaambiwa kama hulipi shauri yako na ndege hupandi.

Kwa hivyo, siku nyengine mtu huyo ama atachagua ndege nyengine ama atachagua kulipa, lakini haya yanatokea kwa sababu uwakala wa mwenye ndege unaweza ukafutwa pale ambapo anavunja masharti ya uwakala, hivyo hili ni muhimu. Wakati mwengine inatokea mtu kapewa tiketi, pengine *complimentary* ambapo kodi analipa yeye aliyepewa ile *complimentary ticket*, maana anakuwa yule mwenye ndege hajakulipia ile tiketi yenyewe. Kwa hivyo, haya yapo mazingira ambayo pamoja na utaratibu uliopo, bado hili linaweza likatokea na ndio maana hii sheria imebidi iweke masharti hayo.

La mwisho aliuliza kwamba aah ushuru wa stempu kwamba sasa hivi mambo yameendelea, barua nyingi zinakuwa barua pepe, sio barua zile za zamani sijui tukiziitaje, lakini sasa hivi wanasema barua pepe, hii stempu tena ni ya peke yake, lakini

sasa hii *stamp* tena inatokea wapi. Lakini naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kupitia kwako Mhe. Spika kwamba bado matumizi ya *stamp* yapo, kwa sababu zinatumika katika mambo mengi.

Kwa mfano, ukitoa *cheque* inalipiwa *stamp*, ukisajili *document* yoyote ya ardhi kuna malipo ya *stamp*, pia kuna mauzo ambayo pengine hayalipiwi *VAT*, pia yanalipiwa ushuru wa *stamp*. Kwa hivyo, sio ile *stamp* ya Posta peke yake ya barua, lakini huu ni Ushuru wa *Stamp*, ambao ni kwa nyaraka na mauzo tofauti ambao sheria imeweza kuelekeza. Kwa maana hiyo, kuwepo kwake ni muhimu sana.

Mwisho kuna suala la Kamishna iliyokusudiwa maana kweli Makamishna wamejaa kwetu na Mhe. Salma Moh'd Ali aliuliza huyu Kamishna ni yupi mbona sheria haikufafanua. Lakini ukitizama hii tunayoifanyia marekebisho ni sheria ya marekebisho, lakini ile sheria tunayoita sheria mama imefafanua nini maana ya Kamishna.

Kwa hivyo, maana ya Kamishna hapa ni Kamishna wa Bodi ya Mapato. Mhe. Spika, ule ufafanuzi umo katika sheria lakini inawezekana haukuwemo kwenye mswada kwa sababu huu ni mswada wa marekebisho tu lakini ile sheria yenyewe mama inao ufafanuzi wa suala hili.

Mhe. Spika, nadhani lile moja la kuhusu kiwango kitakachopatikana limefahamika. Kwa hivyo, Mhe. Spika niseme kwamba michango iliyotolewa hapa kusema kweli ni mizuri na itatusaidia. Vile vile niwaombe na wenzetu nao hasa lile la uaminifu na hili la ulinzi najua kwamba Bodi ya Mapato, Wizara ya Fedha yenyewe imekuwa ikichukua juhudi kubwa kusomesha watu zaidi, kwa ajili ya kuwapatia maarifa zaidi.

Lakini kusema kweli hii ni changamoto kuhusu suala la uaminifu ni jambo ambalo linahitaji juhudi maalum na Waheshimiwa Wajumbe wamelizungumza hapa, nyenzo na mikakati nadhani ipo iliyoandaliwa ni muhimu hivi sasa kuisimamia.

Baada ya kusema hayo, Mhe. Spika niunge mkono hoja na ninakushukuru kwa kunipa fursa hii. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwa kuwa mswada huu ni tofauti kidogo na ile miswada ambayo tumeizoea huu unaitwa papo kwa papo. Kwa hivyo, naomba kwa ruhusa yako nitoe taarifa kwamba niko tayari kujibu hoja za Waheshimiwa Wajumbe. *(Makofi).*

Mhe. Spika, kwanza nataka nitoe shukurani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wajumbe kwa kuuchangia mswada huu wa marekebisho ya sheria mbali mbali, ili kuweza kuipa nafasi Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kuweza kufikia malengo yale ambayo tuliyokusudia ya kuweza kupata fedha ili tuweze kuwatekelezea wananchi wetu yale majukumu ambayo wametutuma.

Mhe. Spika, mswada huu umechangiwa na Waheshimiwa Wajumbe 14, ambapo Mhe. Mjumbe mmoja amechangia kwa maandishi na 13 wamechangia kwa kuzungumza.

Kwa hivyo, kama ilivyo kawaida yetu Mhe. Spika, naomba niwataje kwa majina wale waliochangia na ninajua wengine pia walikuwa na hamu ya kuchangia, lakini mawazo yao yamewakilishwa na hawa waliochangia. Mhe. Farida Amour Mohamed, ambaye amechangia kwa maandishi.

Vile vile waliochangia kwa kuzungumza ni hawa wafuatao:-

1. Mhe. Ussi Jecha Simai kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti.
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.
3. Mhe. Ismail Jussa Ladhu.
4. Mhe. Hamza Hassan Juma.
5. Mhe. Hija Hassan Hija.
6. Mhe. Asha Bakari Makame.
7. Mhe. Hamad Masoud Hamad.
8. Mhe. Subeit Khamis Faki.
9. Mhe. Jaku Hashim Ayoub.
10. Mhe. Fatma Mbarouk Said.
11. Mhe. Asaa Othman Hamad.
12. Mhe. Salma Mohammed Ali.
13. Mhe. Mwanasheria Mkuu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwanza nataka nikiri mawazo michango, maoni pamoja na mapendekezo yote yalikuwa mazuri na sisi tuliopewa dhamana kwa niaba ya wananchi kwa upande wa serikali tumeichukua michango ile yote ili tuweze kuifanyia kazi.

Ni dhahiri Mhe. Spika, lazima nikiri mbele yako sitaweza wala sisi serikali hatutaweza kuifanyia kazi michango ile kwa masaa 24. Lakini kwa sababu mumeichangia basi nataka nikiri kwamba tutaifanyia kazi na hatimaye wananchi wetu wa Zanzibar kupitia michango iliyowasilishwa na Wawakilishi wao, basi waweze kuona kazi zilizofanywa na serikali yao.

Vile vile nataka nikiri Mhe. Spika, baadhi ya michango iliyochangiwa ilikuwa na tija lakini ilielekeza zaidi kwenye bajeti kuliko kwenye mswada na mimi nimeipokea michango hiyo. Kwa mfano, kulikuwa na mchango wa Bandari ya Mpigaduri, Mhe. Spika, nimeeleza hapa kwa lengo la serikali ni kujenga Bandari ya Mpigaduri.

Pia kulikuwa na mchango kuhusu kuendeleza *Airport* ya Zanzibar. Lengo la serikali kuiendeleza *Airport* ya Zanzibar na sio kuacha kama vile ilivyo. Mhe. Spika, kulikuwa na mchango kuhusu kuendeleza maeneo huru ya kiuchumi na lengo letu ni kuendeleza maeneo huru ya kiuchumi.

Kwa kweli haya yote Mhe. Spika kama nilivyosema jana yamo kwenye kalenda na hivi karibuni mtaanza kuona baadhi ya maeneo yanafanya kazi na wala haitakuwa siri. Kwa mfano, bandarini pale mtapita na mtaona *crane* zinaanza kufanya kazi na wala sio siri. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza kwamba ni dhahiri kuwa serikali kukamilisha yale mambo ambayo imeyaanza na hilo ndilo lengo la serikali, yaani pale penye matatizo serikali lazima iingilie kati, ili kurekebisha yale matatizo na pale ambapo kuna kitu kinatafutwa serikali lazima ichukue muda itafute hicho inachokitafuta, kwa ajili ya mradi ule uweze kufanya kazi.

Mhe. Spika, nataka nimshukuru Mhe. Mwanasheria Mkuu amefanyakazi ile ya kisheria, kwa sababu Mwanasheria, wajumbe wake ni kuwasaidia mawaziri katika sheria na mimi nataka nikiri sio mwanasheria. Kwa maana hiyo, Mhe. Mwanasheria Mkuu amefanya kazi ya kunisaidia katika vile vifungu vya kisheria na namshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu. *(Makofi)*

Lakini nina imani kwamba Waheshimiwa Wawakilishi ambao wameuliza maswali yao kupitia kwenye vifungu vya mswada, nadhani majibu aliyoyatoa Mhe. Mwanasheria Mkuu yanakidhi haja na kiu yao, mimi kama nitapita basi nitapita juu juu tu, lakini Mwanasheria Mkuu ameshakamilisha ile haja. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kulikuwa kuna mawazo, maoni pamoja na mapendekezo kwamba badala ya kuongeza kodi, basi serikali ingeandaa mazingira mazuri ya kuwakaribisha wawekezaji kuwekeza katika viwanda, ili kodi zaidi ziweze

kupatikana kwenye viwanda vitakavyoekezwa. Kwa kweli nakubaliana na wazo hilo na serikali imeanza kufanya utaratibu huo na mimi naamini kwamba mazingira mazuri sasa yapo.

Kwanza tunao umeme wa uhakika na nitaendelea kulisema hili kwa sababu tumesahau hivi karibuni tulikuwa tunapata umeme hapa kwa resheni au vivunge na leo hatuna tena mgao wa umeme, isipokuwa tunao umeme wa uhakika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mwekezaji yeyote hataweza kuwekeza kiwanda kama umeme si wa uhakika na leo tunao umeme wa uhakika ni mazingira mazuri, yaani tunaandaa mazingira mazuri kama tunaisoma hotuba yangu kwa ukamilifu. Kwa mfano, tumesema kwamba miradi ya viwanda na kilimo itaekewa utaratibu mzuri wa kupata vivutio zaidi. Kivutio kimoja tutakachokiangalia ni ardhi na yale yatakuwa ni maeneo ambayo tuliyaita humu ni *Strategic Investment*, yaani lazima tuwavutie wawekezaji wa viwanda.

Kwa hivyo, vivutio hivi tunaviangalia kwa undani kabisa ili wawekezaji wa viwanda waje. Mhe. Spika, kuna Waheshimiwa Wajumbe wawili au mmoja wamezungumzia kuhusu ziara ya Mhe. Rais. Kwa kweli mimi nilipata bahati kuwemo katika ziara ya Mhe. Rais kule China nikiwa na mwenzangu Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi pamoja na Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Katika ziara ile Mhe. Rais alizungumza na wawekezaji wa viwanda na wameahidi watakuja mwaka huu Zanzibar kabla hawajamaliza mwaka. Kwa hiyo, vivutio tumeanza kuviweka na kuwakaribisha. Vile vile kama nilivyosema jana jitahidini mnapokwenda nje Waheshimiwa Wawakilishi tafuteni wawekezaji wa viwanda na nyinyi muwe munawaalika kuja kuwekeza katika sekta ya viwanda, kwani tukipata viwanda vingi kodi itatanuka zaidi na wala hatutaweza kubinya binya katika maeneo yetu yale yale.

Mhe. Spika, la pili ambalo limezungumziwa ni suala zima la kusimamia kodi zilipwe wakati ule unapotakiwa kulipwa. Mhe. Mwanasheria Mkuu ameeleza na ameonesha vifungu tulivyoviweka. Mhe. Spika, unapotafunwa na nyoka ukiona ung'ong'o ndipo unapokimbia, tumepata kesi mbili na ni kubwa. Mhe. Mwanasheria Mkuu ameitaja kesi ya *Venta Club* amekimbia na madeni, kesi ya *Precision* ni kesi mbili kubwa sana na zina mifano hai kabisa.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wawakilishi mnapozungumzia kodi ilipwe pale inapotakiwa kulipwa ni sahihi kabisa na mimi nakubaliana na nyinyi, tutawaambia wenzetu wenye dhamana ya kukusanya kodi *ZRB* na *TRA*

kwamba watumie sheria yao, sheria inawapa muda, kuna kodi nyengine zinawapa mpaka siku kumi, nyengine siku saba iwe imeshalipwa vyereje unakwenda nayo miaka na miaka kodi ile inarundikana mpaka inafikia pahala tunaanza kuhangaishana. Kwa hivyo, mimi nakubaliana na nyinyi Waheshimiwa Wawakilishi kwamba tusimamie hili na tutalisimamia kwa udhati wa moyo wetu.

Kuna wengine wameeleza matumizi bora ya ardhi wakasema kwamba Zanzibar ni kisiwa na ni dhahiri kwamba leo mahoteli yote yanayojengwa yanakwenda tambarare tu, yanachukua maeka kwa maeka tutafika pahala tutakuwa hatuna ardhi, kwa nini sasa tusiweke utaratibu wa kuwaambia wajenge kuelekea juu ili ile *value* ya ardhi iendane na *value* ya *investment vis-à-vis* mapato tutakayoyapata kupitia kodi yatakuwa bora.

Ushauri mzuri tumeupokea na mimi nataka nikuahidini kwamba Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati atakaporejea tutakaa pamoja na watendaji wetu tuanze kulitizama suala hili, pamoja na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ambayo inasimamia masuala ya utalii. Tutaanza kulitazama kwa pamoja hili suala ili tuone tunawaelekeza vipi wawekezaji wetu. Tumelipokea ndugu zanguni.

Jengine ambalo limezungumziwa hapa sheria ya nishati na hii sheria ya kodi ya mafuta hazigongani. Mhe. Mwanasheria Mkuu ameeleza kwamba hizi sheria mbili hazigongani, moja inaelekeza utekelezaji wa kulipa kodi na moja inaelekeza utaratibu wa kusimamia *the product* yenyewe, lile suala ambalo tunalizungumzia kwamba mafuta machafu liko kule nalo vile vile, kiwango gani cha mafuta anatakiwa aweke kabla hajaingiza nyengine na kodi za mafuta. Kwa hivyo, nasema hizi sheria mbili hazigongani na kama zitaonekana kuna kifungu kinagongana na kama sheria moja haija *override* sheria nyengine tutazileta hapa Barazani Wawakilishi makini tupo tutafanyia marekebisho.

Suala la magendo ya mafuta tumeagizwa hapa tulitizame kwa ukamilifu na kwa ujumla wake, zaidi imezungumziwa usimamizi wa sheria. Sheria zetu za kodi, sheria yetu ya fedha nataka nikubaliane na nyinyi kwamba marekebisho ambayo tumeyafanya katika mswada huu mengine yanalenga zaidi katika usimamizi. Kwa sababu Mwanasheria Mkuu hapa mimi namsifu sana, ameeleza kitu ambacho ni *practical*, wewe ukitengeneza sheria kuna mwengine anatafuta *loophole* ya ile sheria ili aitumie na unapoona kwamba sheria hii tayari ina mianya ni wajibu wake kuja kufanyiwa marekebisho kuziba ule mwanya na hizi sheria za fedha ndugu zangu unaweza ukazifanyia marekebisho kila mwaka. Kwa sababu na hawa walipa kodi nao wana akili kama sisi watunga sheria, kila ukiziba huku basi imekuwa kama guruguru vile

ukiziba huku anazibua huku. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba hizi sheria ni muhimu tuwe tunazifanyia marekebisho kila kipindi ili kuziba ile mianya.

Lakini nataka nikubaliane na wale wenzangu akiwemo Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba usimamizi wa sheria zetu ndio muhimu zaidi kuliko hata kuwa kila mara tunarekebisha sheria. Tutafanya hivyo, tutakumbushana kila muda na wenzetu tuliowapa kazi ya kukusanya kodi ili wazisimamie sheria hizi kwa karibu zaidi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu pamoja na Waheshimiwa wengine walieleza kwamba tunafanya nini kupitia sheria hizi za fedha na kodi katika suala zima la kuwapatia unafuu wafanyabiashara wadogo wadogo, ili waweze kukua. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka niseme kwamba nimeeleza kwenye hotuba yangu, tunao mpango ambao tumeuandaa, jambo la msingi ni kwamba tutawaambia wenzetu wa *ZRB* ule mpango tuliouandaa usiwe uko kwenye makaratasi zao na ofisi zao, isipokuwa wauweke vizuri na wauchapishe katika magazeti yetu, ili kila mfanyabiashara ndogo ndogo aweze kuusoma. Kwa kweli tunayo imani mpango huo wafanyabiashara wetu wadogo wadogo hawa hatutakuwa tunafukuzana nao katika masuala ya kodi. Kwa hivyo, hilo tunalo na tutajitahidi tuweze kulitangaza, ili na wao waweze kufaidika nalo.

Suala jengine ambalo limesisitizwa zaidi ni kuhusu usimamizi ambalo tayari nimeshalizungumzia. Pia kuna jambo jengine ambalo limezungumzwa na wajumbe wengi, hapa nadhani ningetoa ufafanuzi kidogo.

Mhe. Spika, nimeeleza kwenye hotuba yangu kwamba tena nadhani tokea mwaka jana na ninafikiri Waheshimiwa Wajumbe sote tumeshawahi kuona, mimi waziri ambaye ninasimamia kodi nimeshaona si mara moja wala mbili na ninaamini mwenzangu Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, kwamba kuna gari zinatembea hazina *plate number*.

Hali hii maana yake nini? Maana yake inawezekana ile gari imeibiwa pahala na linasafirishwa au gari ile inatumiwa vibaya na majambazi, inawezekana kwamba ile gari imekwepa kulipa kodi yaani ina maana nyingi tu. Kwa bahati mbaya isije ikasababisha ajali, litakaposababisha ajali hali itakuwa ngumu si kwa dereva wala mwenye gari mlolongo mzima itabidi tuutafute mpaka yule aliyeliruhusu lile gari kuanzia bandarini, mwenye gari ile mpaka yule ambaye analiendesha. *(Makofi)*

Sasa tukasema kwa nini tufike huko ni bora ya kinga kuliko tiba. Mhe. Spika, siku zote Mhe. Waziri wa Afya anatuambia tujikingeni, yaani ni rahisi

kujikinga kuliko kujitibu na gharama zake kubwa, sasa hayo hayako kwenye afya tu isipokuwa yako kwenye maeneo mengi.

Kutokana na hali hiyo, tumesema sasa tutatoa gari inapotoka tu bandarini kabla haijatoka nje mwenye gari ile atasema, kwa sababu tunayo midomo na gari haina midomo isipokuwa ina honi tu, lakini wewe mwenye gari utasema hii ni kwa madhumuni gani. Kwa hiyo, hii ni gari yangu nimeileta kwa ajili ya kuiendesha hapa Zanzibar, basi tutakupa *plate number* ya kuiendesha Zanzibar na unailipia, yaani ukiitoa inatoka na namba yake.

Vile vile ukisema hii gari ni kwa ajili ya biashara basi tutakupa *plate number* ya kibiashara na itakaa na *plate number* yake ya kibiashara na hizi bei zitatofautiana. Sasa mtu anapokwenda kwa mfano umeiweka kwenye *yard* yako ina *plate number* ya kibiashara tuna-*record* na *chassis number* yake itakuwemo katika *bill of lading*.

Kwa hivyo, mtu anapokwenda akaondoa ile na akatembea nayo na tukaikamata, basi *chassis number* itatwambia hii gari tumempa nani na ilikuwa na namba gani. Kwa kweli tunakinga jamani kuliko kuanza kutibu, Zanzibar ni eneo dogo, yaani ni kisiwa kidogo na ile amani tuliyokuwa tuki-*enjoy* kila siku tunataka tuendelee ku-*enjoy* na lengo letu ndio hilo.

Mhe. Spika, ukifika pahala ile gari umeweka kwenye *yard* yako ina namba ya kuuzwa, yaani kwa mfano ina namba ya kibiashara au *transit*. Sasa tukifika pahala mimi Jussa nimekuja kuinunua basi atabadilishiwa namba kwa ajili ya kuingia ndani sasa, atapewa ile namba ya Z ili iweze kuingia, vyenginevyo ndugu zanguni tutakuja kujijutia kama hatujakita mapema. Kwa hivyo, nilikuwa nataka nitoe ufafanuzi huo kwamba lengo ni zuri tuli-*practice* na tuone kama litatuletea utata tulifanyie marekebisho, kwa sababu marekebisho wakati wowote tutayaruhusu, lakini tusilikatae lengo ambalo sisi wenyewe tumeliona ni zuri kwa ajili ya kujilinda sisi wenyewe. *(Makofi).*

Mhe. Spika, kuna hoja ambayo imetolewa hapa na tumetakiwa tuangalie mapato yetu yanayotokana na utalii. Sasa moja miongoni mwa marekebisho tuliyaweka ndani ya sheria hii ni hayo ya mapato ya utalii. Leo kila mtu au kila hoteli inasema inataka kuwa *VAT register*, lakini ukimuuliza unatoza kiasi gani wewe kwa mtu anakwambia mimi nalipa dola 40. Maana yake akikwambia yuko *VAT register* anatozwa dola 40, maana yake nini? Maana yake kodi yako na wewe umtoze kwa mujibu wa dola 40 na wala hatuwezi kwenda huko.

Kutokana na hali hiyo, hoteli zote hizi hivi sasa tunazitizama viwango vyake na kodi zake nataka kuwa *VAT register*, basi lazima isishuke dola 100 kwa

kichwa na huko ndiko tunakotaka kwenda katika marekebisho haya, ili mapato haya yanayotokana na utalii yaweze kuonekana, kwa sababu watalii wengi pamoja na hoteli nyingi lakini kila siku tunapiga kelele mapato yetu kidogo.

Mhe. Spika, nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu kila mtakapokuwa na michango mizuri kama hii, basi msisite kutusaidia na sisi tutarekebisha sheria zetu, ili mapato yetu yaweze kuwa bora zaidi na yaweze kutusaidia katika maendeleo yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hoja nyengine ilikuja kwamba tuangalie *sources* vipi mapato yanavuja. Kwa kweli *sources* tunazijua na tumeanza hivi sasa kuzitia puti au rangi ili zisivuje tumeanza. Vile vile kuhusu hili la Uhamiaji litakwisha kesho kutwa, kwa sababu haya ni maelekezo. Mhe. Spika, wakati Mhe. Hamad Masoud Hamad alipokuwa akichangia alisema kwamba mimi na yeye tulipewa hiyo kazi kwenye kamati na Baraza la Mapinduzi, yaani mimi na yeye tukawa tunakwenda mpaka *airport* na badarini kuangalia na tumeyaona. *(Makofi).*

Sasa tumefanya utafiti mdogo na tumeona nini cha kufanya na tukasema sasa hiki ndicho cha kufanya na wala sio ya bandarini tu mengi yametokana na utalii, tumeshayawekea mkakati na *program* iko tayari imeshaandaliwa na hivi sasa watu wanatafuta muda waende kule kwa wakaweke *software* mambo yaanze na muda mfupi tutamaliza. *(Makofi)*

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo limezungumzwa sana ndugu zangu Waheshimiwa Wajumbe na mimi nataka nilifafanue wakati tulipozungumzia kuhusu habari ya kodi zile za mafuta na njia. Kwa kweli nataka nirudie tena kusema kwamba kuanzia tarehe 1 Julai tukeshakumaliza kupitisha mswada huu wa sheria kuwa sheria, basi kuanzia tarehe 1 Julai hakutakuwa tena na ulipaji wa *road license* ambayo itakufanya wewe upate *sticker* ubandike, utaratibu ule utakuwa tumemaliza. Kwa maana hiyo, utaratibu tuliouweka hivi sasa ile *road license* yako utailipa kupitia kwenye mafuta.

Vile vile wapo wengine hapa wamekuwa na wasi wasi hapa na jana nilitoa hesabu ndogo tu na nilisema kama wale washamba kama mimi kutoka mjini kwenda Pwani Mchangani na kurudi unahitaji lita 10 kwa sababu nimeshajaribu kwa gari yangu mpaka Pwani Mchangani kwenda na kurudi bado zimebakia.

Sasa katika zile lita 10 kitakachoongezeka au utakachokilipia kupitia ile *license* ya njia ni shilingi 350/= na kama gari hiyo ni ya abiria basi kila abiria atachangia shilingi mbili. Lakini hawezi abiria akachangia shilingi mbili

mpaka wewe mwenye gari uangalie *road license* kwa mwaka ulikuwa unalipa kiasi gani na sasa unalipa kiasi gani na wala tusiwe na wasi wasi.

Mhe. Spika, watu wamezungumza labda bei ya *transport* zitapanda na nini, kwa sababu kuna Bodi ya Usafiri wa Nchi Kavu na hii ndiyo yenye mamlaka ya kupanga bei zile za daladala na nini. Kwa hivyo, hawa hawawezi kupandisha tu, bila ya ile kuitizama hiyo *mathematics* na wao wataitazama hiyo *mathematics*, kwa hiyo tusipate shida bure kwamba haya mambo sisi tumeyafanyia kazi na tumeyaona.

Kwa maana hiyo, zaidi ni kwamba eneo hili litatusaidia sisi ku-*control* watu wasitengeneze risiti *fake*, yaani zile risiti za *road license* mnazobandika zile nyengine ni *fake*. Mhe. Spika, nasikia kuna watu wanayo mitambo wengine wanatengenezea sehemu tofauti lakini nyengine ni *fake* na tunapoteza mapato kweli. Mhe. Spika, nimesema na *Attorney General* amesema kwamba kila tukiitengeneza sheria ya kodi kuna watu wanajaribu kutengeneza njia za kukwepa, kwa hiyo hili lisitupe wasi wasi sana.

Jambo jengine Mhe. Spika, niliulizwa hapa katika kodi hizi zitachangia kiasi gani. Katika hotuba yangu nimeeleza kila kodi itaongeza mapato kiasi gani. Kwa hiyo, ukifungua kuanzia ukurasa nafikiri 36 kama hivi kila kodi nimeeleza hii inaongeza kiasi gani na kodi ambazo hazitaongeza kitu, lakini zitasimamia ukwepaji utakuwa haupo nimeeleza na hizi tulikuwa na mapato ya nyuma na hivi sasa hazitaongeza kitu, isipokuwa zitasimamia na ukwepaji utakuwa haupo nimeeleza marekebisho hayo.

Mhe. Spika, marekebisho haya ya sheria tumerekebisha sheria 10 na tumezirekebisha kwa mujibu wa muono wa sisi ambao tumeuona zaidi ni yale ambayo Waheshimiwa Wawakilishi wameyataka au wameyaeleza kwamba tusimamie katika suala hili.

Pia kuna suala ambalo limezungumziwa hapa na Mhe. Mwanasheria Mkuu amelieleza kwamba *ZIPA* ipewe mamlaka wale ambao watakaozikimbia zile hoteli zao au zile *investment* zao nipewa mamlaka ya kuziuza. Nataka niseme tu *ZIPA* inayo mamlaka hayo lakini mamlaka iliyonayo *ZIPA* ni lazima ifuate utaratibu wa kisheria, *AG* ameeleza hapa. Sasa ule utaratibu wake kwa sababu unataka kila pande uipe haki ndio inachukua muda kidogo.

Mimi nataka niwashukuru sana ndugu zangu hawa wanasheria kwa kulisimamia lile suala la *VENTA* kama alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu kwamba sasa linakaribia tamati na tukipata uamuzi tu, na napenda nikwambieni Waheshimiwa kuna wateja tayari wameshajitokeza wanataka kulinunua lile eneo ili pesa ipatikane walipwe hawa wanaodai wananchi,

milioni mia saba na ngapi sijui *AG* anasema wananchi wanadai. Kwa hivyo hiyo ipo.

Jengine ambalo limezungumzwa vile vile bado nataka niwanasihi ndugu zangu wanaopiga kelele kuhusu habari ya *single importer* kwa mafuta. Sisi tukifanya jambo tunataka tufanye jambo la uhakika, hasa mimi. Mimi sipendi kufanya jambo ambalo si la uhakika, tunataka tuandae *study*, tutaandaa *study* ndogo itakayotuonesha *position* ya Zanzibar na uuzaji wa mafuta. Mimi nataka nikwambieni wala sio soko la ndani, soko la ndani sina zile takwimu sahihi. Lakini nadhani kwa mwaka kama *metrics tonnes* milioni tano au sita kwa soko la ndani, sisi tuna *focus* masoko ya jirani. Nimetoa mfano ndugu zanguni, Mombaza/Kenya hawana hata lita moja wanayozalisha mafuta, kaangalie katika *statistics of export*, Kenya wanakwambia wana *export oil*. Angalia *statistics* zao na Tanzania, Zanzibar tunakwenda tunanunua pale, ndugu zetu wa Comoro wanakwenda kununua pale na nchi yengine.

Zanzibar iko kwenye *position* nzuri zaidi ndugu zanguni. *Who's important* ambaye sisi ndiye tunayemtafuta sasa hivi wa kuweka matangi makubwa sana hilo ndio lengo letu. Nimesema wapo wanne mpaka sasa hivi hajaniambia hata mmoja kwamba anajiondoa, watatu wa nje na mmoja *local*, hakuna hata mmoja aliyesema kwamba anajiondoa. Lengo letu ni zuri na wala tusiogope kwenye malengo mazuri. Hata hawa tukiwaachia wanaoleta tani tano, tani kumi wanaoleta kwa boti ndogo ndogo, akija yule akileta tani nyingi yule atakuwa na bei nafuu zaidi kuliko hawa, hawa wataondoka wenyewe.

Kwa hivyo hapa tusiwe tunababaika, tusubirini *study* itakavyotuelekeza lakini tunakwambieni tu kwamba lengo letu ni hilo Zanzibar ni kisiwa, kazi yake kuuza huduma, wenzetu Dubai hawazalishi mchele hata robo kilo, lakini wana *export* mchele, wanaleta *tons and tons from Pakistan or India*, wanaumwaga pale watu wote wananunua kutoka pale kwa sababu ya *strategic location* ya Dubai ilivyo. Kwa hivyo na sisi tuko huko jamani.

Suala la kodi ya ardhi limeshazungumzwa na Mwanasheria Mkuu sina haja ya kulirudia. Suala la kodi za hoteli zimeshazungumzwa na Mwanasheria Mkuu na mimi nimeligusia. Mhe. Spika, Mhe. Mwanasheria Mkuu amelizungumzia na hii ilikuwa ni wasi wasi wa baadhi yetu tunamuachia Kamishna kutoa tafsiri. Ile kisheria ni *practice* amelieleza Mwanasheria Mkuu lakini na mimi najaribu kuongeza tu. Huyu kwa sababu yeye ndiye anayesimamia masuala ya kodi, yeye ataeleza zaidi tafsiri ya lile jambo. Lakini kama alivyosema Mwanasheria Mkuu mlipa kodi halazimiki wala hafungiki kukubaliana na tafsiri yake. Anaweza akenda Mahakamani akasema tafsiri hii siikubali akaiomba Mahakama sasa itoe tafsiri, na wale tumesema watajifunga na tafsiri yao na ile tafsiri itakuwa *gazetted* katika gazeti rasmi la serikali ili

isiwe kila Kamishna anayekuja, ndugu yangu Mhe. Salma Mussa Bilal alikuwa anataka kujua Kamishna gani. Kamishna wa *ZRB*, isiwe kila Kamishna anayekuja anakuja na tafsiri yake. Lakini yule mlipakodi hafungiki na tafsiri iliyotolewa pale.

Nadhani Mhe. Spika, nimemaliza yale yote ambayo niliyoulizwa na namshukuru na Mhe. *AG* naye amenisaidia sana. Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima sasa naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Basi baada ya hapo Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri juu ya Mswada huu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, baada ya maelezo yangu sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya kutunga sheria ili kuupitia Mswada huu kigungu baada ya kifungu. Naomba kutoa hoja.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Fedha, Usimamizi wa Mapato ya Mwaka 2013

Sehemu ya Kwanza
Utangulizi

Kifungu 1 Jina Fupi na Tarehe ya Kuanza Kuanza Kutumika

Sehemu ya Pili
Marekebisho ya Sheria ya Ada ya Bandari Nam. 2 ya Mwaka 1999

Kifungu 2 Kusomwa Pemba na Marekebisho Yake

Kifungu 3 Marekebisho ya Kifungu cha 10 pamoja na marekebisho yake

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Spika, niliposimama kuchangia nilisema hivi, kifungu cha 10 cha sheria mama kinarekebishwa kama ifuatavyo kwa

kufuta kifungu kidogo cha 3 na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha 3 kama ifuatavyo:-

“Bila ya kujali sheria yoyote ikayokwenda kinyume na sheria hii, Kamishna kwa amri ya maandishi anaweza kumteua mtu yeyote anayeongoza, anayesimamia, anayedhibiti, au mwenye mamlaka”.

Mimi nitasema hapa ingekuwa *vizuri* tungesema anadhibiti haitokuwa vizuri kusema mwenye mamlaka, lakini tungesema mwenye mamlaka ya kisheria, kushughulikia bidhaa au abiria wa meli yoyote. Nikasema hapa vile vile haiwezekani kwa mujibu wa mwalimu wangu wa kiswahili alivyoniambia kwamba huwezi kusema kwamba meli yoyote unaweza kusema kwamba mtu yoyote sio mtu yoyote.

Vile vile meli yoyote au ndege kwenye bandari yoyote, kwa hivyo hapa nikasema kunataka masahihisho. Vyenginevyo labda kuwe na mtu yeyote kwenye bandari yoyote lakini isiwe meli yoyote. Kwa hivyo Mhe. Spika, hapa Waziri hajanifafanulia kifungu hichi kwamba mimi nilitaka kiwe na marekebisho kwamba baada ya kuwa meli yoyote au bandari yoyote hapa yafanywe marekebisho juu ya marekebisho ambayo yamefanywa na wenye viti lakini hapa bado.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimuombe radhi mheshimiwa kweli alizungumza hilo kwa sababu hicho ndicho kiswahili fasaha alichokisema yeye. Mimi nakubaliana naye.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Kifungu 3 Marekebisho ya Kifungu cha 10 Pamoja na Marekebisho Yake.

Sehemu ya Tatu
Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Hoteli Nam 1 ya Mwaka 1995

Kifungu 4 Kusomwa Pamoja na Marekebisho Yake

Kifungu 5 Marekebisho ya Kifungu cha Tatu

Kifungu 6 Kuongeza Kifungu Kipya cha 14 Pamoja na Marekebisho Yake

Sehemu ya Nne

Marekebisho ya Kodi ya Mafuta Nam. 7 Mwaka 2011

Kifungu 7 Kusomwa

Kifungu 8 Kutozwa Kodi Pamoja na Marekebisho Yake

Kifungu 9 Kufutwa na Kuandikwa Upya Kifungu cha 8(a)Kifungu Kidogo cha (1) Pamoja na Marekebisho Yake

Kifungu 10 Kufuta na Kuweka Kifungu Kidogo Kipya cha 10(a) Pamoja na Marekebisho Yake.

Sehemu ya Tano

Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Stemp Nam. 6 ya Mwaka 1996

Kifungu 11 Kusomwa

Kifungu 12 Marekebisho ya Kifungu cha 3

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia Kifungu Nam. 3 kimesema kwamba uamuzi wa serikali utakuwa mwananchi kumbana kwenye kodi hii. Nilisema kwamba kifungu hichi kitawabana sana wananchi wanyonge wa nchi hii. Nataka maelezo, Kifungu cha 12 cha Sheria ya Kurekebisha kama ifuatavyo, kubadilisha vifungu vidogo vidogo kwa mujibu wa masharti ya sheria zitokanazo na kodi inayojulikana kama ni kodi ya stemp. Kwenye usambazaji wa bidhaa, huduma unaofanywa Zanzibar, mlipa kodi katika uendeshaji wa biashara unaofanywa na mlipa kodi husika.

Mhe. Spika: Sema basi, ufahamike ulichangia sasa iwe vipi?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hii kodi itamuumiza mwananchi anayekwenda kununua bidhaa dukani na si kupata ufumbuzi wakati alipokuwa anajibu swali Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwakilishi anasema kwamba kitambana mwananchi. Sasa mimi sioni kitambanane mwananchi? Kwa sababu hapa tunazungumza kodi ya stemp sijaona kitambanaje mwananchi. Sasa labda angetusaidia kutoa ufafanuzi yeye anakusudia nini hasa, kwa sababu mimi bado sijapata *point* yake.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba kama hichi kifungu kama kitawezekana akiondoshe, kinambana mwananchi anayekwenda kununua bidhaa hii dukani.

Mhe. Spika: Kwamba Kodi ya stemp iondoshwe?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Iondoshwe.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, hebu niwaombe Waheshimiwa Wajumbe kwamba tufahamiane, kodi yoyote ambayo serikali inawekwa mlipa kodi ile ni mwananchi. Sasa atakaposema kodi hii iondoshwe kwa sababu inambana mwananchi. Kwanza mimi sijaona kwamba mwananchi inambana wapi. Lakini anaposema kwamba kodi hii iondoshwe ana mbadala kwamba kodi hiyo nyengine tuiweke wapi. Sasa atusaidie mheshimiwa, tunatunga sheria hapa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 12 Marekebisho ya Kidungu cha 3 Pamoja na Marekebisho Yake

kifungu 13 Kuongeza Kifungu kipya cha 4

Kifungu 14 Kufutwa Kifungu cha 3(b)

Kifungu 15

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kwa madhumuni sheria mbali mbali zinazohusu marekebisho kwa lengo la usimamizi mzuri wa kodi kifungu hichi kimemtaka Waziri aweze kutunga Kanuni kwa ajili ya kusimamia kodi. Mhe. Waziri alinijibu vizuri lakini ili kutoa mfano mzuri kwa serikali kwamba yeye ni Waziri makini anayetafuta uchumi wa nchi na kwa sababu wapo mawaziri ambao kanuni hutungwa baada ya miaka mitatu tukaathirika, atwambie Mhe. Waziri basi muda gani hizi kanuni atakamilisha ili sheria hii iende sambamba na ukusanyaji wa mapato. Kwa sababu wasi wasi wangu asije akafuata mawaziri wengine miaka mitatu, miaka minne hajaitunga, atwambie basi ni muda gani kanuni itakamilishwa ili mapato ya Waziri wa Fedha aweze kuyatia katika mfuko wetu wa serikali.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, mimi naamini Wawakilishi wako ni Wawakilishi makini sana. Moja ambayo hoja ya Mhe. Hija Hassan Hija

mdogo wangu ameliuliza amenitaka ni kutumia kipindi cha miezi sita kukamilisha kanuni. Nataka basi nimuhakikishie kwamba sitochukua muda mrefu. Yeye anataka niwe katika muda wa miczi sita, lakini namwambia kwa sababu kanuni huwa siandiki, mimi kanuni huwa wanaziandika kitaalamu, wanampelekea Waziri anazipitia. Lakini namwambia katika kipindi cha mwaka huu wa fedha basi nitahakikisha kwamba kanuni hizi tumezikamilisha.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nimemuelewa Mhe. Waziri lakini kwa sababu sheria hii inatakiwa ianze Julai mosi kukushanya mapato. Nakusudia kwamba tuna *hansard record* kwamba yeye ametuahidi kwamba mwaka huu hii kazi itatekelezeka ili mwakani tukijaaliwa 2014/2015 asije akatupa lugha kwamba sikukusanya mapato kwa sababu ya kanuni. Namuamini na kwa hivyo tuendelee lakini *hansard* imesha *record* kwamba atafanya kazi hii haraka haraka.

Mhe. Spika: Tunaendelea isipokuwa naomba tu kazi hiyo ifanyike haraka ili usije ukakwamisha katika kutekeleza sheria hii.

Kifungu cha 15 Kuongezwa kwa Kifungu Kipya cha 34 Pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Sita

Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Nam. 4 ya Mwaka 1998

Kifungu 16 Kusomwa

Kifungu 17 Marekebisho ya Kifungu cha 16

Kifungu 18 Marekebisho ya Kifungu cha 74

Sehemu ya Saba

Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi Nam. 7 ya Mwaka 2009

Kifungu 19 Kusomwa

Kifungu 20 Marekebisho ya Kifungu cha 5

Mhe. Spika: Nimearifiwa kwamba marekebisho ya hapa ni kwamba hichi kifungu kimefutwa.

Kifungu 21 Marekebisho ya Kifungu cha 15 Pamoja na Marekebisho Yake

Kifungu 22 Marekebisho ya Kifungu cha 18 Pamoja na Marekebisho Yake

Kifungu 23 Marekebisho ya Kifungu cha 18 Pamoja na Marekebisho Yake

Kifungu 24 Marekebisho ya kifungu cha 32 Pamoja na Marekebisho Yake

Kifungu 25 Marekebisho ya Kifungu cha 45 Pamoja na Marekebisho Yake

Kifungu 26 Kuongezwa Vifungu Vipya Vya 46(a)(b)(c) Pamoja na Marekebisho Yake.

Kifungu 27 Ukurasa wa Tisa Kifungu cha 27 Kufutwa na Kuandikwa Upya Kifungu 52 Pamoja na Marekebisho Yake.

Kifungu 28 Marekebisho ya Kifungu cha 53 Pamoja na Marekebisho Yake

Sehemu ya Nane
Marekebisho ya Sheria ya Rufaa ya Kodi Nam. 1 ya Mwaka 2006

Kifungu 29 Kusomwa Pamoja na Marekebisho Yake

Kifungu 30 Marekebisho ya Kifungu cha 3 Pamoja na Marekebisho Yake

Kifungu 31 Marekebisho ya Kifungu cha 16 Pamoja na Marekebisho Yake

Sehemu ya Tisa

Marekebisho ya Sheria ya Umiliki wa Ardhi Nam. 12 ya Mwaka 1992

Kifungu 32 Kusomwa Pamoja na Marekebisho Yake

Kifungu 33 Marekebisho ya Kifungu cha 47 Pamoja na Marekebisho Yake

Sehemu ya Kumi

Marekebisho ya Sheria ya Usafiri Barabarani Nam. 7 Mwaka 2003

Kifungu 34 Kusomwa Pamoja na Marekebisho Yake

Kifungu 35

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nikiri kwamba Mhe. Waziri hapa amefanya vizuri na bila ya shaka nia ya serikali ni nzuri kwamba lengo ni kudhibiti magari yanayoingia nchini ili kuondosha mapato kupotea na uhalifu na mambo mengine. Mhe. Waziri ametwambia kwamba ataweka usajili tofauti, gharama tofauti kati ya wale wanaotumia ndani na wale wanakuja kwa ajili ya biashara na amesema kutakuwa na tofauti ya bei. Sasa tofauti ya bei inaweza ikawa ni shilingi elfu moja, inawezekana ni shilingi mia tatu. Lengo nakusudia kwamba tumlinde yule anayeingia kibiashara ili asije akaathiri soko la ndani na soko la nje.

Sasa Mhe. Waziri atwambie tofauti itakuaje kati ya wale wanaingiza kibiashara na mimi niliyeingiza kwa ajili ya matumizi ya ndani. Lengo langu ni kwamba yule anaingiza kibiashara kwa maana ya kufanya *transit* basi bei yake ni ndogo zaidi kuliko yule anayetumia. Sasa labda Mhe. Waziri atwambie kwamba tofauti itakuwaje.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, ndugu yangu Mhe. Hija Hassan Hija mimi napenda sana, hili suala kanishtukizia tu sikuwa na ile *figure* hasa. Lakini kama nilivyosema kwamba kutakuwa kuna tofauti kwa sababu yule ambaye gari lake litaingia ndani kwa kufanya matumizi ya ndani atakuwa na *registration* ya ndani, kwa hivyo kutakuwa kuna kodi maalum. Yule ambaye gari lake litakuwa ni *transit* kwa maana ya kwamba linakwenda kufanya biashara nje ya Zanzibar. Yeye kwa sababu ya kudhibiti kwamba lile gari lisitumike vibaya ile *plate number* atakayopewa itakuwa ni tofauti na bei yake nataka nimwambie itakuwa ni tofauti.

Sasa sikumbuki itakuwa tofauti kiasi gani lakini pengine labda kwa sababu si suala la kisheria ambalo limo humu ndani kwamba lazima nijibu bei humu ndani naweza nikamtafuta baadae nikamwambia itakuwa ni tofauti kiasi gani.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ismail Jussa ananiambia Mhe. Waziri ananipenda na baadae ananitafuta. Sasa ninahofu kidogo kwa sababu ni mchanga lakini Mhe. Mwenyekiti, nimeelewa malengo ya serikali na bila shaka ni mazuri naomba tu kwa busara ya serikali kwamba hawa

ambao wanaingiza kibiashara wasije wakakomolewa kusudi waje wakakimbia ndani ya nchi wakenda sehemu nyengine wakatuathiri kimapato. Naomba Mhe. Waziri alizingatie hilo. tuendelee.

Kifungu 35 Marekebisho ya Kifungu cha 27 Pamoja na Marekebisho Yake

Kifungu 36 Marekebisho ya Kifungu cha 29 Pamoja na Marekebisho Yake

Sehemu ya Kumi na Moja

Marekebisho ya Sheria ya Ukuzaji wa Vitega Uchumi Nam. 11 ya Mwaka 2004

Kifungu 37 Kusoma Pamoja na Marekebisho ya Yake

Kifungu 38 Marekebisho ya Kifungu cha 19 Pamoja na Marekebisho Yake

Kifungu 39 Marekebisho ya Kifungu cha 20 Pamoja na Marekebisho Yake

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia Mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na Marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wanaokubaliana na Mswada pamoja na marekebisho mbali mbali wanyanyue mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshindwa. (*Makofi*).

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Fedha, Usimamizi wa Mapato ya Mwaka 2013

(Kusomwa kwa mara ya tatu)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Fedha na Usimamizi wa Mapato ya Mwaka 2013, usomwe kwa mara ya tatu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji basi Waheshimiwa Wajumbe wanaokubaliana na Mswada kusomwa kwa mara tatu, wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa sheria ya Serikali ulisomwa kwa mara ya tatu na kupitishwa)

TAARIFA

Mhe. Spika: Waheshimiwa nafikiri kwa mujibu wa orodha ya shughuli za leo hii ndio shughuli yetu ya mwisho, kwa hiyo kabla ya kusitisha shughuli zetu naomba nitoe taarifa ya maombi ambayo inasomeka kama ifuatavyo.

Waheshimiwa Wajumbe nimeletewa maombi na nikasema maombi haya niyawasilishe kwenu Waheshimiwa Wajumbe ili tuyatafakari kwa pamoja na hatimaye niwaombe tutelekeze hilo ombi ambalo limo katika taarifa hii.

Waheshimiwa Wajumbe napenda kukujulisheni kuwa wadau wa michezo hapa Zanzibar wameona umuhimu wa kuwaenzi wanamichezo wa zamani wa Zanzibar kwa michango yao adhimu katika kuitangaza kwa kuipatia sifa Zanzibar ndani ya nje ya nchi, akiwemo mwana Michezo maarufu Bwana Abdul Majiham.

Ili kufanikisha azma hiyo kuna mfuko maalum umeanzishwa na uzinduzi wake utatangazwa moja kwa moja na vyombo vya habari. Mgeni wa heshma katika usinduzi huo atakuwa Mhe. Mohammed Aboud Mohammed (Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais).

Kwa hivyo kwa barua hii Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar timu ile ya wanamichezo ambayo ni timu yetu, juzi tu tuliitangaza

kwamba ni mahiri sana imetuletea ushindi. Inatuomba tujitahidi na kufanya hima kuuchangia mfuko huo, watakaochangia watatangazwa rasmi.

Barua hii ambayo tumeombwa Waheshimiwa Wajumbe kupitia kwangu imetiwa saini na Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi Sport Club hapa Zanzibar ambaye ni Mhe. Hamza Hassan Juma. Kwa hivyo ipo orodha tayari hapa Waheshimiwa Wajumbe wakati umekuwa ni mkubwa kidogo lakini nategemea siku ya kesho itazungushwa kwenu. Niwaombe basi kesho mifuko yetu tuitayarishe mapema ili mfuko huu tuujaze fedha kwa ajili ya kuwaenzi wana michezo wetu si tu huyu Bwana Abdul Majiham lakini pamoja na wachezaji wengine wote. Ndio maana mfuko huo ukaanzishwa na wapo baadhi ya wajumbe ambao hawataki watajwe tayari wameahidi watatoa mchango mkubwa sana, imani yangu wakiongozwa na Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo.

Kwa hivyo natoa ombi rasmi kwa niaba ya timu yetu ya michezo ya Baraza la Wawakilishi kuchangia na kuwaenzi wanamichezo wetu hawa wa zamani. Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni. *(Makofi).*

Makofi haya yanaashiria kwamba tupo tayari kuuchangia mfuko huo ahsanteni sana. Waheshimiwa Wajumbe basi sasa tusitishe shughuli zetu na tuakhirishe kikao hichi hadi kesho tarehe 21/06/2013, saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 12:34 jioni Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 21/06/2013 saa 3:00 za asubuhi)